# KUCHUNGUZA DHAMIRA YA UKOMBOZI KATIKA RIWAYA YA KUSADIKIKA NA VUTA N'KUVUTE: UTAFITI LINGANISHI

**ASHA KHALFAN SULEIMAN**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA IKIWA NI SEHEMU YA MASHARTI YA KUPATIA SHAHADAYA UZAMILI YA KISWAHILI (M.A.KISWAHILI FASIHI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2019**

## UTHIBITISHO

Aliyeweka saini hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma tasnifu hii iitwayo: ***Kuchunguza Dhamira ya Ukombozi katika Riwaya ya Kusadikika na Vuta N'kuvute: Utafiti Linganishi***; na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya Shahada ya Uzamili (M.A Kiswahili) ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania

**………………………………………**

**Profesa Emmanuel Mbogo**

**(Msimamizi)**

**………………………………..**

**Tarehe**

## HAKIMILIKI

Haki zote za kunakili, kuiga au kuchukua sehemu ya tasnifu hii zimehifadhiwa kisheria. Hairuhusiwi kwa mtu yoyote kunakili au kuiga tasnifu hii bila idhini yangu au kibali cha maandishi kwa niaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

# IKIRARI

Mimi **Asha Khalfan Suleiman** nathibitisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu halisi na kwamba haijawahi kuwasilishwa na haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kinginekwa ajili ya Digirii yoyote.

**……………………………**

**Saini**

**…………………………**

**Tarehe**

## TABARUKU

Natabaruku kazi hii kwa mama yangu mpendwa Zuhura Hamad Khatib, na kaka zangu Suleiman Khalfan Suleiman na Issana Hemed Khalfan Suleiman. Pia dada zangu watiifu Salma,Fatma, Tamima, Khadija Khalfan Suleiman na mdogo wangu mpenzi Halima.Wote nawatakia furaha,upendo,uzima na mafanikio mema katika maisha yenu. Allah awajaze kheri na neema.Aamin.

## SHUKURANI

Kwanza kabisa, kabla sijenda mbele ni vyema kushukuru kwa Mwenyezi Mungu(S.W) na kumtakia rehma mtume wetu Muhammadi (S.A.W) kwa kuniwezesha mimi nikiwa katika hali ya uzima wa afya.Akanitunikia uwezo,akili na maarifa yakuweza kupambanua na kufafanua mambo ya kielimu hasa katika ngazi hii hadi kufikia kilele cha masomo yangu.

Pili, napeleka shukurani zangu za dhati kwa wazazi wangu kwasababu wao ndio walionilea na kunisomesha kuanzia elimu ya awali hadi ngazi ya juu bila ya kujali vikwazo na shida za maisha zilizowakabili katika kunitafutia mahitaji yangu yalazima.

Tatu, nazidisha shukurani zangu kwa wingi kwa mume wangu mpenzi kwasababu yeye ni kiwakilishi kikubwa anayenisaidia kwa hali na mali katika utekelezaji na uwajibikaji wa kazi hii licha ya majukumu yaliyomkabili ili kuhakikisha ninamaliza salama katika masomo yangu haya ya uzamili.

Hata hivyo, natoa shukurani zangu za dhati kwa Msimamizi wangu Profesa Emmanuel Mbogo. Profesa Mbogo amekuwa ni msimamizi na muelekezaji mahiri wa kazi hii asiyechoka kuanzia masomo ya darasani hadi katika ukamilishaji wa tasnifu hii.Mwengine ni Daktari Omar Muhamedi Maguo ambaye alinisomesha kwa juhudi na bidii zake zote alizojaaliwa ili kuhakikisha, naielewa vyema mada ya utafiti ambayo ndio kiungo cha kuhitimu ngazi hii ya elimu. Ni imani yangu kubwa kwa walimu hawa na wengineo niliokuwa sijawataja nitaendelea kufurahia matunda ya maarifa yao na kuahidi kuyatumia vizuri na kwa mafanikio makubwa. Nawaombea kwa Mungu wazidi kufanikiwa. Amiin.

Kwa upande wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, tawi la Pemba, natoa shukrani zangu za pekee kwa uongozi mzima wa chuo akiwemo mwalimu Nassor Ali Suleiman na mwalimu Bakari Kombo Bakari kwa msaada wao hasa wa kitaaluma. Maelekezo, ushauri, nasaha zimenifanya nifaulu vizuri kimasomo na hata kimaarifa.Nashukuru nimejifunza mingi kutoka kwao.Naamini kwa rehma za Allah (sw) hawataniacha nyuma na wataendelea kuniongoza vyema.

Napenda kutoa shukurani zangu za dhatikwa mwalimu Sharif Juma Fakih. Mwalimu huyu amekuwa msaada mkubwa wa masomo yangu tangu awali, alinielekeza mambo mengi ambayo hapo awali sikuwahi kuyajua. Msaada wake hasa wa kitaaluma aliutoa kwa moyo safi na wakati wote bila kuchoka na bila ya upendeleo na khiyana. Alinitia hamasa ya kusomakwa bidii bila ya kukata tamaa pamoja na wanafunzi wenzangu. Ametuhimiza kusoma kwa upendo, umoja na mashirikiano baina yetu na kutuaminisha mafanikio makubwa.

Mbali na mwalimu Sharif, shukran zangu zimfikie mwalimu mwenzangu na kiongozi wetu wa kundi la Shahada ya Uzamili, mwalimu Hemed Said Massoud kwa ushauri, mashirikiano, usimamizi na ufatiliaji wake katika masomo haya. Bila kuwasahau wanafunzi wenzangu ambao baadhi yao ni Safia Said Massoud, Asha Rashid Abdalla, Zaina Omar Othman, Ali Haji Vuai, Nassor Rashid, Maryam Said Massoud, Ziada Ali Hamad na wengineo. Kwa ujumla nawashukuru wale wote walionisaidia kwa hali zote, natambua ni wengi na naomba radhi kwa kutowataja. Namuomba Mungu awajaalie Baraka na neema katika maisha yenu wote. Amiin.

## IKISIRI

Lengola utafiti huu ni ***Kuchunguza Dhamira ya Ukombozi katika Riwaya ya Kusadikika na Vuta N'kuvute: Utafiti Linganishi.*** Ili kukamilisha lengo hili, utafiti huu ulikuwa na malengo mahsusi matatu ambayo ni: (i) Kubainisha dhamira za ukombozi ilivyojitokeza katika riwaya ya *Kusadikika*. (ii) Kubainisha dhamira za ukombozi ilivyojitokeza katika riwaya ya *Vuta N'kuvute*. (iii) Kufanana na kutafautianaa dhamira zilizobainishwa katika riwaya zilizoteuliwa. Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu za usomaji makini na upitiaji wa nyaraka maktabani. Mkabala wa kimaelezo, sambamba na nadharia za Mwitiko wa Msomaji na Fasihi Linganishi ndizo zilizotumika katika kuchambua data za utafiti.Matokeo ya utafiti yamebaini kuwa dhamira ya ukombozi imejitokeza katika hoja mbalimbali kama vile kujitolea muhanga, subrana uvumilivu, umoja na ushirikiano na nyenginezo katika riwaya teule. Vile vile, matokeo ya utafiti huu yamebaini kuwa kuna dhamira zilizofanana na kutafautiana katika riwaya teule kutegemeana sababu na mazingira yaliyomzunguka mtunzi. Dhamira ya Ukombozi inayoakisi kufanana ni pamoja kujitolea mhanga, kuwa na msimamo na umoja na mashirikiano. Kwa upande wa kutofautiana ni pamoja na mapenzi na ndoa, hekima na busara. Kwa ujumla riwaya ya *Kusadikika* na*Vuta N'kuvute* ni katika riwaya adhimu zenye kuakisi uhalisia wa dhamira ya ukombozi kama ambavyo mtafiti amechambua ndani ya tasnifu hii.

## YALIYOMO

UTHIBITISHO ........................................................................................................ ii

HAKIMILIKI......................................................................................................... iii

IKIRARI …. ......................................................................................................... iv

TABARUKU .......................................................................................................... v

SHUKURANI ......................................................................................................... vi

IKISIRI ….. ......................................................................................................... viii

YALIYOMO ........................................................................................................... ix

ORODHA YA VIFUPISHO ..................................................................................... xviii

ORODHA YA MAJEDWELI ..................................................................................... xix

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI WA UJUMLA ........................................ 1**

1.1 Utangulizi ........................................................................................... 1

1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti ......................................................................... 2

1.3 Tatizo la Utafiti.......................................................................................... 5

1.4 Malengo ya Utafiti....................................................................................... 5

1.4.1 Lengo Kuu ........................................................................................... 6

1.4.2 Malengo Mahsusi ..................................................................................... 6

1.5 Maswali ya Utafiti ....................................................................................... 6

1.6 Umuhimu wa Utafiti...................................................................................... 6

1.7 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi wake ......................................................... 7

1.8 Mipaka ya Utafiti........................................................................................... 8

1.9 Muundo wa Utafiti ....................................................................................... 9

1.10 Hitimisho ................................................................................................ 11

**SURA YA PILI: MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA ........ 12**
2.1 Utangulizi ........ 12
2.2 Ufafanuzi wa Istilahi mbalimbali ........ 12
2.2.1 Dhana ya Riwaya ........ 12
2.2.2 Dhana ya Dhamira ........ 13
2.2.3 Dhana ya Ukombozi ........ 14
2.3 Mapitio ya Kazi Tangulizi ........ 14
2.3.1 Mapitio ya Kazi Tangulizi kuhusu Riwaya za Shaaban Robert ........ 15
2.3.2 Mapitio ya Kazi Tangulizi kuhusu Riwaya za Shafi Adam Shafi ........ 18
2.4 Mkabala wa Kinadharia ........ 19
2.4.1 Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji (Upokezi) ........ 20
2.4.1.1 Historia fupi ya Nadharia ya Upokezi na Waasisi wake ........ 20
2.4.1.2 Mihimili ya Nadharia ya Upokezi ........ 21
2.4.2 Nadharia ya Fasihi Linganishi ........ 24
2.4.2.1 Chimbuko la Nadharia ya Fasihi Linganishi na Waasisi wake ........ 25
2.4.2.2 Mihimili / Misingi ya nadharia ya Fasihi Linganishi ........ 28
2.5 Hitimisho ........ 30

**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI ........ 31**
3.1 Utangulizi ........ 31
3.2 Mbinu za Utafiti ........ 31
3.3 Eneo la Utafiti ........ 32
3.3.1 Uteuzi wa Eneo la Utafiti. ........ 32

3.3.2 Sababu za Uteuzi wa Eneo la Utafiti ..................... 33

3.4 Usanifu wa Utafiti ..................... 33

3.5 Kundi lengwa ..................... 34

3.6 Sampuli na Usampulishaji ..................... 34

3.7 Aina za data ..................... 35

3.7.1 Data za msingi (awali) ..................... 35

3.7.2 Dataza upili ..................... 36

3.8 Ukusanyaji wa data ..................... 37

3.8.1 Mbinu za Ukusanyaji wa Data ..................... 37

3.8.2 Mbinu ya Maktabani kupitia Usomaji Makini ..................... 38

3.8.3 Upitiaji wa Nyaraka ..................... 38

3.9 Mbinu za Uchambuzi wa Data ..................... 38

3.9.1 Mkabala wa Kimaelezo ..................... 39

3.10 Usahihi wa Data za Utafiti ..................... 40

3.11 Kuaminika kwa Data ..................... 40

3.12 Maadili ya Utafiti ..................... 40

3.13 Hitimisho ..................... 41

**SURA YA NNE : UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA UTAFITI ..................... 42**

4.1 Utangulizi ..................... 42

4.2 Historia ya Shaaban Robert kwa Ufupi ..................... 42

4.2.1 Uwandishi na Kazi zake ..................... 44

4.2.2 Falsafa yake ..................... 44

4.2.3 Kifo na Kumbukumbu ........ 45

4.3 Historia fupi ya Shafi Adam Shafi ........ 45

4.3.1 Uwandishi wake ........ 46

4.4 Muhtasari wa Riwaya ya *Kusadikika* ya Shaaban Robert ........ 47

4.5 Muhtasari wa*Vuta N'Kuvute*ya Shafi Adam Shafi ........ 50

4.6 Kubainisha Dhamira za Ukombozi katikaRiwaya ya Kusadikika ........ 55

4.6.1 Ukombozi waKifikra ........ 55

4.6.1.1 Kufikiri mbinu za Kukomboa Nchi ........ 56

4.6.1.2 Fikra ya Kuikomboa Nchi ........ 57

4.6.1.3 Fikra za Kutafuta Mawazo ya Wananchi ........ 58

4.6.1.4 Fikra ya Kuanzisha Elimu ya Uanasheria ........ 60

4.6.1.5 Fikra za Wajumbe ........ 61

4.6.2 Ukombozi wa Kielimu ........ 62

4.6.2.1 Umuhimu wa Elimu ........ 62

4.6.2.2 Elimu bora ........ 64

4.6.3 Ukombozi wa Kiuchumi ........ 65

4.6.3.1 Kilimo bora ........ 65

4.6.3.2 Kuboresha Ufugaji ........ 66

4.6.3.3 Kufanya kazi kwa bidii ........ 67

4.6.3.4 Kuondosha uvivu ........ 68

4.6.3.5 Kuondosha umaskini ........ 69

4.6.4 Ukombozi wa Kisiasa ........ 70

4.6.4.1 Namna ya kuendesha siasa bora ........ 70

4.6.4.2 Ulafi wa madaraka ........ 72

4.6.4.3 Kuondosha uhasama ........ 73
4.6.4.4 Fursa ya kujitetea ........ 73
4.6.4.5 Kuwatowa wafungwa ........ 74
4.6.4.6 Kujenga hoja za wajumbe ........ 75
4.6.4.7 Utetezi wa haki za binaadamu ........ 76
4.6.4.8 Kupunguza vifo ........ 77
4.6.4.9 Subra ........ 78
4.6.4.10 Uvumilivu ........ 79
4.6.4.11 Ushujaa ........ 80
4.6.4.12 Ujasiri ........ 81
4.6.4.13 Kutokata Tamaa ........ 82
4.6.4.14 Kujitolea Muhanga ........ 83
4.6.4.15 Uzalendo ........ 84
4.6.4.16 Kuondoa vita na chuki ........ 86
4.6.4.17 Viongozi wawapende raia zao ........ 87
4.6.4.18 Kuendesha nchi kimabavu ........ 88
4.6.4.19 Kuhubiri amani ........ 89
4.6.5 Ukombozi wa kijamii ........ 90
4.6.5.1 Makaazi bora ........ 90
4.6.5.2 Maji safi na salama ........ 91
4.6.5.3 Umiliki wa mali ........ 92
4.6.5.4 Uharifu wa mali za umma ........ 93
4.6.5 .5 Kuondosha chuki na uadui ........ 94
4.6.5.6 Upapiaji wa mali ........ 95

4.6.5. 7 Barabara safi na salama ........................................................................ 96

4.6.5.8 Matibabu bora........................................................................................ 96

4.6.5.9 Kuwepo kwa vyombo vya usafiri........................................................ 97

4.6.5.10 Kuikomboa nchi kutokana na utabaka ................................................ 98

4.6.5.10.1 Kujitukuza na kujisifu kwa baadhi ya viongozi .................................. 99

4.6.5.10.2 Kuepuka Kibri ...................................................................................... 99

4.6.5.10.3 Kutojiona bora..................................................................................... 100

4.6.5.10.4 Kuepuka dharau na kejeli .................................................................. 101

4.6.5.11 uwakomboa wanawake na watoto ..................................................... 102

4.6.5.12 Haki ya kupata elimu......................................................................... 102

4.6.6 Hitimisho ........................................................................................... 104

4.7 Kubainisha Dhamira za Ukombozi katika riwaya ya Vuta N'kuvute .. 105

4.7.1 Ukombozi wa Kiutamaduni............................................................... 105

4.7.1.2 Kuvunja Ndoa yake kwa Bw.Raza .................................................... 105

4 .7.1.3 Kujiunga katika Ngoma za Waswahili ............................................... 106

4.7.1.4 Kuwa na Marafiki Waswahili............................................................ 107

4.7.1.5 Kuhamia Uswahilini ......................................................................... 108

4.7.1.6 Dhamira ya Mapenzi na Ndoa ........................................................... 108

4.7.1.6.1 Mapenzi ............................................................................................. 109

4.7.2 Ukombozi wa Kisiasa......................................................................... 111

4.7.2.1 Subra na Uvumilivu........................................................................... 111

4.7.2.2 Kujitolea Muhanga ............................................................................ 112

4.7.2.3 Umoja na Ushirikiano......................................................................... 113

4.7.2.4 Kutokata Tamaa................................................................................. 114

4.7.2.5 Juhudi na Bidii katika Kazi ... 115

4.7.2.6 Ushujaa na Ujasiri ... 116

4.7.4.7 Uzalendo ... 117

4.7.2.8 Utetezi wa Haki za Jamii ... 118

4.7.3 Ukombozi wa Kifikra ... 119

4.7.3.1 Kufikiri mbinu za kujikomboa ... 119

4.7.3.2 Fikra ya kujitambua na kujielewa ... 120

4.7.3.3 Fikra za kuchoshwa na nyendo zisizofaa ... 120

4.7.3.4 Kufikiria juu ya uongozi usiofaa ... 121

4.7.3.5 Kufikiri namna ya Kujikwamua kutoka katika Makucha ya Wakoloni ... 122

4.7.4 Ukombozi wa Kiuchumi ... 123

4.7.5 Ukombozi wa Kielimu ... 124

4.7.5.1 Dhamira ya Umuhimu wa Elimu ... 124

4.7.6 Hitimisho ... 126

4.8 Kulinganisha na Kulinganua Dhamira ya Ukombozi katika ya *Kusadikika* na *Vuta N' Kuvute* ... 126

4.8.1 Kulinganisha ... 126

4.8.1.1 Dhamira ya Juhudi na Bidii katika Kazi ... 126

4.8.1.2 Uzalendo ... 127

4.8.1.3 Umoja na Mshikamano ... 129

4.8.1.4 Ushujaa na Ujasiri ... 130

4.8.1.5 Utetezi wa Haki za Binaadamu ... 130

4.8.1.7 Subra na Uvumilivu ... 132

4.8.1.7 Kutokata tamaa ........................................................................ 133
4.9 Hitimisho ................................................................................ 134
4.10 Kutafautisha Dhamira katika Riwaya tajwa ....................................... 135
4.10.1 Dhamira ya elimu ................................................................... 135
4.10.2 Upendo (mapenzi na ndoa)................................................................ 136
4.10.3 Hekma na busara .................................................................... 137
4.11 Hitimisho ................................................................................ 138

**SURA YA TANO : MUHUTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .... 139**

5.1 Utangulizi ................................................................................ 139
5.2 Muhutasari ............................................................................... 139
5.2.1 Sura ya kwanza unahusu utangulizi kwa ujumla................................. 139
5.2.2 Sura ya pili ilihusu mapitiyo ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia ................................................................................ 140
5.2.3 Sura ya tatu-Mbinu za utafiti ............................................................. 140
5.2.4 Sura ya nne -Ukusanywaji ,uchambuzi na uwasilishwaji wa data ....... 141
5.2.5 Sura ya tano -muhutasari, hitimisho na mapendekezo ......................... 141
5.3 Lengo mahsusi la kwanza.................................................................. 142
5.3.2 Lengo Mahsusi La Pili...................................................................... 142
5.3.3 Lengo Mahsusi la Tatu ..................................................................... 143
5.4 Hitimisho ................................................................................ 143
5.5 Mapendekezo.............................................................................. 144
5.5.1 Mapendekezo kwa Taaluma ............................................................. 144
5.5.2 Mapendekezo kwa Serikali................................................................ 144

5.5.3 Mapendekezo kwa Jamii ........ 145

5.6 Hitimisho ........ 145

**MAREJELEO ........ 146**

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| ACLA | Chama cha Fasihi Linganishi cha Marekani (American Comperative Literature Association) |
| A.U | Umoja wa Afrika |
| BAKIZA | Baraza la Kiswahili Zanzibari |
| BCLA | Chama cha Fasihi Lingnishi cha Uengereza (British Comperative Literature Association |
| BOT | Benk Kuu ya Tanzania |
| FCLA | Chama cha Fasihi Lingnishi cha Ufaransa (French Comperative Literature Association) |
| GCLA | Chama cha Fasihi Lingnishi cha Ujerumani (German Comperative Literature Association) |
| ICLA | Chama cha Fasihi Lingnishi cha Kimataifa (International Comperative Literature Association) |
| OAU | Ushirika wa Umoja wa Afrika (Organisation of Africa Union) |
| Nk | Na kadhalika |
| PAFMECA | Pan African Freedom Movement for East and Central Africa |
| SUZA | Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar |
| Uk | Ukurasa |
| UWAVITA | Umoja wa Uwandishi wa Vitabu Tanzania |

## ORODHA YA MAJEDWELI

Jedwali na. 4.1: Muhutasari wa Dhamira za ukombozi katika riwaya ya Kusadikika ........ 104

Jedwali na. 4.2: Muhutasari wa dhamira za ukombozi katika riwaya ya Vuta N'kuvute ........ 125

Jedwali na. 4.3: Muhutasari wa dhamira zilizofanana katika riwaya ya Kusadikika na Vuta N'kuvute ........ 134

Jedwali na. 4.4: Muhutasari wa dhamira za ukombozi zilizotafautiana katika riwaya ya Kusadikika na Vuta N'kuvute ........ 138

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI WA UJUMLA

## 1.1 Utangulizi

Kazi hii imejihusisha na mada isemayo: Kuchunguza dhamira ya ukombozi katika riwaya *ya* Kusadikika na *Vuta N'kuvute*: Utafiti linganishi. Katika sura hii mtafitiamejadili vipengele vya msingi vifuatavyo:Usuli wa mada,tatizo la utafiti,malengo ya utafiti,maswali ya utafiti,mipaka ya utafiti,umuhimu wa utafiti, vikwazo vya utafiti na utatuzi wake na mwisho ni hitimisho. Vipengele hivyo ni kama vifuatavyo:

Vipengele hivi ni muhimu na vimemsaidia mtafiti katika kazi yake ya utafiti. Kiuhakika mada hii imekusudia kufikisha lengo la utafiti ambalo ni: Kuchunguza dhamira ya ukombozikatika riwaya ya *Kusadikika* na *Vuta N'kuvute***.** Lengo la mtafiti ni kujua ni kwa kiasi gani watunzi hawa wameweza kuibua suala la ukombozi na namna ukombozi huo ulivyojitokeza kupitia riwaya zao. Hii ni kutokana na kuwa, riwaya hizi mbili zimetoka kwa waandishi wawili tofauti, wenye asili tofauti na nyakati tafauti. Kwa mfano, riwaya ya *Kusadikika* ya ShaabanRobert imeandikwa mwaka (1951) na riwaya ya *Vuta N'kuvute* ya Shafi Adam Shafi imeandikwa mwaka (1999). Si hivyo tu, watunzi hawa nimiongoni mwa waandishi mahiriwa kazi ya fasihi ya Kiswahili. Kwa mfano, Shaaban Robert ambaye ni mzaliwa wa Tanga-Tanganyika (Tanzania bara) amefanikisha kuandika kazi nyingi za fasihi zikiwemo riwaya na mashairi. Miongoni mwa kazi zake katika riwaya ni pamoja na:*Utubora Mkulima*(*1946), Kufikirika* (*1947), Kusadikika (1951) na Adili na Nduguze (1952)***.**Kwa upande wa Shafi Adam Shafi ambaye naye ni mzaliwa wa Zanzibar

(Tanzania visiwani) ameandika *Kasriya Mwinyi Fuad (1978*), *Kuli (1979), Haini (2003),Vuta N'kuvute (1999)*n.k

Kwa ufupi ni kwamba, mtafiti amekusudia kuchunguza bidii na juhudi za waandishi(Shafi Adam Shafi na Shaaban Robert) katika kuonesha dhamira ya ukombozi kupitia riwaya hizo teule. Mtafiti amechunguza kwa kinadhamira ya ukombozi pamoja na kulinganisha na kutafautisha dhamira hiyo katika nyanja za kijamii,kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni kwa kurejelea riwaya teule za *Kusadikika* na *Vuta Nkuvute.*

## 1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Kwa ujumla tunaweza kusema, ukombozi ni ile hali ya kuwatoa au kuwaokoa watu (wanaadamu) na hata viumbe vyenginevyo kutoka katika hali ya dhiki, madhila na maovu kwenda katika tabia au matendo mema yanayokubalika na yaliyo sahihi kwa ajili ya maslahi ya wahusika hao na jamii au taifa kwa ujumla.

Ukombozi katika fasihi ni kitendo cha wahusika kupigania uwepo wa haki na usawa, imani na matendo mema yenye kukubalika ambapo hapo awali wahusika hao walikuwa wakiishi katika madhila na maovu makubwa kutoka tabaka tawala la jamii au taifa husika. Wasanii na waandishi mbalimbali katika kazi zao za fasihi huweza kuwachora / kuwasawiri wahusika katika pande mbili kubwa; yaani tabaka tawala na tabaka tawaliwa.

Tabaka tawala kawaida ndio linaloendeleza ukatili, unyanyasaji, udhalilishaji, mauwaji na maovu mengineyo kwa tabaka tawaliwa. Kwa upande mwengine tabaka

tawaliwa ndio wale wenye kufanyiwa madhila na tabaka tawala. Hivyo basi kwa maonevu hayo huweza kuzinduka na kuweza kusimama imara kwa lengo la kujikomboa na kuwa huru ili na wao waweze kuishi maisha mema na yenye mafanikio katika jamii husika. Kwa ujumla ukombozi huweza kuwa wa kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na hata ukombozi wa kifikra/ kibinafsi.

Mei 25 ya kila mwaka ni siku ya Afrika, siku iliyowekwa na Umoja wa Afrika (AU) kwa nia ya kukumbuka na kutathmini nguvu za umoja huo katika harakati za kukomboa nchi za bara la Afrika. Nia ya umoja huo ilianza tangu Muafrika alipokataa kuvunjiwa utu wake na kujenga harakati za kudai uhuru na ukombozi wake kutokana na kuonewa, kudhalilishwa na kunyonywa na wakoloni ambao kwa kweli wamechukuwa mali nyingi za mama Afrika bila ya ridhaa ya watoto wa Afrika. Kuanzishwa kwa vyama vya ukombozi katika nchi mbalimbali Afrika, mfano umoja wa vyama vya ukombozi Afrika Mashariki na kati (Pan African Freedom Moment for East and Central Africa - PAFMECA) unaohusisha nchi za Kenya, Uganda, Tanganyika, Malawi, Zambia na Zanzibar katika umoja huo kumeamsha ari na hamasa ya Waafrika kuendelea kujikomboa na kutafuta maslahi bora kwa nchi wanachama na bara lote la Afrika.

Nchi sita hizo ziliunda umoja huo na kuzaliwa kwake mjini Mwanza, Septemba 1958 na kuchagua mwenyekiti wake kuwa mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Vijana wa Afrika nao hawakuwa nyuma katika harakati za ukombozi huo, walianzisha umoja wa vijana wa Afrika na kumteua kijana shupavu Kingunge Ngombale Mwiru kuwa katibu mkuu wake.Harakati za ukombozi zilipamba moto na baadhi ya mambo yakipewa uzito wake kama vile kupinga ukoloni na kupambana na ukoloni mamboleo

na ubeberu ulioendeshwa katika nchi za Afrika. Katika mapambano hayo dhidi ya ukoloni yaliendeshwa kwa kutumia silaha na katiba. Pia yalishamiri na baadaye nchi moja baada ya nyengine ilijikomboa kutoka katika makucha ya wakoloni.Ukombozi huo ulipofikia mwaka 1987 nchi zipatazo 50 katika bara Afika zilikwishapata uhuru.

Harakati hizo za ukombozi zilitowa njia pia ya kuunda kamati ya ukombozi ya umoja wa nchi huru za Afrika mwaka (1963). Juhudi hizo zilikamilisha kuundwa rasmi umoja wanchi huru za Afrika (Organization of Africa Union, OAU) mnamo Mei 25, 1963 mjini Adis Ababa, Ethiopia. Leo umoja huo unaitwa umoja wa Afrika (AU).Hakika umoja huo ulianzishwa na nchi huru 30 chini ya viongozi wao wakuu; Tanzania ikawa ni nchi mojawapo.Lengo la historia hiyo ni kujua shabaha ya uhuru na ukombozi wa Afrika tangu uhuru wa nchi ya Ghana mwaka 1957 hadi uhuru wa nchi ya Afrika Kusini 1994, ikiwa ni miongoni mwa nchi ya mwisho kujikomboa barani Afrika.Jee kwa harakati hizo muafrika amejikomboa? Ukweli ni kwamba amejikomboa kwa baadhi ya mambo ila si kwa mambo yote, hivyo kwa sasa waafrika wengi wamo katika mfumo wa ukoloni mamboleo.

Kwa hakika dhana ya ukombozi ina nafasi kubwa katika maisha ya kila siku kwa lengo la kujinasua kutoka katika dimbwi la dhulma, udhalilishaji, unyonyaji, utabaka, ubaguzi na maovu mengineyo kwenda katika misingi ya baraka na neema, haki usawa na amani. Kwa misingi hiyo utafiti huu umelenga kuchunguza kwa undani dhamira ya ukombozi kupitia riwaya teule ya *Kusadikika* na *Vuta N'kuvute*.

## 1.3 Tatizo la Utafiti

Watafiti mbali mbali wamefanya tafiti juu ya dhamira zilizomo katika riwaya za Shaaban Robert na Shafi Adam Shafi lakini hawakuibua dhamira ya ukombozi bali walijikita zaidi katikaa dhamira nyenginezo kama za kisiasa nk.Miongoni mwa watafiti hawa ni kama wanavyofuata:-

Amrose(2014) aliandika utafiti unaohusu "Kuchunguza Dhamira za Kisiasa katika Riwaya za Shaban Robert" Matokeo yake yalikuwa ni kuonesha ni namna gani Shaaban Robert aliathiriwa na usiasa katika kutunga kazi zake. Khatibu (1983) alifanya uhakiki wa riwaya ya "*Kuli*" kueleza kuwa dhamira kuu katika riwaya hiyo ni ukombozi wa kiutabaka. Khatibu (ameshatajwa) hakuchambua kwa kina juu ya dhamira za riwaya hii ambayo ni utabaka na badala yake ameishia kutaja tu na kueleza kwa ufupi. Hata hivyo, maelezo yake kuwa ukombozi unofanywa na watu tabaka la chini huwashusha watu tabaka la juu. Adam (2014) katika tasnifu yake yenye mada: "Kuchunguza dhamira za kijamii na kiutamaduni katika riwaya za Kiswahili: "*Kuli*" na "*Vuta N'kuvute*".Katika utafiti wake hakujihusisha na dhamira nyengine zozote isipokuwahizozilizotajwa, yaani dhamira kuhusu masuala ya kijamii na kiutamaduni. Kutoana na sababu hiyo mtafiti aliona ipo haja ya kuchunguza dhamira ya ukombozi katika riwaya tajwa ili kuziba pengo ambalo bado halijajadiliwa.

## 1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu una malengo ya aina mbili ambayo ni lengo kuu na malengo mahsusi.

### 1.4.1 Lengo Kuu

Kuchunguza dhamira ya ukombozi katika riwaya ya *Kusadikika na Vuta N'kuvute: Utafiti linganishi*.

### 1.4.2 Malengo Mahsusi

Utafiti huu umejikita juu ya malengo mahsusi ya utafiti yafuatayo:-

i) Kubainisha dhamira za ukombozi katika riwaya ya *Kusadikika.*

ii) Kubainisha dhamira za ukombozi katika riwaya ya *Vuta'kuvute*.

iii) Kufananisha na kutafautisha dhamiraya ukombozi katika riwaya teule.

## 1.5 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu una jumla ya maswali ya utafiti matatu yafuatayo:-

i) Ni dhamira zipi za ukombozi zilizojitokeza katika riwaya *Kusadikika?*

ii) Ni dhamira zipi za ukombozi zilizojitokeza katika riwaya ya *Vuta N'kuvute?*

iii) Dhamira ya ukombozi katika riwaya teule inafanana na kutafautiana vipi?

## 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Kwanza**,** Matarajio ya mtafiti katika utafiti huu yanaonekana zaidi katika mambo yafuatayo:

Utafiti huu unatarajiwa kuwa ninyenzo muhimu kitaaluma katika kutoa msukumo wa ngazi mbalimbali za kielimu kama kupata data za kufanya utafiti mwengine, kuboreha kiwango cha elimu n.k

Pili, Utafiti huu utakua ni msingi mzuri kwa watafiti wengine kuendeleza juhudi zao za kuchunguza dhana ya ukombozi na nafasi yake katika kazi za fasihi na jamii kwaujumla.

Tatu, Utafiti huu unategemewa kuwa utasaidia katika kudhihirisha umuhimuwa kujikomboa kutoka katika madhila yaani maovu pamoja na changamoto anazokabiliana nazo na njia za kujinasua kutokana na madhila hayo katika maisha ya kila siku kupitia riwaya ya *Kusadikia* na *Vuta N'kuvute*.

Nne, utafiti huu utakuwa ni msaada muhimu kwa wale watakaoamua kufanya utafiti wa fasihi linganishi ya Kiswahili.

## 1.7 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi wake

Kama inavyojulikana kwamba utafiti nikazi muhimu na yenye mafanikio mengi kwa mtafiti na jamii kwa ujumla. Utafiti pia ni kazi ngumu na yenye uzito na vikwazo ndani yake. Katika utafiti huu mtafiti amekabiliana na vikwazo tafauti ambavyo ameweza kuvitatua kwa madhumuni ya kufikia malengo ya utafiti wake vyema. Vikwazo hivyo na utatuzi wake ni kama ifuatavyo:

**Kwanza, uhaba wa marejeleo**

Marejeleo ni nyenzo muhimu mno katika utafiti,kwa vile mtafiti ni mkaazi wa kisiwa cha Pemba, Wilaya ya Micheweni amekumbana na kikwazo kikubwa cha kupata marejeleo yatakayofaa kulingana na mada yake kwa sababu ndani ya Wilaya hiyo hakuna maktaba na maktaba ya mkoa iliyopo haitoshelezi. Hivyo, hiyo imepelekea kuzorotesha kwa kiasi fulani kazi hii ya mtafiti.

**Utatuzi wa kikwazo**

Mtafiti amekabiliana na kikwazo hicho kwa kwenda maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) na Maktaba ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), maktaba kuu ya Zanzibar. Maktaba zote hizo zimepatikana katika tawi la Pemba. Mtafitipia ametumia wavupepe (internet) kufanikisha utafiti huu.

**Pili, mwalimu muwajiriwa**

Tatizo jengine ni kuwa, mtafiti ni mwalimu wa skuli ya Sekondari Msuka iliyoko Wilaya ya Micheweni – Pemba.Kikwazo hasa ni kukosa kufanya utafiti wake ipasavyo kutokana na majukumu aliyopangiwa ya shule kulazimikakuyatekeleza kikamilifu. Hali hii imechangia kuzorotesha utafiti huukwa kiwango fulani.

**Utatuzi wa kikwazo**

Mtafiti imempasa atumie siku za mapumziko (Jumamosi na Jumapili),muda mwingi wa usiku na siku moja ya ruhusa kazini kwa ajili ya masomo (Jumanne). Kwa hakika juhudi hizo zimesaidia sana kukamilisha utafiti huu kwa wakati.

Kwa ujumla, utafiti huu ulifanikiwa kumaliza katika muda mwafaka baada ya utatuzi wa changamoto hizo kufanyiwa kazi ipasavyo.

## 1.8 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu umejihusisha katika kuchunguza dhamira ya ukombozi katika riwaya ya *Vuta N'kuvute* ya Shafi Adam Shafi na*Kusadikika* ya Shaaban Robert. Mtafiti anaelewa vyema kwamba watunzi wa riwaya hizi ni weledi, mahiri na mashuhuri waliotunga kazi nyingi za fasihi zikiwemo riwaya.Kwa kuthibitisha hili, waandishi

hawa wameandika vitabu mbalimbali.Kwa mfano, Shaaban Robert aliandika riwayakama vile: *Kusadikika (1951),Kufikirika (1968), Adili na Nduguze (1952).* Kwa upande wa Shafi Adam Shafi aliandika riwaya kama vile: *Kasri ya Mwinyi Fuadi (1978), Kuli (1979), Haini (2003) na Vuta Nkuvute (1999).*

Kutokana na hayo, mtafiti amezingatia zaidi katika kuchunguza ukombozi ndani ya riwaya teule ambazo ni*Kusadikika* na*Vuta N'kuvute*.Mtafiti amechagua riwaya hizi kwa sababu anaamini zinalingana kimaudhui licha ya hitilafu chache zilizomo ndani yake.Hivyo, mtafiti hatajikita katika kuhunguza riwaya nyengine zozote au mada nyengineakiamini riwaya alizochagua zimetosha katika kufanikisha malengo na maswali yake ya utafiti kwa kiwango kinachotakikana. Marejeleo mengineo yakiwemo ya riwaya yametumika ili kufikisha ukomo wa utafiti huu.

## 1.9 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu wenye mada isemayo: "*Kuchunguza dhamira ya ukombozi katika riwaya ya Kusadikika na Vuta N'kuvute"* ni utafiti linganishi uliogawanywa katika sura tano zifuatazo:-

**Sura ya Kwanza**: **Utangulizi kwa Ujumla**

Vipengele vyake ni utangulizi,usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti,umuhimu wa utafiti,vikwazo vya utafiti na umuhimu wake,mipaka ya utafiti,muundo wa utafiti na hitimisho.

**Sura ya Pili: Mapitio ya Kazi Tangulizi na Mkabala wa Kinadharia**

Sura hii imehusu utangulizi, ufafanuzi wa istilahi mbalimbali, mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia, nadharia ya Mwitiko wa Msomaji (upokezi), nadharia ya Fasihi Linganishi na hitimisho.

**Sura ya Tatu: Mbinu za Utafiti**

Sura hii inaeleza vipengele vifuatavyo: Utangulizi,maana ya mbinu za utafiti,eneo la utafiti,uteuzi wa eneo la utafiti,sababu za uteuzi wa eneo la utafiti,usanifu wa utafiti,kundi lengwa,sampuli na usampulishaji,sampuli ya watafitiwa,sampuli lengwa,ukusanyaji wa data (data za awali na data za upili) mbinu za ukusanyaji wa data,mbinu ya maktabani,mbinu za kukusanya data za awali/msingi:usomaji wa makini,mbinu za kukusanya data za upili:upitiaji wa nyaraka,mbinu za uchambuzi wa data,mkabala wa kimaelezo,usahihi wa data za utafiti,maadili ya utafiti na hitimisho .

**Sura ya Nne: Uchambuzi na Uwasilishwaji wa Data**

Katika sura hii, mtafiti ameanza nautangulizi, historia ya mtunzi wa riwaya ya *Kusadikik*a ambayo imejumuisha uwandishi wake, falsafa yake,kifo na kumbumbu yake. Baada ya hapo ameingia katika historia ya mtunzi wa *Vuta N'kuvute*.Vile vile, kuna muhtasari wa riwaya ya *Kusadikika*, muhutasari wa riwaya ya *Vuta N'kuvute*,ubainishaji wa dhamira za ukombozi zilizomo katika *Kusadikika*,ubainishaji wa dhamira za ukombozi zilizomo katika *Vuta N'kuvute*,ulinganishaji wa dhamira zilifanana katika riwaya hizo,utafautishaji wa dhamira zilizotafautiana na riwaya teule baadaye ni hitimisho.

**Sura ya Tano : Muhutasari, Hitimisho na Mapendekezo**

Hii ni kama ifuatavyo:Utangulizi juu ya sura husika, muhutasari wa kila sura, malengo ya utafiti nayo yamezingatiwa vilivyo, pia kuna hitimisho lilijikita juu ya uchambuzi wa dhamira za ukombozi kwa kuzingatia kuwa, ukombozi ndio chanzo cha mafanikio ya mahitaji ya umma popote palipo na uovu na uonevu panatakikana pakombolewe kwa namna yoyote ili paondokane na dhulma inayotendeka.Vile vile inatoa mapendekezo ambayo anaamini yatafaa kitaaluma,kiserikali,kijamii na kwa watafiti wengine.

## 1.10 Hitimisho

Sura hii ni muhimu mno katika utafiti huu kwa sababu inajadili vipengele adhimu vya utafiti ambavyo ni dira katika utafiti huu wenye mada isemayo *"Kuchunguza dhamira ya ukombozikatika riwaya ya Kusadikika naVutaN'kuvute : Utafit linganishi.* Katika sura hii zaidi viliangaliwa vipengele vifuatavyo: Usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti,maswali ya utafiti,umuhimu wa utafiti, vikwazo vya utafiti na utatuzi wake,mipaka ya utafiti,muundo wa utafiti na mwisho ni hitimisho.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sura hii nayo ni muhimu kama zilivyo sura nyenginezo. Vipengele vilivyojadiliwa katika sura hii vimeendelea kutoa sura kamili ya utafiti huu kama vile vipengele vilivyotangulia. Vipengele hivyo ni pamoja na: Ufafanuzi wa istilahi mbalimbali, Mapitio ya kazi tangulizi, mkabala wa kinadharia na mwisho ni hitimisho.Uchambuzi wa vipengele hivyo ni kama ifuatavyo:

## 2.2 Ufafanuzi wa Istilahi mbalimbali

Katika utafiti huu baadhi ya istilahi muhimu zimejadiliwa kwa lengo la kurahisisha uelewa wa utafiti huu katika dhana teuliwa. Istilahi zitakazojadiliwa ni kama zifuatazo:

### 2.2.1 Dhana ya Riwaya

Maana ya "Riwaya"si dhana ngeni kwa wasomi hasa wa Fasihi.Wataalamu kadhaa wamejaribu kuelezea juu ya dhana hii kwa kina zaidi wakitoa mawazo yao tofauti.Miongoni mwa wataalamu hao ni pamoja na hawa wafuatao:

Muhando na Balisidia (1976) wanafafanua, riwaya ni kazi ya kubuni yenye uwezo wa fanani, mazoea yaani mazingira ya fanani, maneno kuanzia 35000, yenye mchangamano wa matukio, ujenzi wa wahusika, dhamira, muundo na mtindo maalumu. Nkwera (1978) amesema, riwaya ni hadithi iliyo ndefu kuweza kutosha kufanya kitabu kimoja au zaidi.

Senkoro (1982:73) anaeleza, riwaya ni kisa ambacho ni kirefu vya kutosha chenye zaidi ya tukio moja ndani yake, ni kisa mchangamano ambacho huweza kuchambuliwa na kupimwa kwa uzito na undani wa mambo mbalimbali, riwaya ni kisa ambacho urefu wake unakiruhusu kutambaamahali pengi na kuambaa vizingiti vingi kama apendavyo muandishi. Ndungo, na Mwai (1991) wanaeleza, riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni yenye mchangamano wa visa ambavyo huchambuliwa na kupimwa kwa mapana na marefu kimaudhui na kifani.

Mulokozi (1992) anafasili, riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni yenye mawanda mapana, lugha ya kinathari, mchangamano wa visa na dhamira, wahusika kadhaa na matukio yaliyosukwa kimantiki, yenye kufungamana na wakati na kushabihiana na maisha halisi.Wamitilla (2003) amesema, riwaya ni kazi ya kinathari au kibunilizi ambayo huwa na urefu wa kutosha, msuko uliojengeka vizuri, wahusika wengi, walioendelezwa kwa kina,wenye kuchukuwa muda mwingi katika maandalizi na kuhusisha mandhari maalumu.

Kwa kuhitimisha, riwaya ni hadithi ndefu yenye mawanda mapana na yenye kuhusisha wahusika wengi ambao hupewa matendo ya kubuni yanayoendana na mandhari husika kulingana na matukio maalumu yanayojitokeza ndani ya jamii fulani.

### 2.2.2 Dhana ya Dhamira

Wamitila (2002) anafafanua, dhamira ni jumla ya maana anayoivumbua mwandishi aandikapo na jumla ya maana anayoitambua msomaji katika usomaji wake**.** Madumulla (2009) anasema, dhamira ni wazo kuu katika kazi ya fasihi. Senkoro

anatahadharisha kuchanganya “dhamira” na “Maudhui”, jambo ambalo hutokea kwa wengi. Dhamira ni sehemu tu ya Maudhui. Aghalabu, dhamira kuu ndiyo hujenga kiini cha kazi ya fasihi. Dhamira kuu husindikizwa na dhamira ndogo ndogo. Wazo kuu hubeba funzo kuu.

Kwa ujumla, dhamira ni makusudio au ni jumla ya mawazo ya dhati ambayo mwandishi amekudia kuifikishia jamii kwa lengo la kutoa elimu sahihi kwa jamii husika. Dhamira huweza kuwa dhamira kuu au dhamira ndogondogo.

### 2.2.3 Dhana ya Ukombozi

BAKIZA (2010) wanaeleza, ukombozi ni utoaji wa mtu kwenye hali ya madhila au uduni wa maisha. Kamusi ya karne ya ishirini (2015) wanafafanua, ukombozi ni matendo au vita vya kuokoa watu kutoka kwenye hali mbaya yenye mateso au hali ya unyonge. Pia, ukombozi ni hali ya kutoa watu katika dhambi. Ukombozi huweza kujitokeza katika aina kuu zifuatazo: Ukombozi wa kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na kibinafsi.

## 2.3 Mapitio ya Kazi Tangulizi

Enon (1998) anafafanua kuwa mapitio ya kazi tangulizi ni usomaji wa kina wa maandishi ya watafiti watangulizi, unaofanywa na mtafiti kwa ajili ya uchambuzi kuhusu suala la utafiti. Mapitio ya kazi tangulizi lazima yaonyeshe uhusiano wa maandishi hayo na mada ya utafiti. Katika mapitio ya kazi tangulizi huoneshwa pia nadharia zilizotumika katika uchambuzi wa data.

Msingi muhimu wa kuandika mapitio ya kazi tangulizi ni kuweza kuhakikisha kwamba, mada inayofanyiwa utafiti ni mada tofauti na mada zilizotangulia lakini zina uhusiano na mada ya mtafiti. Hii ina maana kwamba kazi tangulizi zitasaidia sana kutoa muongozokwa kurejelea uhusiano na mada teule na kuwa sababu muhimu ya kutosheleza kufanya utafiti huo ipasavyo.

### 2.3.1 Mapitio ya Kazi Tangulizi kuhusu Riwaya za Shaaban Robert

Mapitio ya kazi tangulizi kuhusu mwandishi Shaaban Robert yana thamani kubwa katika utafiti huu. Hii ni kwa sababu, Robert ameandika vitabu zaidi ya ishirini vikiwemo vya utanzu wa ushairi na riwaya. Kazi hizo zimesaidia sana katika mapitio ya kazi tangulizi ya utafiti huo. Miongoni mwa kazi tangulizi kuhusu riwaya za Robert ni kama zifuatazo:-

Sengo(1975) aliandika kazi juu ya mada isemayo,“Shaaban Robert,uhakiki wa maandishi yake,”Katika uhakiki huu Shaaban Robert ameelezwa kuwa ni mtu ambaye alijali sana ubinaadamu katika jamii,alipenda kuona kuwa kila mtu anapata heshima yake, haki zake na kutendeana mema kati ya wanaadamu katika jamii.Mawazo haya yalikuwa katika kipindi ambacho Tanganyika ilikuwa imetawaliwa na wakoloni ambao hawakujali haki za Watanganyika,kwa mantiki hiyo Shaban Robert aliwataka wakoloni kuwapatia wananchi haki zao na kuwaheshimu.

Kezilahabi (1976) alifanya utafiti kuhusu “Shaaban Robert Mwandishi wa Riwaya,”Matokeo ya utafiti wake yameonesha kuwa Shaban Robert ni mtunzi wa riwaya mwenye uoni na umahiri wa hali ya juuukilinganisha na waandishi wengine ulimwenguni.Vilevile, Kezilahabi (2011) alifanya utafiti uliolenga “Kuchunguza

Itikadi katika Riwaya za Shaban Robert,"Matokeo yake yameonesha kuwa riwaya za Shaban Robert zimesheheni itikadi mbalimbali kama vile ujamaa, ubepari, unyonyaji n.k.

Utafiti huo umekuwa na faida kubwa kwa mtafiti kwa sababu umejikita kuzungumzia juu ya uandishi uliobora wa Shaaban Robert ambao unahusu mambo mbalimbali ikiwemo maadili, maonyo na maisha mema kwa binaadamu au viumbe wote.Dhana hii ndio ambao mtafiti ameipa nafasi kubwa kuhusu mwandishi huyo kupitia riwaya mojawapo ya "*Kusadikika"*anayoitafiti.

Mjema (1990) aliandika makala yenye kichwa: "*Kusadikika*"Katika makala hii aliibua dhamira zenye kuonesha maudhui hasi na chanya baina ya matabaka yaliomo ndani ya jamii. Kwa hakika utafiti wa Njema (ameshatajwa) umeendelea kutilia mkazo juu a juhudi za mwandishi katika usawiri wa maudhui hasi na chanya kupitia riwaya teule ya "*Kusadikika"*. Juhudi hizo zimeenda sambamba na mada ya mtafiti katika utafiti huu kwa sababu riwaya iliyojadiliwa na Mjema (ameshatajwa) ndio riwaya mojawapo inayojadiliwa katika utafiti huu isipokuwa msingi wake mkuu ni kuhusu mada ya ukombozi katika ulinganishaji wa riwaya ya "*Kusadikika"* na "*Vuta Nkuvute"*.

Kyando (2013) aliandika makala iliyohusu "Kuchunguza Majina Sadifa ya Wahusika katika Riwaya za *Kusadikik*a na *KichwaMaji*" Matokeo yake yalionesha kuwa majina yaliotumiwa ndani ya riwaya hizo yamesadifu vya kutosha kiasi cha kuweza kulinganisha na matendo ya wahusika hawa.Tasnifu ya Kyando (ameshatajwa) imeengeza ladha utafiti huu kwa sababu msingi wa yanayojadiliwa

katika tasnifu hiyo kuhusu riwaya mbili hizo ikiwemo riwaya ya *Kusadikika* imeengeza mchango wa kutambua nafasi za wahusika kusadifu matendo yao. Suala hilo limeengeza msukumo zaidi wa kufanikisha utafiti huu kuhusu mada ya mtafiti kupitia riwaya ya "*Kusadikika*"

Amrose(2014) aliandika utafiti unaohusu "Kuchunguza Dhamira za Kisiasa katika Riwaya za Shaban Robert" Matokeo yake yalikuwa ni kuonesha ni namna gani Shaaban Robert aliathiriwa na usiasa katika kutunga kazi zake.Kwa hakika kazi ya Amrose (ameshatajwa) imeongeza tija katika utafiti huu, hii ni kwa sababu dhamira kuhusu siasa ina umuhimu wake katika jamii. Hivyo basi tasnifu hiyo imechangia kuwa ni tija nyengineyo katika kuimarisha utafiti huu.

Ponera (2010) alifanya utafiti kuhusu "Ufutuhi katika Nathari za Shaban Robert: Maana yake, Sababu za kutumiwa na Athari zinazopatikana kwa Wasomi" na Kabeja (2013*)* alitafiti kuhusu"Dhana ya Ufutuhi katika Riwaya za Shaban Robert. Saleh (2015) alitafiti mada isemayo "Ufasihi Simulizi katika Riwaya za Shaban Robert: Mifano kutoka Riwaya ya "*Adili na Nduguze*" na "*Wasifu wa Siti Binti Saad*". Salim (2015) alifanya utafiti wenye mada "*Kuchunguza Ufasihi Simulizi unaojitokeza ndani ya Hadithi za Kusadikika na Adili na Nduguze*"

Kwa muhtasari tasnifu za Ponera, Kabeja, Saleh, na Salim (wameshatajwa) zimeendelea kutilia mkazo juu umuhimu wa kuthamini juhudi za mtunzi mahiri Shaaban Robert kupitia riwaya zake na kusisitiza kufuata matendo mema

anayoyaelekeza na kuusia kuacha yale maovu ili kujenga jamii imara na yenye mafanikio.

### 2.3.2 Mapitio ya Kazi Tangulizi kuhusu Riwaya za Shafi Adam Shafi

Khatibu (1983)alifanya uhakiki wa riwaya ya *"Kuli"* kueleza kuwa dhamira kuu katika riwaya hiyo ni ukombozi wa kiutabaka. Khatibu (ameshatajwa) hakuchambua kwa kina juu ya dhamira za riwaya hii ambayo ni utabaka na badala yake ameishia kutaja tu na kueleza kwa ufupi. Hata hivyo, maelezo yake kuwa ukombozi unofanywa na watu tabaka la chini huwashusha watu tabaka la juu. Mulokozi (1990) aliandika makala juu ya utunzi wa riwaya za kihistoria ya Kiswahili na kueleza mambo mbali mbaliya kifani na kimaudhui yanayoipamba riwaya hiyo.Katika harakati zake za kukamilisha lengo hili alimtaja Shafi Adam Shafi kuwani miongoni mwa waandishi ambao wanatunga riwaya za kihistoria. Amelisema hili kwa kutolea mfano kuwa ujenzi wa wahusika katika riwaya za mtunzi huyo zilishia kuwa yeye ni mtunzi wa riwaya za kihistoria.

Diegnar (2011) alifanya mazungumzo na Shafi Adam Shafi kuhusu maandishi yake ya riwaya tangualipoanza hadi alipofikia katika mazungumzoyao alimuuliza maswali mengi kuhusu mambo yaliomsukuma hadi kuandika riwaya alizoziandika. Bila choyo, Shafi Adam Shafi alijibu maswali alioulizwa kwa ustadi wa juu kabisa kiasi cha kumuezesha mtafiti au msomaji kupata mambo mengi kuhusu utunzi wa riwaya uliofanywa na Shafi Adam Shafi.

Walibora (2013) aliandika makala kuhusu riwaya mpya ya tawasifu iliyoadikwa na Shafi Adam Shafi juu ya maisha yake. Pamoja na mambo mengi aliyoyaeleza kubwa

ni kumsifu Shafi Adam Shafi kuwa ni miongoni mwa watunzi wajasiri ambaye ameweza kueleza mambo mbali mbali yanayoeleza maisha yake bila kificho.

Adam (2014) katika tasnifu yake yenye mada: "Kuchunguza dhamiraza kijamii na kiutamaduni katika riwaya za Kiswahili: "*Kuli*" na "*Vuta N'kuvute*".Katika utafiti wake hakujihusisha na dhamira nyengine zozote isipokuwahizozilizotajwa, yaani dhamira kuhusu masuala ya kijamii na kiutamaduni.

## 2.4 Mkabala wa Kinadharia

Nadharia ni neno lenye mawanda mapana. Maana mbalimbali zimetolewa kuhusu neno "nadharia" Wana taaluma na wana nadharia mbalimbali wa fasihi wameeleza kwa urefu kuhusu "Nadharia". Miongoni mwa wataalamu hao ni pamoja na wafuatao:

Msokile (1993) anafafanuakuwa, nadharia ni mawazo, mpango, mwongozo, maelezo, yaliyowekwa ili kusaidia kutatua au kutekeleza jambo fulani. Wamitila (2002) anaeleza, nadharia za uhakiki ni muongozo unaomuelekeza msomaji na mhakiki kwenye vipengele vya msingi vya nadharia anayoitumia.

Wafula na Njogu (2007) wanasema kuwa, nadharia ni jumla ya maelekezo yanayomsaidia msomaji au mhakiki kuifahamu kazi ya fasihi kwa kufuata utaratibu maalum. Massamba (2009) anasema kuwa, nadharia ni taratibu, kanuni na misingi ambayo imejengwa katika muundo wa kimawazo kwa madhumuni ya kutumiwa kama kielelezo cha kuelezea jambo.

Kwa ujumla, Nadharia ni jumla ya mwongozo, maelekezo, taratibu, kanuni, misingi na mpango unaotumiwa na mhakiki au mtafiti ili kumsaidia kuifanikisha na kutekeleza kazi yake ya fasihi vyema na katika kiwango cha ufanisi zaidi. Utafiti huu umeongozwa na nadharia kuu mbili, Nazo ni: Nadharia ya Mwitiko wa msomaji (upokezi) na nadharia ya Fasihi linganishi. Mtafiti amechagua nadharia hizi akiwa na imani kuwa zinatosha katika kujibu maswali ya utafiti pamoja na malengo ya utafiti, sambamba na kufanikisha mada ya utafiti kwa ujumla na asilimia timilifu. Ufafanuzi wa nadharia hizo ni kama ifuatavyo:

### 2.4.1 Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji (Upokezi)

Nadharia inayoshughulikia upokeaji wa matini za fasihi inahusiana na ulimbwende na mitazamo ya kisaikolojia. Kimapokeo, msomaji huwa na mawazo kuhusu matini anayopitia. Kutokana na tajriba ya usomaji, msomaji hupata hisi maalum. Uteuzi na upokeaji wa sanaa hushirikishwa sana na hisi kwa mujibu imani na nadharia za kilimbwende. Hisi ndizo humpa mwana sanaa msukumo wa kutunga. Vilevile msomaji anatazamiwa kuipokea kazi ya fasihi kwa kuzingatia mielekeo yake binafsi. Ulimbwende ni mwelekeo wa kusimulia ambapo wahusika walikuwa mashujaa na wenye nguvu za ajabu na ambao walikuwa wanajeshi. (Wafula na Njogu, 2007)

#### 2.4.1.1 Historia fupi ya Nadharia ya Upokezi na Waasisi wake

Nadharia hii inayomweka msomaji katikati ya uhakiki wa fasihi ilianza miaka ya sitini na sabini hasa kule Marekani na Ujerumani. Waasisi na watetezi wakuu wa nadharia hii ni Stanley Fish (1980), Jane Tompkins (1980), Wolfgang Iser (1974, 1978). Kwa mujibu wa tovuti ya Wikipedia, wananadharia wa upokezi wanaweza kubainishwa katika makundi matatu:

i. Wanoangazia tajriba za kipekee za msomaji (Individualists). Hawa ni pamoja na Lewis (1961), S. Fish (1967) na N. Holland (1968) ambao ni Wamarekani.

ii. Wanamajaribio ya kisaikolojia kwa kikundi wasomaji (Experimenters). Ni Reuven Tsur, Richard Gerrig, David Miall na Donald Kuiken.

iii. Wanaochukulia wasomaji wote wataipokea kazi ya fasihi kwa njia sawa. (Uniformists) ni Wajerumani kamaWolfgang Iser na Haus Robert Jauss.

**2.4.1.2 Mihimili ya Nadharia ya Upokezi**

Waitifaki wa nadharia hii huuliza maswali ambayo kwayo misingi ya nadharia hii imejengeka. Maswali hayo ni:-

i) Je kuna uwiano wowote kati ya maana inayosomwa na jinsi msomaji anavyoihakiki?

ii) Je, kila kazi ya fasihi ina maana kufuatana na msomaji binafsi na jinsi anavyoichukulia?

i) Je kuna wasomaji ambao husoma na kufasiri kazi za fasihi vizuri zaidi kuliko wasomaji wengine.

ii) Je msomaji hutumia vigezo gani kujijulisha iwapo mawazo yake juu ya kazi fulani yanafaa au hayafai?

Adena Rosmarin katika (Murfin,1991) anadai kuwa kazi ya fasihi ni kama kinyago ambacho hakijakamilika na kwa hivyo mchongaji hujaribu kukikamilisha. Kwa hivyo, mihimili ya nadharia hii ni kama ifuatavyo:

i) Msomaji huikamilisha kazi ya sanaa kwa kuijaliza kwa usomaji makini au kuidhalilisha kwa usomaji wa kiholela. Iser na Fish wanadai kwamba kazi ya fasihi huwa na mapengo mengi ambayo msomaji hulazimika kuyajaliza. Kwa hivyo, msomaji hushurutika kutunga matini mpya ambazo zimechochewa kuzalika kutokana na matini asili zilizoko kwenye kurasa.

ii) Nadharia hii inasisitiza athari za kazi za fasihi juu ya akili na maarifa ya mwandishi. Wasomaji mbalimbali hufasiri athari hizi kupitia njia tofauti kutegemea:

- Tofauti kati ya matini na hisia za kibinafsi za msomaji.
- Namna matini inavyoelekezea au kutatiza Mwitikio wa Msomaji. Sifa inayozua usomaji mzuri au mbaya wa kazi inayohusika.

iii) Wana nadharia hawa wanashikilia kuwa kuna njia mbili za kusoma kazi ya fasihi nazo:

- Njia inayofafanua na kusisitiza mawazo ambayo kitambo yamejulikana na kutambuliwa na msomaji.

- Kuwasilisha kazi ya fasihi kimafumbo ili kumchochea msomaji kujitafutia na kujiamulia ujumbe uliomo katika kazi anayoisoma. Kwa hivyo mafumbo hayo yanapaswa kusomwa mara kadhaa ili msomaji aelewe matini anayosoma.

iv) Usomaji ni tendo linalofanyika na kutekelezwa kwa wakati maalum, wakati wa kusomwa kwa matini huathiri maana ya matini hiyo. Fish anadai wasomaji wanapasa kufanya mikataba ya aina fulani na matini hizi katika miktadha mbalimbali.

v) Msomaji anayetumia mkakati wa mwitikio kusoma kazi ya sanaa hufuata hatua tatu katika weledi wa kazi za fasihi:

- Hurejelea kazi inayosomwa kwa tafsiri ili ithibitishwe kwamba kazi hiyo inaafikiana na yale yanayokumbukwa na msomaji.

- Hubainisha jinsi miktadha ya matini isiyohusiana moja kwa moja na maandishi inavyoweza kuhusishwa na kutangamanishwa na msomaji.

- Hudhihirisha kuwa maoni ya msomaji yanafungamana na mada muhimu za hadithi.

vi) Nadharia hii inazingatia usomaji, msomaji na upokezi. Huck (1976) anadai kuwa lengo kuu hapa ni kuwabainisha wasomaji, kuwachunguza pamoja na tendo zima la usomaji. Kwake mvuto wa watoto kwa sanaa ni kigezo muhimu katika kutathmini ubora wa kitabu cha watoto.

Naye Louis Rosenblatt (1938) katika kitabu chake *Literature and Exploration* anasema kuwa ni muhimu kwa mwalimu kuepuka kulazimisha kasumba au misimamo fulani ya jinsi wanafunzi wanapaswa kuipokea kazi fulani ya fasihi.

Kwa kuhitimisha, baadhi ya wahakiki wa kisasa wanadai uhakiki wa nadharia ya upokezi umekosa kutambua kuwa matini ina uwezo wa kupanua kuelewa kwa msomaji. Aidha, wanadai nadharia hii imewaruhusu wasomaji kufasiri matini/kazi ya fasihi jinsi wapendavyo. Maoni yetu hapa yanaafiki yale ya Iser (1976) aliposisitiza kuwa msomaji hana budi kuzielewa mbinu, kaida na kanuni zinazotumiwa katika kazi fulani ya fasihi ili kuweza kuisoma kikamilifu. Kwa hivyo, nadharia hii ni muhimu katika utafiti huu kwani inasaidia kujibia lengo la utafiti la kubainisha dhamira za ukombozi katika riwaya tajwa.

### 2.4.2 Nadharia ya Fasihi Linganishi

Boldor (2003) akimnukuu Remak (1971) anaeleza kuwa Fasihi Linganishi ni taaluma ya fasihi inayovuka mipaka ya zaidi taifa moja na kuonesha uhusiano uliopo baina taaluma ya Fasihi na taaluma nyenginezo kama sanaa (uchoraji, uchongaji, usanifu majengo na muziki), Falsafa, Historia, Sayansi Jamii (mfano: Siasa, Uchumi, Sosholojia), Sayansi, Dini na nyenginezo. Kwa ufupi, ni ufananishaji wa fasihi moja na fasihi nyenginezo na uhusiano wa taifa nyengin: Fasihi Linganishi ni mbinu ya kitaaluma inayoangaziwa katika sura mbili kubwa:- Kwanza, Fasihi linganishi ni taaluma inayojishughulisha na lugha na fasihi ya zaidi ya taifa moja na maarifa hayo yanayotumiwa katika kustawisha taaluma hasa ya Fasihi. Pili, Fasihi linganishi ni taaluma ambayo msingi na stadi yake kubwa ni kujielekeza katika itikadi ya

kuzijumuisha fasihi za jamii zote za ulimwenguni ikihusishwa na tanzu nyengine hazipewi nafasi kubwa sana na kushughulikiwa.

Kiujumla ni kwamba, fasihi linganishi ni taaluma inayojumuisha lugha na fasihi baina ya mataifa mbalimbali kwa kulinganisha ama kuonesha uhusiano uliopo kwa misingi iliyowekwa na stadi za kufanikisha taaluma hiyo.

#### 2.4.2.1 Chimbuko la Nadharia ya Fasihi Linganishi na Waasisi wake

Ponera (2014) anaeleza kuwa usuli wa dhana ya Fasihi Linganishi uko katika maneno ya Kifaransa *"la Literature Comperee"* yenye maana ya "*Compared Literature"* katika lugha ya Kiingereza na yakatafsiriwa *"Fasihi Linganishi"*kwa Kiswahili. Baadaye, huko Ulaya, dhana hii ilipewa majina mbalimbali kulingana na vipindi ilivyovipitia. Miongoni mwa majina hayo ni *"Fasihi Linganishi ya Kihistoria"*,*"Fasihi Linganishi ya Kisasa"*, *"Fasihi Linganifu ya Kimataifa"*

Dhana ya Fasihi Linganishi ilianza mwishoni mwa karne ya kumi na tisa (19) na kupata mashiko mwanzoni mwa karne ya ishirini (20). Inaaminika kuwa fukuto la kuipatia dhana ya Fasihi Linganishi umbo lililonayo sasa lilianza huko Ufaransa mnamo karne ya kumi na tisa ikijikita sana katika tamthiliya. Hii ni kwa sababu tanzu nyingine kama riwaya bado zilikuwa changa sana. Maarifa ya awali ya taaluma hii yalijikita kulinganisha maudhui ya sanaa na kaida za maisha ya kila siku ya mwanadamu na mambo yazungukayo kama vile dini, siasa na matabaka.

Wadau wakubwa wa Fasihi Linganishi mwanzoni walikuwa watu binafsi wachache waliokuwa wanafanya kazi kipwekepweke. Hawa walitoa mchango mkubwa sana

katika kuitangaza na kuieneza dhana hii. Mifano michache ya watu hao ni Paul Van Tieghem ambaye aliendesha makongamano huko Sorbonne katia ya mwaka 1827 na 1840. Pia aliandika makala na vipeperushi kuhusu dhana ya Fasihi Linganishi na kuvisambaza katika sehemu mbalimbali huko Ulaya. Katikati ya miaka ya 1800 kulikuwa na machapisho mengi ya Fasihi Linganishi kwa lugha ya Kifaransa yakiwa yametolewa na Dostoevsky na Marius Franco.

Mwaka 1886 Hutchenson Macaulay Posnett alitoa andiko zito kuhusu taaluma ya Fasihi Linganishi kwa Kiingereza na kufanya dhana hii ienee katika nchi nyingi za Ulaya Magharibi. Wataalamu wengine waliotoa mchango katika taaluma hii ni Alezander Veselovsky na Fyodor Buslaev wa Urusi, Johann Wolfgang von Goethe wa Ujerumani na Hugo Meltzl de Lomnitz.

Mtaalamu mwingine, na ambaye ndiye nembo ya taaluma hii kwa sasa, ni Steven Totosy de Zepetnek. Zepetnek ni Profesa wa uga huu ambaye amejipatia umaarufu sana katika karne ya ishirini (20). Amejikita katika kulinganisha tamaduni na asili za jamii mbalimbali na baadaye mawazo yake yakaathiri dunia nzima. Zepetnek ni mwana Fasihi Linganishi aliyejihusisha pia na taaluma za Sayansi. Alizilinganisha taaluma za sayansi na taaluma nyinginezo zinazohusu Tamaduni, Filamu, Fasihi Habari na Mawasiliano.

Zepetnek alihariri na kutunga kazi mbalimbali za Fasihi ki-ulinganishi. Akiwa Chuo Kikuu cha Martin Luther aliandika, kuchapisha na kuhakiki kuhusu taaluma ya Fasihi Linganishi takriban vitabu ishirini (20) na makala mia moja na ishirini (150). Mojawapo wa vitabu vyake maarufu ni kile kiitwacho "*Comparative Literature:*

*Theory, Method and Application (1998)"* Pia alijishughulisha na kutafsiri makala mbalimbali zilizohusu lugha za Kijerumani, Kichina, Kifaransa, Kihungaria, Kiitaliano, na Kipolandi. Kwa kufanya hivyo, alisaidia kuikuzana kuieneza Fasihi Linganishi ulimwenguni.

Kwa hivi sasa, mashiko ya taaluma ya Fasihi Linganishi yameongezeka duniani kote. Zaidi ya kuwa mojawapo ya masomo maarufu katika Vyuo Vikuu vingi, pia katika baadhi ya Vyuo Vikuu hivyo, Fasihi Linganishi imefanikiwa hata kuwa na hadhi ya kuwa kitengo au idara inayojitegemea. Fasihi Linganishi yamtaka mdau wake azitalii kazi za vipindi mbalimbali kama vile: *"Zama za Giza"* hadi zile za *"Zama za Ufufuo na Ustaarabu"*, za kabla ya Ukoloni hadi baada ya Ukoloni, na za Urasmi Mkongwe hadi zile za Ulimbwende (Uromansia) na Uhalisia.

Taaluma ya Fasihi linganishi imeundiwa jumuiya ya kimataifa ijulikanayo kama *"International Comparative Literature Association (ICLA)"* Kwa sasa, jumuiya hii hufanya kazi zake kwa kushirikiana na vyama mbalimbali vihusikavyo na taaluma hii kutoka katika kanda tofauti ulimwenguni. Kanda kuu ni

i) Chama cha Fasihi Linganishi cha Ufaransa (French Comparative Literature Association -FCLA)

ii) Chama cha Fasihi Linganishi cha Marekani (American Comparative Literature Association- ACLA)

iii) Chama cha Fasihi Linganishi cha Urusi (Russian Comparative Literature Association RCLA)

iv) Chama cha Fasihi Linganishi cha Ujerumani (German Comparative Literature - GCLA)

v) Chama cha Fasihi Linganishi cha Uingereza (British Comparative Literature-BCLA)

Kanda hizi hufanya kazi kwa kushirikia na baadhi ya mataifa madogo. Kwa mfano, kijamii Tanzania iko karibu zaidi na nchi za Ujerumani na Uingereza (Ponera, 2014).

**2.4.2.2 Mihimili / Misingi ya nadharia ya Fasihi Linganishi**

Zepetnek (1998) anafafanua misingi kumi (10) ya Nadharia Fasihi Linganishi kama ifuatavyo:

i) Kutambua taaluma hii kwa kuzingatia mbinu stadi na sahihi katika mafunzo ya fasihi kwa lengo la kuimarisha uhusiano wa Fasihi Linganishi na tamaduni nyengine.

ii) Fasihi Linganishi ni nadharia na pia ni mbinu muhimu inayodaiwa kujikita hasa katika uhusiano baina ya Utamaduni, Lugha, Fasihi na Maarifa.

iii) Kuwa na hamu ya mwana-Fasihi Linganishi mwenye uwezo mkubwa wa kutambua Lugha na Fasihi za jamii mbalimbali pamoja na maarifa mengineyo kwa undani na uhusiano wa nadharia na mbinu nyenginezo stahiki.

iv) Kuwa na hamu ya kujifunza Fasihi Linganishi ikihusishwa na stadi nyengine kama (Sanaa, Filamu, Utamaduni, Maigizo na mengineyo) ambayo nayo

yanahusishwa na matawi makuu ya taaluma ya Sayansi Jamii katika fani zake (Historia, Sosholojia, Saikolojia na nyenginezo)

v) Kutambua na kujifunza Lugha na Fasihi katika mazingira ya kuzingatia Nadharia ya Fasihi Linganishi na matumizi yake lakini mazingira hayo yakienda sambamba na lugha ya Kiingereza ambayo nayo imekitwa katika taaluma nyingi za nasaba yake.

vi) Kutambua nadharia na mbinu za Fasihi Linganishi zinazolenga na uhusishwaji wa utafiti na uchambuzi wake kwa lengo la kutolea ushahidi wake juu ya ubora na udhaifu wake.

vii) Kuwa na hamu ya kuitumia vyema Fasihi Linganishi kwa kuzingatia nadharia na mbinu na kuihusisha na mwamko wa kimawazo na kiitikadi ya siasa yake

viii) Kutambua vyema uhusiano na uhusishwaji wa kimaudhui baina ya kazi mbalimbali za sanaa kwa kuzingatia wakati, mfumo, wahusika, upekee na maudhui husika katika uhalisia au udhanaishi wake kitaifa na kiulimwengu.

x) Kuhamasika juu ya matumizi ya nadharia katika mfumo wa kiutandawazi, kiteknolojia, kiviwanda na mawasiliano katika utekelezaji wa maendeleo kwa ujumla na kuhadharika juu ya jamii, utaifa, jinsia, na mafunzo mengineyo.

xi) Kuwa na shauku kubwa ya kujifunza nadharia ya Fasihi Linganishi ili kuweza kuwa mweledi / mjuzi wa matumizi yake, katika fasihi, sanaa na matumizi mengineyo stahiki.

## 2.5 Hitimisho

Kwa kuhitimisha ni kwamba sura hii ilijumuisha maeneo muhimu ambayo nayo yamezidisha na kutoa mwelekeo mzuri wa tasnifu hii. Miongoni mwa vipengele vilivyojadiliwa ni pamoja na maana ya istilahi mbalimbali, mapitio ya kazi tangulizi, na mkabala la kinadharia na nadharia iliyojadiliwa ni nadharia ya Mwitiko wa Msomaji na nadharia ya Fasihi Linganishi. Ni imani ya mtafiti kuwa sura hii imeimarisha utafiti huu ipasavyo na kwa ukamilifu.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii imechambua vipengele vifuatavyo: Utangulizi,maana ya mbinu za utafiti,eneo la utafiti,uteuzi wa eneo la utafiti,sababu za uteuzi wa eneo la utafiti,usanifu wa utafiti,kundi lengwa,sampuli na usampulishaji,sampuli ya watafitiwa,sampuli lengwa,ukusanyaji wa data,data za msingi,dataza upili,mbinu za ukusanyaji wa data,mbinu ya maktabani,mbinu za kukusanya data za awali/msingi,usomaji wa makini,mbinu za kukusanya data za upili,upitiaji wa nyaraka,mbinu za uchambuzi wa data,mkabala wa kimaelezo,usahihi wa data za utafiti,maadili ya utafiti, baadaye ni hitimisho .

## 3.2 Mbinu za Utafiti

Chuo Kikuu Cha Abuja (1992) kinafasili mbinu za utafiti ni utaratibu maalumu wa kufuatwa au kuchunguza kitu kwa kuzingatia hali ya umakini,malengo na mantiki nzuri kwa lengo la kufanikisha kazi husika vyema.Enon(1998)anaeleza, mbinu za utafiti ni njia na taratibu zote zinazopaswa kufuatwa wakati wa ukusanyaji wa data /taarifa kulingana na aina ya utafiti. Mwaipopo (1999) anaeleza kuwa, mbinu za utafiti ni ule mpango ambao data zitakusanywa, sampuli itachukuliwa na data zitachambuliwa na kutafasiriwa.Kothari (2004) anafafanua mbinu za utafiti kuwa ni jumla ya mbinu/ taratibu zote stahiki zinazotumika wakati wa kufanya utafiti.

Kwa ujumla mbinu za utafiti ni njia,taratibu,muongozo aumpango maalumu unaofaa kufuatwa wakati wa kufanya utafiti kwa lengo la kufanikisha kazi ya utafiti kwa usahihi.Hivyo ni vigumu kwa mtafiti yeyote kufanya utafiti wake bila ya kuzingatia

na kufuata utaratibu kwa namna inavyostahiki.Ni vyema kwa mtafiti kujua mbinu za utafiti stahiki kabla ya kuanza utafiti wake.

## 3.3 Eneo la Utafiti

Kwa mujibu wa Enon(1998),eneo la utafiti la kijiografia ni pahala ambapo mtafiti amekwenda au amelitumia katika kukusanya data za utafiti wake.Pia, Babbie(1992)anafafanua kuwa eneo la utafiti ndipo data hupatikana kwa mtafiti kufanya usaili,mahojiano,kushuhudia au kushiriki shughuli au tukio fulani pamoja na watafitiwa.Kiuwazi eneo la utafiti ni sehemu, mahala, au mazingira ambayo yanatumika katika kuendeshea na kukusanyia data za utafiti.Eneo la utafiti hasa wa kitaaluma ndio kiuzi muruwa wa utafiti,kwani kupitia eneo ndipo atakapojua mtafiti atumie mbinu gani stahiki za kukusanyia data. Katika utafiti huu, mtafiti ametumia eneo la utafiti la kijiografia ambalo amelionesha katika kipengele cha uteuzi wa eneo.

### 3.3.1 Uteuzi wa Eneo la Utafiti.

Katika utafiti huu mtafiti amechagua maeneo yafuatayo:

Maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) - Tawi la Pemba, Maktaba ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA),Maktaba kuu Zanzibar - tawila Pemba.Mbali na maktaba hizo, wavuti (internet) mbalimbali zimetumika kwa ajili ya kukuza maarifa kuhusu mada ya utafiti. Sambamba na hilo, tasnifu na makala nyenginezo mbalimbali zimetumika zenye uhusiano na mada ya mtafiti.

### 3.3.2 Sababu za Uteuzi wa Eneo la Utafiti

Kwanza, Uteuzi wa maktaba tajwa,mtafiti anaamini kuwa kuwa maktaba hizo zimemsaidia sana kupata muongozo mzuri kupitia walimu na wasimamizi walioko chuoni na katika maktaba hizo teule. Marejeleo mbalimbali zikiwemo tasnifu na makala zimemsaidia sana mtafiti kupata ushuhuda mwema kulingana na mada ya mtafiti na kuimarisha utafiti huu ipasavyo.

Pili, Uteuzi wa maktaba teule za shule za Pemba, mtafiti anaamini kupitia maktaba teule anapata marejeleo ya ziada yakiwemo majarida ambayo yanamsaidia katika kuchambua na kukusanya data zinazofaa na muruwa katika kazi yake kupitia mada husika.

### 3.4 Usanifu wa Utafiti

Kothari (2008) anafasili, usanifu wa utafiti ni mpangilio maalumu unaoonesha namna na jinsi utafiti utakavyofanyika ili kuwezesha kujibu maswali ya utafiti husika. Utafiti huu umetumia mbinu ya usanifu ijulikanayo kama uchunguzi kifani katika kukusanya data.

Yin (1994) anasema kwamba uchunguzi kifani ni aina ya usanifu ambapo mtafiti huteua sehemu au jambo au kitu maalumu ambacho atakifanyia utafiti kati ya vingi vilivyopo ili aweze kukidhi mahitaji ya utafiti wake. Kothari (2008) anasema kwamba uchunguzi kifani ni mbinu ambayo humwezesha mtafiti kuufanya utafiti wake kwa gharama nafuu.

Katika utafiti huu mtafiti amechunguza kwa kina dhana ya ukombozi na ilivyosawiriwa katika riwaya ya *“Kusadikika”*na*“Vuta N’kuvute”*. Mtafiti anaamini kuwa riwaya hizi teule zinafaa na zinatosha kwa ukamilifu wake baada ya kufanya uchunguzi na baadaye uchambuzi wa kina kwa mujibu wa mada ya mtafiti. Sambamba na hilo, mbinu hii hutoa fursa kwa mtafiti kuchunguza na baadae kuchambua jambo moja kwa kina na kutosheleza mahitaji ya mada ya mtafiti.

## 3.5 Kundi lengwa

Uteuzi wa watafitiwa ni kitendocha kuchagua au kupata  kikundi fulani ili kuwakilisha kundi lengwa.Enon(1990)anaeleza kuwa uteuzi lengwa ni ule wamtafiti kwenda moja kwa moja kwenye chanzo cha data alizozihitaji ili kupata data za utafiti wake.Kundi lengwa ni jumla ya watu wote ambao huhusishwa katika utafiti (Kothari 2004), Bryman(2004),Kombo na Tromp(2006).

Uteuzi lengwa ni aina ya uteuzi ambao huteuliwa na mtafiti kwa makusudi akifahamu kuwa uteuzi huo utampatia data (taarifa) sahihi zitakazojibu maswali yake ya utafiti (Babbie,1999).Kwa mujibu wa wataalamu hao, mtafiti ameeleza kwamba, kundi lengwa ni uteuzi wa kitu au watu kidogo kati ya wengi kwa lengo la kupata taarifa zilizosahihi bila ya hitilafu yoyote.Kundi lengwa la utafiti huu ni riwaya za *Kusadikika* ya Shaban Robert na *Vuta N’kuvute* ya Shafi Adam Shafi.Uteuzi huu ni kwa sababu unampatia mtafiti kila anakachohitaji katika utafiti wake.

## 3.6 Sampuli na Usampulishaji

Prewitt(1996) anaelezausampulishaji ni  mchakato au njia ambayo mtafiti hutumia katika kupata sampuli atakayoitumia  katika utafiti wake ili  kutoa na hitimisho

kutoka katika kundi lengwa la utafiti. Babbie(1999) anaeleza kuwa, usampulishaji lengwa ni mbinu ya uteuzi wa sampuli fulani ya watafitiwa wake akiamini kuwa sampuli hiyo ni sahihi na ndio itakayompa data sahihi za kuweza kutimiza malengo ya utafiti wake.*Oxford Advanced Dictionary* (2010) wanafasili, usampulishaji ni njia, mchakato au mbinu ya kuteua kikundi fulani cha watu au vitu na kuvitumia katika kujumuisha na kutoa suluhisho au hitimisho kutoka katika kundi lengwa la utafiti. Kwa mujibu wa Kothari (2004), sampuli ni watafitiwa ambao wameteuliwa kutoka katika kundi kubwa ili watumike katika utafiti. Nae Bryman (2004) anasema, sampuli ni mchakato wa kuchagua kikundi cha vitu au watu ili kitumike katika utafiti kama kiwakilishi cha kundi lolote linalotafitiwa kwani sio rahisi kutafiti kundi zima. Mchakato wa kuteua sampuli kutoka katika kundi lengwa unajulikana kama mbinu ya usampulishaji. Sampuli hutumika kutoa taarifa zinazochunguzwa na mtafiti.Kwa hivyo mtafiti amechagua sampuli tajwa yaani sampuli nasibu kwa sababu ndio anayoamini inaweza kujibu vyema maswali na malengo ya utafiti wake

## 3.7 Aina za data

Data ziko za aina mbili nazo ni data za awali (msingi) na data za upili (fuatizi).

### 3.7.1 Data za msingi (awali)

Furlong(2000) ameeleza kuwa, Data za msingi ni zile ambazo zimekusanywa kwa mara ya kwanza na hazijawahi kukusanywa na mtafiti mwengine yeyote kwa lengo na matumizi kama yanayofanywa na mtafiti wa kwanza.Data za msingi hujulikana kama data ghafi ambazo ndio kwanza zinaingia katika taaluma ya utafiti kwa mara ya kwanza tayari kwa ajili ya kuchambuliwa. Data hizo zikishachambuliwa na kuandikwa katika ripoti au tasnifu hubadilika na kuwa ni data za upili.Kimsingi data

za msingi ni data ambazo mtafiti anazikusanya kwa mara ya mwanzo na hazijakusanywa au kuwekwa katika maandiko yoyote kabla. Mtafiti humlazimu kutafuta na kuzikusanya ama katika maandiko au vinasasauti.

Hivyo data za awali ambazo mtafiti amezitumia katika utafiti wake ni riwaya ya *Kusadikika* na *VutN'kuvute*.Mtafiti amechagua  riwaya hizi teule kwa sababu anaamini atapata mengi yanayotokana na watunzi wa riwaya hizo. Pia, aliajua mengiyanayohusiana na ukombozi na hata vipingamizi ambavyo husababisha kujikomboa na mbinu za kujikwamua kutokana na vikwazo hivyo.

### 3.7.2 Dataza upili

Creswell(2009) anasema kuwa,dataza upili ni zile ambazo tayari zilikwishakusanywa na watafiti wengine kwa ajili ya kutimiza malengo ya utafiti wao na kuandikwa katika ripoti,makala,majarida,wavuti na vitabu tayari kwa ajili ya kusoma kama marejeleo katika maktaba mbalimbali.Kwa dhahiri ni kwamba data za upili ni zile ambazo zimeshatafutwa na kukusanywa ama katika maandiko au vinasa sauti.Mara nyingi mtafiti huzipata data hizo kupitia kazi za watu waliokwishazikusanya katika kazi zao na kwa hivyo hujulikana kama ni marejeleo ya kazi stahiki.

Katika utafiti huu, data za upili ambazo mtafiti amezitumia ni kupitia tasnifu, makala, vitabuna majarida mbalimbali yenye uhusiano na mada ya mtafiti. Mtafiti ameamini kupitia data za upili atapata muongozo wa kutosha unaomsaidia katika kufikia hatima ya utafiti wake. Vile vile, kupitia data hizo zikiwemo tasnifu ni dhahiri kuwa zimemsaidia kujua ni kiasi gani watafiti waliopita wamefanikisha katika kufanyia utafiti riwaya za Shaban Robert na Shafi Adam Shafi na ni maeneo

waliliyochagua kutafili hapo awali.Aina nyengine ya data za upili amezitumia mtafiti katika utafiti wake ni wavuti na baadhi ya vyombo vya habari ikiwemo redio na televisheni, hizi zimemsaidia mtafiti kupata data za ukweli na usahihi zenye mnasaba na mada ya mtafiti.

### 3.8 Ukusanyaji wa data

Enon (1998) anafasili kuwa, ukusanyaji wa data ni zoezi la awali katika utafiti, zoezi ambalo humuwezesha mtafiti kupata taarifa alizokusudia ili kumfikisha katika lengo la utafiti. Kothari (2004) anafafanua kuwa, ukusanyaji wa data ni kama zoezi la awali katika utafiti ambalo humuwezesha mtafiti kupata taarifa alizozikusudia ili kumfikisha katika malengo yake ya utafiti.

#### 3.8.1 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Mbinu za kukusanya data ni dhana ya ukusanyaji wa data kuwa ni zoezi la awali katika utafiti ambalo humuwezesha mtafiti kupata taarifa zilizokusudiwa ili kufanikisha lengo la utafiti.Kothari(1990) anaelez kuwa, mbinu za kukusanya data ni njia au mbinu au mpango anaokusudia mtafiti kuutumia katika kutafuta na kufanikisha zoezi la utafiti wake. Mbinu hizo zinaweza kuwa maktabani,uwandani/ maskanini au hata maabarani.Uteuzi sahihi wa mbinu unategemea kulingana na utafiti anaofanya mtafiti. Katika utafiti huu mtafiti ametumia mbinu ya maktabani kwa sababu anaamini inamrahisishia kupata taarifa anazozihitaji kwa urahisi kupitia vitabu teule vya *Kusadikika* na *Vuta Nkuvute* na kulingana na mada yake ya utafiti

### 3.8.2 Mbinu ya Maktabani kupitia Usomaji Makini

Usomaji makini au usomaji wa kina ni mbinu ya kukusanya data za msingi kutoka kwa matini tafitiwa zilizoteuliwa katika utafiti husika (Kothari,1990). Mtafiti kupitia utafiti huu amepitia kwa kina, neno kwa neno, sentensi kwa sentensi, aya kwa aya na mfano wa hayo kuanzia mwanzo hadi mwisho wa riwaya teule na wakati anasoma kwa kina amerikodi / kunukuu maeneo muhimu yanayoendana na maswali na malengo ya mada ya utafiti wake pamoja na kurasa zake katika daftari/shajara maalum aliloliandaa kwa kazi hiyo na kwa lengo la kujiridhisha na kutimiza shauku ya mada husika. Sambamba na hayo taarifa / data ambazo amezinukuu mtafiti amezitumia katika uwasilishaji na uchambuzi wa data hizo baadaye na kwa usahihi.

### 3.8.3 Upitiaji wa Nyaraka

Kimsingi mbinu ya upitiaji wanyaraka maktabani ni mbinu ya kukusanya data za upili kwa mtafiti katika kukusanya machapisho yanayohusiana na mada yake ya utafiti na kuyasoma kwa uzingativu (Kothari, 1990). Katika utafiti huu mbinu ya upitiaji nyaraka kwa marejeleo ya magazeti, majarida, vitabu au machapisho mbali mbali yalitumikakwa uzingativu na umakini wa hali ya juu kulingana na malengo, maswali na mada ya utafiti.

## 3.9 Mbinu za Uchambuzi wa Data

Kothari (2013) anaeleza kuwa, ukusanyaji wa data ni kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo itasaidia kujibu maswali ya utafiti husika.Wakiunga mkono hoja hii Bagdam na Biklen(1992) wakinukuliwa na Omari(2011)kuwa, hii ni hatua muhimu sana katika kutafuta majibu ya tatizo la

utafiti husika. Zipo mbinu kadhaa za uchambuzi wa data lakini data za utafiti huu zitachambuliwa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi maudhui.

Kwa mujibu wa Kombo na Tromp (2006), mbinu ya uchambuzi maudhui ni mbinu ambayo huziweka data kulingana na jinsi zinavyofanana na kuhusiana.Kiujumla ni kwamba, mbinu za uchambuzi wa data ni kitendo kinachotumika katika kuchambua data kwa kutafuta na kuchagua taarifa zinazopatikana katika uchambuzi wa data hizo kwa kuzifupisha ili kupata zilizosahihi baada ya kulinganisha na kutafautisha data hizo na madhumuni ya utafiti unaokusudiwa kufanywa. Mbinu hizo zinaweza kuwa katika mkabala wa kimaelezo au mkabala wa kitakwimu.Katika utafiti huu mtafiti ametumia mkabala wa kimaelezo kwa sababu utafiti wake umejikita katika upande wa fasihi na fasihi inahusiana zaidi na maandishi kuliko nambari.

### 3.9.1 Mkabala wa Kimaelezo

Kothari(1990) anasema kuwa, mkabala wa kimaelezo ni mbinu ya uchambuzi wa data ambapo mtafiti huzichambua data zake kwa kuzitolea maelezo yanayohusiana na madhumuni ya utafiti wake.Mkabala wa kimaelezo ni mbinu anazotumia mtafiti katika kuchambua data zinazohusiana na kazi yake ya utafiti. Katika utafiti huu mtafiti ametumia mkabala huu kwa sababu anaamini unamsaidia sana kufanikisha tasnifu hii. Sambamba na hilo mtafiti ametumia njia hii ni kutokana na ukweli kwamba mbinu hii inatoa uhuru zaidi katika uchambuzi hususan upande wa fasihi. Pamoja na hayo, matumizi ya mbinu ya kitakwimu yametumika kwa kiwango kidogo na kwa lengo la kurahisisha ufahamu na ufupisho/muhtasari wa vipengele vinavyojadiliwa.

### 3.10 Usahihi wa Data za Utafiti

Cohen na wenzake (2000) wanafafanua kuwa, usahihi wa mbinu za kukusanyia data ni utaratibu wa utafiti na kuhakikishwa na kuzingatia matumizi ya mbinu maalum za ukusanyaji na uchambuzi wa data za utafiti. Mbinu zinazotumika ni mbinu ya usomaji makini kupitia maktaba kwa data za awali na mbinu za upitiaji wa nyaraka kwa data za upili. Katika uchambuzi wa data wa kina na mkabala wa kitakwimu kwa kiwango kidogo cha kufanya muhtasari na urahisishaji wa ufahamu wa data zinakazochanganuliwa.

### 3.11 Kuaminika kwa Data

Kothari (2008) anaeleza kuwa, kuaminika kwa data za utafiti kunatokana na uwezo wa mbinu za utafiti kutoa matokeo yaleyale utafiti unaporudiwa kwa kutumia mbinu zilezile. Furlong na Lovelace (2000) nao wanafasili kuwa, kuaminika kwa data hujitokeza pale ambapo huwepo uhusiano au ulinganisho katika taarifa zilizotolewa na watu walewale au vyanzo kadhaa kwa muda tofauti. Katika utafiti huu, kuaminika kwa data kulihakikishwa kwa kutumia mbinu za kukusanyia data ambazo ni mbinu ya usomaji makini kupitia maktaba na mbinu ya upitiaji wa nyaraka.

### 3.12 Maadili ya Utafiti

Maadili ni dhana muhimu katika muktadha wowote ikiwemo misingi ya kitaaluma kama ilivyofasiliwa kutoka vyanzo mbalimbali: TUKI (2004) wanafasili kuwa, maadili ni kama onyo/katazo kuhusu jambo fulani. BAKIZA (2010)wanaeleza wanaelea kuwa, maadili ni mwenendo unaokubalika katika jamii fulani au mafunzo ambayo yanahusu mwenendo mwema.Kwa ujumla, maadili katika utafiti ni pamoja na mazingatio ya nidhamu, heshima, mafunzo, mwenendo mwema, adabu pamoja na

maonyo yanayolenga kuzingatiwa na kuthaminiwa na mtafiti katika shughuli au kazi nzima ya utafiti kuanzia mwanzo hadi mwisho ikiwemo uzingativu wa nidhamu hizo wakati wa kukusanya data kutika utafiti na uchambuzi wake.Kwa kuzingatia misingi hiyo maadili ya utafiti yamelenga kwa mtafiti kuwajali watafitiwa wake ipasavyo pamoja na vyanzo vyenginevyo vya upatikanaji wa taarifa sahihi za utafiti ili kuweza kuzifanya taarifa ziwe thabiti na zenye kuaminika kwa kiwango cha juu. Miongoni mwa mambo muhimu katika maadili ni kutunza au kuhifadhi siri za mtafitiwa/watafitiwa, vyanzo vya upatikanaji wa taarifa.Pia, ni kuheshimu thamani ya data hizo na kuzieleza kadiri zilivyowasilishwa kutoka chanzo husika na kutotoa taarifa hizo kusikohusika.

## 3.13 Hitimisho

Kwa muhtasari sehemu hii imezidisha thamani ya utafiti huu na kuufanya uzidi kuleta ladha na ubora wa hali ya juu. Kwa hakika vipengele vilivyojadiliwa vina umuhimu mkubwa katika utafiti huu. Baada ya utangulizi vipengele vilivojadiliwa ni pamoja na dhana ya mbinu za utafiti, mbinu za uteuzi wa eneo la utafiti, uteuzi wa eneo la utafiti na sababu zake, usanifu wa utafiti, sampuli na usampulishaji, data za awali na data za upili**,** mbinu za ukusanyaji na uchambuzi wa data, usahihi, kuaminika na maadili ya utafiti na mwisho ni hitimisho.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Sura hii imejikta zaidi katika kuwasilisha, kuchambua na kujadili data zilizopatikana katika riwaya husika ambazo ni riwaya ya *Kusadikika* na *Vuta N'kuvute*.Katika sura hii, mtafiti ameanza na historia ya mtunzi wa riwaya ya *Kusadikika* ambayo imejumuisha uwandishi wake, falsafa yake, kifo na kumbumbu yake. Baada ya hapo amefafanuahistoria ya mtunzi wa *Vuta N'kuvute*.Vile vile kuna muhtasari wa riwaya ya *Kusadikika,* muhutasari wa riwaya ya *Vuta N'kuvute,* ubainishaji wa dhamira za ukombozi zilizomo katika Kusadikika, ubainishaji wa dhamira za ukombozi zilizomo katika riwaya ya *Vuta N'kuvute,* ulinganishaji wa dhamira zilizofanana katika riwaya hizo, utafautishaji wa dhamira zilizotafautiana katika riwaya teule na baadaye ni hitimisho. Uchambuzi wote huo umezingatia maswali na malengo ya utafiti vyema.

## 4.2 Historia ya Shaaban Robert kwa Ufupi

Shaaban Robert alizaliwa tarehe 01 Januari 1909.Robert alianza shule mwaka 1922 na kumaliza mwaka 1926katika shule ya Kichwale ambayo kwa sasa inafahamika kama Uhuru Mchanganyiko.Alipenda sana kusoma na alijiendeleza kielimu lakini jitihada zake hazikuzaa matunda kwa haraka kwa sababu aliporwa na wakoloni kwa lengo la kumtumia kama chombo cha kutawalia.Hata hivyo mwaka 1932 aliendelea na masomo kwa njia ya posta ambapo mwaka 1934 alitunukiwa Diploma ya Fasihi.Mwaka 1936-1937 alitunukiwa Cheti cha English Level.Ni dhahiri kuwa Shaaban Robert alikuwa ni mtu mwenye juhudi kubwa katika kujiendeleza kielimu na kama si wakoloni angalifika katika ngazi za juu zaidi. Ilipofika mwaka 1926

aliaajiriwa na serikali ya Kikoloni kama karani na kuanza kazi katika idara ya Forodha -Tanga,ambapo alidumu kwa miaka takriban 18.Mwaka 1944-1946 alihamishiwa idara ya Wanyamapori huko Mpwapwa.Bila shaka kukaa kwake miaka mingi hivi katika mji wa kihistoria uliokuwa mahala pa utamaduni wa Kiswahilitena kumesaidia maendeleo yake kama mwandishiwa Kiswahili.Mwaka 1946 alirudishwa Tanga na kuwa Afisa wa Ardhi wa jimbo la Tanga. Aidha barua zake zilionesha kwamba aliwahi kufanya kazi katika mikoa ya Kilimanjaro,Arusha,Dar-es-salam na Kisiju.

Maandishi yake ya awali yalikuwa ya kishairi katika jumla ya kazi alizoziandika. Ameandika mashairi mengi zaidi ya kazi za kinathari.Kwa wanafasihi wengi Shaaban ni mshairi zaidi ya kuwa mwandishi wa riwaya. Mbali na maandiko yake alikuwa naathari kubwa katika maendeleo ya lugha ya Kiswahili akiwa mjumbe wa kamati za *East Africa Swahili Committee,East Africa Literature Bureau na Tanganyika Languages Board.* Maeneo aliyofanyia kazi ni pamoja naIdara ya Forodha Pangani mwaka 1926 hadi 1944,Idara ya Wanyama pori tokea mwaka 1944 hadi 1946,Afisi ya Mkuu wa Jimbo Tanga tokea mwaka 1946 hadi mwaka 1952 na Afisi ya kupima nchi tokea mwaka 1952 hadi mwaka 1953.

Ailipandishwa cheo na kuwa Grade III Higher Division mwaka 1926,na katika mwaka wa 1944 akapandishwa tena kuwa Grade II local Service.Alikuwa mwanachama wa Taasisi tatu ambazo mtafiti tayari ameshazitaja hapo juu.

#### 4.2.1 Uwandishi na Kazi zake

Mzee Shaban Robert aliandika vitabu ishirini na mbili ambavyo vyengine vimetafsriwa katika lugha mbalimbali ikiwemo Kichina,Kiingereza na Kiurusi.Vitabu vyake alivyotunga ni pamoja na: *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini (1949), Kusadikika (1951), Adili na Nduguze (1952), Wasifu wa Siti bint Saad (1967), Kufikirika (1968), Siku ya Watenzi Wote (1967)*

#### 4.2.2 Falsafa yake

Watu wengi ambao wamesoma kazi za Shaaban Robert wanasema kuwa kazi zake zimeonesha msimamo fulani ambao unatokana na falsafa yake juu ya maisha kwa ujumla.Binaadamu aghlabu hufikia msimamo katika maisha baada ya kutafakari sana na kupata busara na mantiki fulani katika maisha hayo.Busara inayofikiwa na binaadamu huwa ndio falsafa yake,yaani falsafa ni busara inayofikiwa baada ya mtu kuwa katika harakatiza kutafakari juu ya jambo lolote la kilimwengu. Falsafa ya binaadam yoyote ni lazima iwe na misingi yakekatika jamii au mambo mengine yaanayohusiana na binaadamu wengine. Kwa mfano,falsafa ya Shaaban ilifika katika dini na utamaduni; dini hasa ya Kiislamu ilimuathiri sana Shaaban. Alizingatia mambo mengi yaliyoasisiwa na dini.Katika kazi zake zote alisisitiza mambo kama vile haki,usawa, uadilifu,ukarimu n.k. Aliamini kuwa mtu yoyote aliyekuwa na utu siku zote alikuwa na nafasi ya kufaulu duniani na mtu muovu alielekea kuangamia.Huu ndio ujumbe kwa mfano unaojitokeza katika kazi zake kama vile*Adli na Nduguze, Kufikirika* na *Kusadikika.* Ingawa falsafa yake ilijikita katika dini na utamaduni lakini vilevileiliathiriwa sana na maandishi ya wanafalsafa wengine wa ulimwengu kama vile Voltaire,katika utangulizi wa *Koja la lugha.*

*Voltaire* ni mmoja katika walimu wakuu waliokuwa mahiri kabisa kwa kazi zao ambae alitokea Ufaransa.

### 4.2.3 Kifo na Kumbukumbu

Shaaban Robert alifariki mkoani Tanga tarehe 22 Juni 1962. Alizikwa Machui hukohuko Tanga.Alitunzwa kwa zawadi ya mwandishi inayoitwa “Margaret Wrong Memorize Prize”.

## 4.3 Historia fupi ya Shafi Adam Shafi

Shafi Adam Shafi jina lake hasa ni Adam Shafi Adam alizaliwa mwaka 1940 Mwembe Kisonge, mjini Zanzibar. Baba yake ni mzee Shafi Adam Hila aliyekuwa ni mfanyabiashara katika maeneo ya Kwahajitumbo mjini Zanzibar. Alikuwa na asili ya Komoro. Mama yake ni bi Riziki aliyekuwa ni mama wa nyumbani na alijishughulisha na biashara ndogo ndogo.

Adam Shafi alisoma skuli ya msingi ya French Comorian School ambayo kwa sasa inajulikana kwa jina la Hamamni. Alisoma shuleni hapo tangu darasa la kwanza hadi la sita. Baadaye alijiunga na skuli ya Gulioni Primary School ambapo sasa ni sehemu iliyojengwa Benki Kuu ya Tanzania (BOT) .Katika shule hiyo, Shafi alisoma darasa la saba hadi la nane.Baada ya kufaulu mwaka 1957 alipata nafasi ya kujiunga na Chuo cha Sayyidi Khalifa Teacher Training College ambachokwa sasa ni Chuo Kikuu cha Taifa Cha Zanzibar(SUZA).Katika chuo hiki yeye na wenzake walikuwa wakisoma miaka minne kwa sababu walikuwa wakisoma masomoya secondari pamoja na mafunzo ya ualimu wa msingi,kwa kiwango cha cheti.Katika Chuo hiki Adam Shafi alipata hamasa ya kwenda chuo cha nje,kuandika kazi za kifasihi na

hamu ya kujishughulisha na harakati za kisiasa.Licha ya vikwazo vilivyojitokeza, Adam Shafi alifanikiwa kusoma Diploma katika fani ya siasa ya uchumi katika chuo cha Fritz Heckert mwaka 1963 huko Ujerumani na alipata mafunzo ya uandishi wa habari katika vyuo tofauti kama Prague nchini Czechoslavakia ambayo sasa ni jamhuri ya Czech mwaka 1964 hadi mwaka 1965. Pia aliwahi kupata mafunzo nchini Sweden mwaka 1982 na nchini Marekani mwaka 1983.

Mtunzi huyu alishiriki kikamilifu katika harakati za siasa ya Zanzibar kwa kushiriki katika vyama vya wafanyakazi na hata vyama vya kisiasa kabla ya mapinduzi ya Zanzibar ya 1964. Alianza harakati za uandishi wa vitabu akiwa katika Chuo Cha Sayyid Khalifa na kutoa kitabu chake cha kwanza cha *Kasri ya Mwinyi Fuadi* mwaka 1978.Kazi nyengine alizotunga ni *Kuli (1979),Vuta n'kuvute (1999), Mbalina nyumbani(2013)*. Pamoja na kushiriki katika harakati za ukombozi Zanzibar alituhumiwa kushiriki katika njama za mauaji ya hayati Abedi Amani Karume ambaye alikuwa ni Raisi wa kwanza wa Zanzibar. Hivyo alifungwa miaka mitatu na baadaya kufunguliwa alifukuzwa kazi katika kampuni ya Publishing Center mwaka (1974) na hii ndio iliyokuwa sababu ya kuhamia Dar es salam na hadi sasa yuko huko kimaisha.

### 4.3.1 Uwandishi wake

Katika kuendeleza kazi yake ya fasihi, Adam Shafi alitunga vitabu pia amewahi kuwa mwenyekiti wa Umoja wa Uwandishi wa Vitabu (UWAVITA) kuanzia mwaka 1998 hadi 2002 na ni miongoni mwa watu wachache waliowahi kuwa wanasiasa mashuhuri na kuwa wachangiaji wakubwa wa maendeleo ya fasihi Tanzania

## 4.4 Muhtasari wa Riwaya ya *Kusadikika* ya Shaaban Robert

Kwa ufupi riwaya ya *Kusadikika* imekusanya maeneo kumi na mbili. Katika ukurasa wa (v) ni utangulizi ambao umeonesha picha nzima ya nchi ya Kuasadikika na mambo yote yaliyomo katika nchi hiyo ambayo yana utafauti mkubwa na nchi nyengine zinazoonekana katika mazingira halisi. Mwandishi anaielezea nchi hiyo kwa kusema kuwa:

> "Kusadikika ni riwaya inayosawiri nchi iliyoko angani na wananchi wake,nchi ambayo kuwepo kwake ni kwa kusadikika tu.Hii ni ishara ya kuwa mtunzi amechora picha halisi inayoonesha maisha ya wanajamii kuwa yanaweza kuwa katika hali kama ilivyoelezewa katika riwaya hii.Kusadikika na nchi ambayo kuwepo kwake ni kufikirika kwa mawazo tu, nchi hiyo iko katikati ya mipaka sita.Kwa upande wa Kaskazini imepakana na upepo wa Kaskazi,upande wa Kusini imepakana na upepo wa kusi.Mashariki imepakana na Matlai, na Magharibi mpaka wake ni Upepo wa Umande.Kwa kuwa nchi yenyewe inaelea katika hewa kama wingu, zaidi ya kupakana na pepo nne hizo, ina mipaka mengine miwili ambayo ni kwa juu mpaka wake ni mbingu na kwa chini ni ardhi.Wanawake wote katika nchi hiyo huzaa pacha. Hii ni habari ya ajabu sana lakini haionekani kuwa imepata kugusa ndoto za wazee"(uk:v)

Ukurasa wa kwanza hadi wa tano inaonekana ni serikali ya Kusadikika ambapo waziri Majivuno alikuwa ni waziri wa wafalme watatu, pia ni serikali iliyongozwa kwa kurithishana mamlaka.Mwandishi ameanza kwa kusesema:

> "Waziri wa kusadikika alikuwa mtu mwenye haiba kubwa na uhodari mwingi, kwa hivi aliitwa Majivuno. Uwaziri wake ulianza zamani sana .Alikuwa waziri wa wafalme watatu katika nyakati mbali mbali, babu yake mfalme aliyesimuliwa aliposhika ufalme yeye alishika uwaziri, baba yake alipokuwa nahodha wa chombo cha serikali, yeye alikuwa rubani wake,akaendelea katika hadhi mpaka enzi za ufalme mpya" (uk:1).

Pia, mashtaka ambayo muhusika Karama ni mshtakiwa na waziri Majivuno ndiye muendeshaji wa kesi hiyo. Waziri huyu alikuwa na sifa ya ujinga wa kupindukia kiasi ambacho hakujielewa yeye mwenyewe ila alijiona kama anakuwa katika mstari uliosahihi kwa kila anachofanya na kusema, hivyo anajisifu mbele ya baraza kuwa ni mtendaji aliyemakini.Mwandishi anasema:

> "Kwa sababu ya kudumisha sheria, dini na mamlaka na kwa mujibu wa kazi yangu,lazima nidhihirishe mbele ya baraza hii kuwa si jambo jema hata kidogo kuamuru madarasa ya utaalamu na uwezo kuwa daraja ambalo chini yake utapita mambo ya kuichafua salama ya Kusadikika kwa dharau, ukaidi na jinai"(uk:1).

Ukurasa wa sita hadi wa tisa ni uanasheria ambapo mwandishi amemtumia muhusika Majivuno kama ni kiongozi aliyejaa jeuri,ari, kejeli, inda na taadi kwa wananchi wake. Mwandishi anasema:

> "Majivuno, mtu aliyejihesabu mwenyewe kuwa kidole chake kidogo kilikuwa na akili nyingi kuliko vichwa namiili ya Wasadikika wote,ikiwekwa pamoja"(uk:6).

Kwa upnde mwengine, mtunzi ametoa wasifu wa mshtakiwa Karama kuwa ni mtu aliyeonekana kama kiumbe duni kwa wasifu wa nje ila kwa wasifu wa ndani ni kiumbe aliyepambika kwa sifa kadhaa ambazo zilionekana kuwa tunu kwa Wasadikika wote.Mtunzi anathibitisha hayo kwa kusema:

> "Kwa wasifu wa nje mshtakiwa alikuwa hana umbo la kufanya mvuto kwa watu ila wasifu wa ndanialikuwa na ajabu tatu, kichwa chake kilikuwa na ubongo wa hekma, kifuani alikuwa na moyo wa ushujaa, kinywani ulimi wa ufasaha,vipawa hivi vilikuwa katika siri kubwa sana"(uk:7).

Katika ukurasa wa nane alitakiwa mshitakiwa atoe elimu juu ya uanasheria akafanikisha kuitoa ila kwa vile serikali imo katika kiza hakuaminika badala yake aliitwa mudiri wa sheria na kuitafsiri sheria kwa namna anavyotaka yeye ili kumridhisha waziri wake.

Ukurasa wa kumi hadi arubaini na sita ni safari zawajumbe sita waliojiteua bila kulazimishwa kuelekea katika miji mbalimbali kwa lengo la kutafuta ushahidi juu ya kesi ya mshtakiwa. Katika safari zao wanakumbana na vikwazo tofauti ila hawaoni wala hawajali vikwazo hivyo isipokuwa kuzidi kusonga mbele na kutarajia matumaini yaliyomazuri.Mwandishi anasema:

> “Kila alipokutana na shida, ndipo bidii yake ilipozidi kukua.Baadhi ya watu hulegea mioyo mbele ya dhiki,lakini wengine hukazana mpaka wameishinda.Bidii ya Buruhani ilifanya mwangaza kama wa taa mbele yake,akazidi kupanua hatua kufululiza katika kazi aliyotumwa kwa uthabiti na furaha kubwa”. *(Kusadikika uk:11)*.

Maelezo haya yameoneshwa kwa Buruhani ili ijulikane ya kwamba hakuna mjumbe kati yao alidiriki kurudi nyuma bila ya kupata alichokusudia, wote walikwenda kwa furaha bila ya kujali vituko walivyoviona.

Ukurasa wa arubaini na saba hadi arubaini na tisa ni huku juu ya kesi ya mshtakiwa ambayo ilisimamiwa na kutolewa na mfalme mwenyewe. Kwa bahati njema, mshtakiwa hakuwa na hatia wala wajumbe wake wote sita hawakuwa na haja ya kutiwa gerezani na kuteswa baada ya kujulikana kwamba wanachokifanya kizuri na kina mafanikio makubwa kwa nchi yao.Kutokana na sababu hizo, mfalme aliidhinisha wafunguliwe na walipwe fidia kutokana na mateso yote waliyoyapata dhidi ya serikali yao. Mwandishi anasema:

> "Wanastahili uhuru na heshima kubwa, hasara zao lazima zifidiwe Kusadikika inamshukuru sana Karama kwa kuitanabahisha wajibu wake". (uk:48).

Kutokana na sababu hiyo, mwandishi alimchora Karama na wajumbe sita kama ni kikomboleo cha madhila hayo dhidi ya jamii yao. Hivyo basi, mwandishi ameonesha kwamba siku zote umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu kwa sababu kushiriki vyema kwa wajumbe hawa kulisaidia sana kujenga Kusadikika mpya.

Ama katika ukurasa wa hamsini hadi sitini na tano ni kielelezo ambacho kinatoa maana ya maneno na maswali juu ya yale yaliyomo ndani ya kitabu na hapo ndipo mwisho wa kitabu cha *Kusadikika.*

## 4.5 Muhtasari wa*Vuta N'Kuvute*ya Shafi Adam Shafi

*Vuta N'kuvute* ni riwaya ya Shafi Adam Shafi iliyochapwa kwa mara ya kwanza mwaka 1999 na kampuni ya Mkuki na Nyota Publishers. Kitabu hiki kina jumla ya sura kumi nanane na kukamilishwa kwa tamati. Pia hii ni riwaya ya tatu kutungwa na kuchapishwa katika kazi za Shafi Adam Shafi. Kazi hii ni ya kwanza kuanza kupata ubora katika ubunifu baada ya kupata uzoefu kupitia kazi zake mbili za mwanzo.Kazi hii imetolewa sanifu mpya mwaka 2014 ambayo tofauti yake ni kupungua kurasa tu, si hivyo tu kazi hii imepambika na kupendeza kwasababu imetumia mbinu zote za kifasihi kama wanavyotumia watunzi wengine wa kazi za kifasihi.Mwandishi ametumia mtindo wa matukio ya kihistoria,kutumia fasihi simulizi ndani ya fasihi andishi kwa kutumia nyimbo za kila aina,methali,mtindo wa barua n.k

Katika kuchambua tunaona sura ya kwanza inaanza kwa kumueleza Yasmin na muumewe Bwana Raza, mwandishi anaanza kwa kuchora taswira ya uzuri wa Yasmin yenye kujenga mvuto na hamu ya kusoma kazi hii ili msomaji aone hatima ya kazi hii. Kwa mujibu wa Shafi, Yasmin ni mtoto wa Kihindi mwenye ya kuvutia.

> "Yasmin alikuwa na kijuso kidogo cha mdawiri,mfano wa tungule na macho makubwa ambayo kila wakati yalionekana kama yanalengwalengwa na machozi.Alikuwa na pua ndogo nyembamba na chini ya pua hiyo ilipangana midomo miwili mizuri iliyokuwa haitulii kwa tabia yake ya kucheka cheka" (uk:1).

Pia sura hii imeeleza mazingira ya ndoa ya Yasmini na mume wake wa kwanza ambaye ni Bwana Raza na namna alivyokuwa akiishi naye. Bwana huyu alikuwa mtu mzima, muhindi kama alivyo Yasmin na alikuwa mfanya biashara. Hata hivyo hakuwa chaguo sahihi la Yasmin kuishi naye kama mume. Bwana Raza aliamua kuhama Zanzibar kwenda Mombasa ndoa yao inakumbwa na matatizo ya hapa na pale kutokana na kutoridhika kwa Yasmini kuolewa na Bwana Raza.Yasmin alivutika na mji wa Mombasa ila kwa bahati mbaya hakuvutika na aliyekwenda naye kwani alikuwa ni mtu asiyefanana naye kiumri,hivyo ilipelekea kupendana na mtu asiyekuwa kabila lake ambaye alikuwa ni Bukheti hadi akaamua kumfuata wakati Yasmin alipomtoroka mke wake na kuja Zanzibar.

Katika sura ya pili mpaka ya tano, mtunzi anaonesha jinsi Yasmin anavyioingia Unguja kutoka Mombasa, anafika kwao  na kufukuzwa na mjomba wake kwa kumtoroka Bwana Raza. Kuanzia hapo Yasmin anahamia Uswahilini na kujikita na mambo yote ya Waswahili bila kizuizi chochote. Anakwenda kwa Mwajuma ambaye alikuwa ni shoga yake wa zamani wakati alipokuwapo Zanzibari Yasmin anaishi

maisha mapya na anakuwa katika mazingira mengine magumu na ya dhiki kwa siku za mwanzo kwasababukila mtu kwake ni mgeni pamoja na mambo yote aliyoyaona kwake yalikuwa ni kikwazo kikubwa hadi kufikia kuyazoea. Baada ya muda kuyazoea na kuwa kama aliyezaliwa nayo. Mwandishi anatueleza juu ya ushoga wa Mwajuma na Yasmin kuwa:

> "Siku zilivyozidi kupita ndipo ushoga waYasmin na Mwajuma ulivyozidi kustawi mfano wa bustani iliyokuwa ikitiliwa maji kila siku.Baina yao hapakua na ugomvi wa kutafautiana na wote wawili wakawa na maisha ya bahati nasibu,leo wapae kesho wakose" (uk:44).

Sura ya sita mpaka ya kumi na mbili zinatuonesha namna Denge anavyoendesha mapambano ya kuwapinga wakoloni wa Kiingereza waliokuwepo Zanzibar kwa kushirikiana na Mambo, Chande, Yasmin na wengineo. Mwandishi anasema:

> "Najua sana kuwa polisi wananitafuta kilan'napokwenda lakini nimewashinda ujanja.Hata wakinikamata wakanifunga kazi hii ataendelea kwani siko peke yangu,tupo wengi Zanzibar,Dar es salam,Ulaya na kila pahali duniani" (uk:108).

Mapambano yameendelea kwa njia mbalimbali na kushirikisha wazalendo na wafanyakazi wanaodhalilishwa, walisambaza vikaratasi kwa ajili ya kuelimisha wazalendo na kutoa propaganda juu ya wakoloni. Pia walitumia maandamano, migomo na hata kuwafanyia fujo wakoloni katika sehemu zao za starehe.Wakoloni nao walitumia njia na mbinu mbalimbali za kuvunja jitihada za wazalendo.Pamoja na hayo, juhudi za wakoloni zilishindwa kama anavyoeleza mwandishi:

> "Waliingia ndani na baada ya kuingia tu Yasmin alimkabidhi Denge yale makaratasi. "Koplo Matata kanambia niyalete kwako lakini wewe asijuwe kama nimeyaleta" (uk:137)

Wakati Yasmin alitumiwa na wakoloni anaamua kuungana na mpenzi wake Denge na wanajaaliwa kupata mtoto wa kiume, ambaye baadaye alipelekwa Donge kwa mama yake Mwajuma kwenda kulelewa. Pia Yasmin anapendana na Shihabu na hatimaye kuolewa kabisa na bwana huyu ila nahuku anakuwa ni mpenzi wa Denge. Mwisho Shihab anakufa kwa kihoro cha kuoza kutokana na kumpenda Yasmin.Si hivyo tu, Yasmin anatumiwa na wakoloni, anaamua kuwasaliti na kuungana na mpenzi wake Denge. Naye Denge anapenda harakati zake za ukombozi na nimkuu wa harakati hizo na muunganishaji wa harakati hizo baina ya wale walioko Dar es salam na walioko Ulaya na Zanzibar.Mtunzi anasema:

> "Alichukua moja na kumpa Mambo "soma"alimpa karatasi moja iliyokuwa imechapwa kwa maandishi makubwa. Alisoma 'kufa au kupona tunataka uhuru" (uk:166).

Hali hii inaonesha namna gani alikuwa na simanzi ya ukoloni zaidi kuliko kumfikiria Yasmin.

Sura ya kumi na tatu mpaka ya kumi na nne inaonesha namna matukio yanavyoshuka chini kwa kukamatwa na kutiwa ndani wanaharakati wa kupigania uhuru.Wakoloni walianza kumkamata Denge na wenzake.Waliwafungulia kesi zisizokuwa na ushahidi.Hata hivyo hali hii haikuwavunja moyo,walipotoka ndani waliendelea na harakati kama kawaida. Yasmin akiwa na mume wake Shihab huko Tanga, maisha ya utawala yalianza kumshinda na kufanya juhudi ya kumtoroka kama alivyofanya kwa Bwana Raza. Mvuto wa Yasmin kwa Bukheti haukuishia Mombasailibidi amfuate Unguja na kumsaka nyumba hadi nyumba. Alifanikiwa kumkuta na kwa hivyo kiu yake ikaanza kukidhiwa haja yake. Yasmin hakuwa na mapenzi na Shihab

wala Bukheti bali alikuwa amevutika na Denge aliyemfanya kuwa mwanaharakati wa kupigania uhuru na kusaliti ubaguzi wa Wahindi  wa kutotaka kuolewa na Waswahili.Yasmin anampenda Denge ambae sasayuko gerezani. Wakati huohuo Bukheti anampenda Yasmin ila Yasmin alimtaka Bukheti ashiriki katika kumtorosha Denge kutoka gerezani.Mipango ya Denge kutoroka ilipangwa na Mambo, Panzi, Yasmin, Mwajuma na washiriki wengine.Hali hii ilileta vuta n'kuvute kati ya kupigania uhuru na mapenzi kwa Yasmin alivutwa na Bukheti nayeye anamvuta Denge kama inavyoelezwa:

> Denge alipanda ngazi ambayo Mambo ameizua ngazi kwa chini, Yasmin ameizuia ngazi kwa juu.Bukheti anamvuta mkono Denge kumsaidia kupanda jahazi, alipanda mpaka juu akaingia ndani akaangukia juu ya mikono ya Yasmin wakakumbatiana wameng'ang'aniana kama kupe akiing'ang'ania ngozi…Yasmin na Bukheti walishuka kutoka jahazini nakuingia ndani ya mashua, Denge amesimama anatazama wenzake (uk:273-274).

Haya yalikuwa mafanikio ya kumtorosha Denge gerezani.Suala hili lilikuwafaraja kubwa kwa Bukheti na kuwa fursa ya kuanzisha harakati za uchumba kwa Yasmin. Kwa kweli Denge hakuwa na mapenzi ya kweli kwa Yasmin, bali alikuwa na mapenzi ya kuendesha harakati zake tu, aliridhia suala la uchumbakwa Yasmin na Bukheti na kuibariki ndoa yao.

Tamati ya kitabu hiki ilimalizia kwa kuonesha kuwa Bwana Raza alioa mke Mombasa na mambo yake yakawa mazuri kwake. Anapata mtoto na kumwitaYasmin. Denge anaondoka Zanzibar na Yasmin anakwenda Tanga kuchukua vitu vyake vya urithi kutoka kwa marehemu Shihab. Bukheti anamshawishi mjomba wake aende kumposea Yasmin na posa yake inakubaliwa

baada ya mvutano nzito wa kuvunja ubaguzi wa Wahindi kwa Waswahili, ubaguzi usio na msingi wowote. Bukheti anahamia Zanzibar rasmi na kuwa ni mfanyabiashara ya madoriani.Yasmin na Denge wanabaki kukumbukana kupitia mtoto wao na salamu wanazotumiana kama inavyoelezwa:

> "Baada ya miezi mitatu Yasmin akapata kadi kutoka kwa Denge akampa hongera kwa kuolewa na kumtakia kila la kheri na mafanikio mema katika maisha". (uk:346).

## 4.6 Kubainisha Dhamira za Ukombozi katikaRiwaya ya Kusadikika

Kwa kurejelea mada ya utafiti isemayo: Kuchunguza Dhamira ya Ukombozi katika riwaya ya "*Kusadikika"* na "*Vuta N'kuvute"*: Utafiti Linganishi, mtafiti amezingatia kwa kina dhamira ya ukombozi na mgawanyiko wake katika maisha ya kila siku. Kwa msingi huo mtafiti amechambua migawanyiko/ aina mbalimbali za ukombozi kwa kurejelea riwaya teule akianzia na riwaya ya*"Kusadikika"* kama ifuatavyo:

### 4.6.1 Ukombozi waKifikra

Huu ni ukombozi unaohusiana na akili za mwanaadamu kuweza kufikiri juu ya jambo fulani hadi akaweza kulipambanua, kulieleza,kulitengeneza,kulifafanua au kulifuata kabisa bila ya hitilafu yoyote itakayowajia wakati mtu anapokabiliana na jambo hilo. Katika kutafuta maendeleo, kufikiri namna ya kutenda jambo ni bora kuliko kulivamia bila ya kuangalia hatima ya jambo hilo.Riwaya ya *Kusadikika* imeonesha ukombozi wa kifikra katika sehemu tofauti. Miongoni mwao ni kama zifuatao.

#### 4.6.1.1 Kufikiri mbinu za Kukomboa Nchi

Ni hali ya mtu kutafuta namna ya kuweza kuibadilisha nchi yake kutoka hali moja na nyengine. Hivyo mara nyingi, hujenga hisia za kujiamini na kujiepusha na hofu kwa kuweza kueleza ukweli uliofichikana na kuudhihirisha hata kama utawachukiza walengwa, au ni kuweza kujitetea ama kwa kauli au kimatendo bila ya kutetereka. Katika riwaya ya *Kusadikika,* mtafiti amegundua kuwa miongoni mwa mbinu za kutafuta ukombozi ni ushujaa, hekima na ufasaha vitu hivi vitatu ni viwakilishi vikubwa vya maendeleo ya jamii na upatikanaji wa ukombozi dhidi ya udhalilishwaji juu ya jamii husika. Jamii yoyote iwayo ikiwa inahitaji ukombozi, hivyo ndivyo vikomboleo vya ukombozi huo. Hata jamii ya Wasadikika ilikomboka kutokana na ushujaa wa wajumbe wao wakifuatiwa ni Karama ambaye alikuwa kama baba wa utafutaji ukombozi. Yeye ni muhusika aliyekuwa na ushujaa, hekima na ufasaha wakati alipojikita katika masuala ya uanasheria ambayo ilikuwa hata haijulikani kabisa kwa jamii ya wasadikika, hivyo ilikuwa kikwazo, shida na dhiki kubwa kuelimisha hadi ikafahamika kwa jamii hiyo iliyopofuka kabisa na kuwa nyuma kwa maendeleo yote ya jamii. Kwa ustadi mkubwa, Karama ambaye alikuwa kiumbe duni na dhalili kwa serikali wa Wasadikika, alitumia ushujaa wake aliokuwa nao ambao ndio uliomtengeneza na kumpa hadhi hadi kuvuta nyoyo za wasikilizaji wote waliokuwapo katika mahakama hiyo mbele ya kiongozi Majivuno aliyejaa taadi na inda dhidi ya Wasadikika wote. Msanii anasema:

> “Kwa wasifu wa nje, mshtakiwa alikuwa hana umbo la kufanya mvuto kwa watu, lakini kwa wasifu wa ndani alikuwa na ajabu tatu, kichwa chake kilikuwa na ubongo wa hekima, kifua kilikuwa na moyo wa ushujaa na kinywani ulimi wa ufasaha.Vitu hivi vitatu vilikuwa katika siri kubwasana. Hata baadhi ya wasiri wake hawakuweza kukisia kuwa alikuwa na hazina kama hii….Basi pale

> kizimbani alipokuwa amesimama wima aliinama kwa unyenyekevu mbele ya baraza, alipoinuka kwa sauti ya taratibu lakini imara,aliyavuta masikio ya baraza mzima kumsikiliza kama imamu aliyekuwa akihutubu juu ya mimbari ya msikiti mkubwa….Ushujaa ni hazina kubwa na bora ya kudumishwa.Ushujaa kwa mtu ni ngao,kwa nchi ni tegemeo na kwa taifa ni uwezo.(uk:17)

Kwa kuhusisha na nadharia teule ya Mwitiko wa Msomaji,inaonesha kwamba ni kweli kuna wasomaji ambao husoma na kufasiri kazi za fasihi kutokana na kuwa mawazo yake yanafaa na yana maana pana katika jamii iwapo watayasikiliza, kuyapima na kuyafuata katika matendo yao ya kila siku. Mtafiti kwa kumrelea msanii anakusudia kuielimisha jamii iachane na woga, hofu au shaka yoyote katika kupambana na maendeleo yake.

#### 4.6.1.2 Fikra ya Kuikomboa Nchi

Ni hali ya mtu kuwa na mawazo au mtazamo fulani juu ya kutaka mabadiliko ya nchi yake. Katika riwaya hii, Karama hakuwa nyuma kabisa katika kuibua fikra hii. Alijua vyema kuwa nayo ni nyezo kuu ya kujipatia ukombozi katika maisha ya mwanadamu, lakini popote panapokombolewa nchi ni lazima patatokea mvutano bina ya viongozi na raia. Hivyo, pakiwa katika hali hiyo, ni budi kwa wanamapinduzi kupambana nayo ili kupatikana mafanikio na akaweza kuhiili vikwazo na vitisho vitakavyotokana na adui zake kwani mara nyingi maadui hao huwa ndio wenye nguvu kuliko wanaotafuta ukombozi. Si hivyo tu, kuwepo na jambo hili kuna umuhimu mkubwa juu ya maslahi ya jamii na umma kwa ujumla.Pia, kutawafanya hata wale wanaojidai kuwa ama wana madaraka au nafasi fulani kusalimu amri na kukata tamaa na mwisho utesaji huondoka na kuwapa fursa na uhuru wale watafutaji wa uhuru au ukombozi na hapo hufikia kilele cha matarajio na mafanikio ya jamii.

> "Nchi za Mashariki kama zijulikanavyo ziko n'gambo ya matlai na bahari zilizo pana sana. Fadhili ilimpasa kuabiri na kujihaulisha katika vyombo mbalimbali. Kwa kufanya hivyo aliingia katika bandari kadhaa wa kadhaa.Safari yake ilichukua miaka mingi ya majaribu magumu,walakini alikuwa ni mvumilivu wa ajabu, uvumilivu wake ulikuwa hauna mwisho. Labda kwa kufadhiliwa kipawa hichi ndipo alipoitwa Fadhili". (uk:16)

Mtafiti akihusisha na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ameona kuwa kipengele hiki kina uwiano halisi kati ya maana inayosomwa na jinsi msomaji anavyohakiki kwa sababu kwa mujibu wa riwaya hii ya *Kusadikika* bila shaka imeonesha vya kutosha juu ya fikra ya kuikombo nchi na ndio ikapelekea muhusika huyu kutoka na kuacha familia yake kwa kutafuta namna ya ukuikomboa nchi yake. Hivyo, Fadhili hakujali vikwazo vya safari isipokuwa alizidi kustahamili na kusonga mbele na mwisho wa safari yake alipata faraja na matumaini makubwa ambayo kwa masikitiko yalipuuzwa na kutupiliwa mbali bila ya kujaliwa umuhimu wake. Vilevile, wajumbe wengine waliosalia nao walisibiwa ni janga hilo la upofu na iziwi wa serikali yao wakati walipoleta fikra yao hiyo na hapo ndipo palipotokea chanzo cha mateso waliyoyata.

#### 4.6.1.3 Fikra za Kutafuta Mawazo ya Wananchi

Ni hali ya mtu, watu au kikundi cha watu kuweza kufikiri namna ya kutoa mawazo, mchango au maelekezo juu ya jambo Fulani au kitu kinachowakwaza kwa lengo la kulitatua au kurekebisha kwa kushirikiana, kuungana na kusaidiana katika jambo au shughuli hiyo. Katika *Kusadikika*, Karama alijitolea kuielimisha jamii ya Wasadikika juu ya umuhimu wa kutafuta mawazo ya wananchi. Kiuwazi, alibainisha ushirikiano ulijitokeza kwa wajumbe sita ambao walijitolea kutafuta maendeleo ya nchi yao kabla ya kuibuka mawazo ya Karama juu ya elimu ya uanasheria,

hadikufikishwa kizimbani kwa kesi hiyo na kuwa mshtakiwa. Karama ambaye alikuwa kizuizini chini ya serikali ya waziri Majivuno kama walivyowekwa kifungoni wajumbe hao. Bila ya kujali vitimbi vya serikali yao walijitolea kwa khiari zao kutembelea nchi jirani na kuleta mawazo na maelekezo waliyoyapata katika marejeo yao. Hatimae waliteswa na kuadhibiwa kama ndio malipo ya michango yao kwa Wasadikika na serikali yao. Uthibitisho wa hayo, unaonekana kwa Buruhani aliyejitolea mwenyewe kuwa mjumbe wa Kaskazini.(uk:11). Wajumbe wengine ni Fadhili, mjumbe wa Mashariki.(uk:15),Kabuli,mjumbe wa Kusini.(uk:20), Auni, mjumbe wa Magharibi. (uk:25),Ridhaa, mjumbe wa Mbinguni. (uk:32) na Amini, mjumbe wa Ardhini.(uk:38)

Kwa kuhusisha na nadharia lengwa ya Mwitiko wa Msomaji ni kuwa mtafiti anathibitisha kuwa ni kweli kila kazi ya fasihi ina maana kufuatana na msomaji binafsi na jinsi anavyoichukulia kwa sababu alipoangalia kwa undani zaidi aliona kuwa, kitendo cha kukubali kwa wajumbe kwa hiari zao bila kulazimishwa ni ushirikiano wa kutosha usio na tone la shaka yoyote kwa sababu, lau kuwa hawana ushirikiano wasingaliweza kujitolea au wasingalikwenda na wasingekuwa tayari kuhatarisha maisha yao ila zaidi walijua kuwa penye maendeleo lazima panahitaji mawazo ya wananchi. Hivyo walikweda walikokwenda na kuleta michango yenye maana moja kubwa ambayo ilikuwa kunyanyua maendeleo ya Wasadikika tu. Nae Karama akapata mwanya wa kuyatetea mawazo hayo hadi yakaweza kutumika katika nchi yao na kupatikana maendeleo baada ya miaka michache.

#### 4.6.1.4 Fikra ya Kuanzisha Elimu ya Uanasheria

Fikra hii alijkuja nayo Karama katika nchi ya Kusadikika ili iwe ni elimu itakayofaa kwa Wasadikika wote, kimsingi alitaka kuinzisha iwe kikomboleo cha Wasadikika wote kwa sababu, mshtakiwa aliamini kwamba endapo jamii yake itaelewa na kujua athari ya maovu yaliyozama nchini mwao itajua mbinu za kukabiliana na maovu hayo hadi kufikia suluhisho linalotakikana. Hivyo alifikiria na kuona kuwa ni vyema kuianzisha kimatedo na hatimae akafikia kwenye kiriri ambako ndiko aliokusudia hasa kufikisha ujumbe wake huu. Mwandishi anasema:-

> “Ilipoonekana kuwa matendo ya mshtakiwa yalikuwa hayavumiliki na yenye hatari kubwa kabisa katika nchi niliamuru akamatwe na kuhukumiwa. Alipofika mbele yangu mara ya kwanza aliulizwa kama alikuwa mwalimu wa uanasheria. Alikubali upesi kama alieona ametunukiwa hadhi kubwa. Wa aidha alisema kuwa nafasi ya uanasheria katika nchi hii ilikua tupu. Kwa hivi alikusudia kuwa mwanasheria wa kwanza katika nchi ya Kusadikika”(Kusadikika uk:3).

Kwa kuhusisha nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ni kwamba nayo inakubalika kwani, elimu yoyote duniani ni vyema kuisoma na kuifanyia kazi katika njia zinazo stahiki.Hivyo muhusika Karama hakurudi nyuma kuielimisha elimu hii, hakuona aibu, haya, woga wala hofu yoyote mbele ya serikali ya Waziri Majivuno na baraza lake. Inasikitisha kuona kuwa, mara nyingi ndani ya serikali mawaziri ndio wanaokerwa zaidi ni jambo linalozuka katika jamii ambalo haliko katika mswaada au maamzi waliyotoa wao, kabla ya kufika kwa raisiau mfalme na wao huchukuwa nafasi ya kulipinga au kuhukumu hata kama wanahukumu kinyume na sharia. Hii ni kwa sababu, labda wana hofu ya kutawaliwa ni wengine au kupunguzwa hadhi na sifa zao za kuweza kutunga mambo na kuyangalia ipasavyo**.**

#### 4.6.1.5 Fikra za Wajumbe

Kila mjumbe alikuja na fikra yake ndani ya nchi hii ya Kusadikika kabla ya kuzuka kwa Karama ingawa fikra hizo ndizo zilizokuwa chanzo cha kuadhibiwa na kuteswa. Kwa mfano, mjumbe wa Kaskazini alikuja na fikar ya kuipamba nchi kwa kuijenga miji mikubwa na kunyanyua uchumi wanchi kwa kilimo, mifugo, kuondoa magonjwa na umasikini. (uk:12), mjumbe wa Mashariki alikuja na fikra ya elimu iliyoeleza utawala wenye ufasaha, kujenga mahusiano na nchi jirani na kuchukia vita na uonevu.(uk:16-17), mjumbe wa Kusini alikuja na fikra ya mamlaka, heshima, uhuru na nguvu yenye mipaka. (uk:23), mjumbe wa Magharibi alikuja na fikra juu ya athari ya wivu ubadhirifu wa nchi ya Kusadikika(uk:30), mjumbe wa Mbinguni alikuja na fikra ya kuihadharisha jamii ya Kusadikika iachane na wivu na kuitaka ifanyekazi kwa bidii (uk:36-37) na mjumbe wa Ardhini alikuja na fikra yake mara baada ya kurudi safari yake ya huko ardhini.Fikra za wajumbe wote waliotajwa zinawiana kimaana kwani zote zilikuwa zinalenga kwenye kuiboresha nchi ya Kusadikika kiuchumi na kimila.

Kwakuhusisha na nadharia teule ya Mwitiko wa Msomajini kuwa inaakisi kwa sababu, kwa kawaida ndani ya jamii hiyo na watu wenye mawazo mazuri na uwezo mkubwa wa kufikiria kitu kitakacholeta maendele ya nchi a taifa kwa ujumla. Lakini wanapotaka kufanya jambo au kuwaza juu ya jambo hilo huonekana wanazusha mambo ya ajabu na badala yake hupingwa na kuonywa waachane nalo au kuteswa kabisa bila ya kuangaliwa umuhimu wa hoja hiyo kwa jamii husika. Mwishojamii hiyo ikabaki katika majanga na dhiki isiyokwisha.

### 4.6.2 Ukombozi wa Kielimu

Ni ukombozi unaohusu ujuaji wa elimu,ufundi, ujuzi au fani yakazi fulani ambayo mwanadamu anaweza kukabiliana nayo.Jamii ikielimika bila ya shaka hutoka katika ujinga na kupelekea maendeleo kwa sababu“elimu ni ufunguo wa maisha”.Maisha ya mwanadamu mwenye elimu yanakuwa rahisi zaidi na yenye matumaini mema ukilinganisha na yale ya mjinga / asiye na elimuMwanadamu mwenye elimu ataweza kutumia akili yake ipasavyo katika kujikwamua na matatizo yote yatakayomkabili.Mshtakiwa Karama alikusudia kuielimisha kwa kina jamii yake juu ya umuhimu wa elimu ya uanasheria ili jamii hiyo iondokane najanga la upofu,uziwi na ujinga wa kutojua umuhimu wa elimu hiyo. Mwanadishi anabainisha:

> “Uanasheria ni elimu ya hukmu kwa mujibu wa sheria zilizokubalika.Hamna kitu chochote cha kuhofia kuwa kama pingamizi katika sheria.Elimu hii hasa husaidia sheria kuenda katika njia ya haki,haina budi kukumbukwa kuwa kugawanya haki kwa watu ni dhima itakayo hekma,hadhari na saburi yote iwezekanavyo kufanywa na mwanaadamu”(Kusadikika uk:9).

Kwa kurejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji, ni kuwa mtafiti ameona wazi kuwa inaakisi kulingana na jinsi alivyoifahamu. Kwani katika kuchunguza nukta hiyo, mtafiti amebaini kuwa Karamaanalenga kuwataka watu wa Kusadikika waijue elimu hii ili waepukane na dhulma, udhalilishwaji, unyanyaswaji na uovu wanaotendewa dhidi ya serikali ya Majivuno na kaumu yake.

#### 4.6.2.1 Umuhimu wa Elimu

Katika riwaya teule, elimu imesaidia ipasavyo katika kuleta mabadiliko auukombozi wa jamii ya Wasadikika. Tukiacha mbali Karama, katika uteuzi wa mashahidi wa mtunzi ni ameteua wale wenye elimu hii ni kutokana na kuwa hawa ndio ambao

watajuwa hasa kuyaelezea vizuri watakayoyaona na hata watu walioelimika huwa ni wenye kuheshimika zaidi ukilinganisha na wale ambao wako nyuma kielimu.Mfalme alipowaangalia mashahidi aliona hakuna haja yoyote ya kuwatia hatiani walisema ukweli kwa sababu wote ni wasomi kama anavyoeleza mwandishi.

> "Maombezi ya mshtakiwa yaliyochukua karibu muda wa juma moja. Sasa tunahiari mbili za kuchagua, yaani kuihairisha kesi hii mpaka ushahidi mwengine upatikane au kuikata kwa ushahidi uliopatikana. Katika njia hizi mbili mimi nataka sana njia ya pili. Sababu zangu za kufanya hivyo ni kuwa ushahidi tulio nao umetoka kwa mashahidi walio mahiri au stadi sana katika sheria za nchi hii . Wa kwanza amehitimu ubalozi, na wa pili ni mufti katika ukadhi. Wote wawili ni watu mashuhuri sana. Mashahidi hawa hawakuoyesha dalili yoyote kuwa ushahidi mwengine ulilazimu. Kwa hivi naona kama kwamba hawakuwa na neno lingine la kuongeza. Kama hili likiwaafiki kazi yetu itupasayo itatimizwa. Mwasemaje waungwana?" (Uk.47)

Mtafiti akihusisha nukta hii na nadharia ya mwitiko wa msomaji amethibitishakuwa ni kweli kwamba kila msomaji husoma na kufasiri kazi za fasihi vizuri kuliko wasomaji wengine,kila muhakiki huwa mawazo yake yenye kulingana na fikra,akili na ubunifu alijaaliwa kuwa nao juu ya kipimo hicho ndipo unapoona kuwa hata kama watu wote wna kazi moja,wana elimu kiwango kimoja ila miongoni mwao wengine huwa na umuhimu zaidi ukilinganisha na wengine.Pamoja na hayo elimu ndio inayomtoa mtu katika kiza cha ujinga na kumpeleka katika mwangaza. Mwenye kuelimika huwa tofauti na mjinga, huheshimika, hutukuka na mawazo yake huthaminiwa zaidi ukilinganisha na jahili yaani mjinga kwa sababu yeye huwa duni,dhalili na mara nyingi hudharauliwa kwa namna moja au nyengine. Si hivyo tu pahala popote pale, elimu ndio ufunguo wa maisha na pasipo na elimu ujinga hutawala na kupelekea kutwendwa mambo yasiyofaa.

Elimu nyengie zilizodhihirishwa katika riwaya hii ni elimu ya uanasheria kama ishavyoelezwa , elimu ya kuishi na watu, kuondosha ubaguzi, kuwaeliisha wanawake na watoto, elimu ya kunenga urafiki na wengine na elimu ya kujimboa kutokana na madhila. Zote zimeshapambanuliwa katka nukta zilizopita.

#### 4.6.2.2 Elimu bora

Katika riwaya teule, elimu imesaidia ipasavyo katika kuleta mabadiliko ya ukombozi wa jamii ya Wasadikika. Mifano yote aliyotoa Karama, katika uteuzi wa wajumbe mtunzi ameteua wale wenye elimu iliyo na ubora na kiwango cha hali ya juu kabisa. Hii ni kutokana na kuwa hawa ndio ambao watajuwa hasa kuyaelezea vizuri watakayoyaona, hata watu walioelimika huwa ni wenye kuheshimika zaidi ukilinganisha na wale ambao wako nyuma kielimu.Mfalme alipowaangalia aliwaona hakuna haja yoyote ya kuwatia hatiani walisema ukweli kwa sababu wote ni wasomi kama anavyoeleza mwandishi.

> "Maombezi ya mshtakiwa yaliyochukua karibu muda wa juma moja. Sasa tunahiari mbili za kuchagua, yaani kuihairisha kesi hii mpaka ushahidi mwengine upatikane au kuikata kwa ushahidi uliopatikana. Katika njia hizi mbili mimi nataka sana njia ya pili. Sababu zangu za kufanya hivyo ni kuwa ushahidi tulio nao umetoka kwa mashahidi walio mahiri au stadi sana katika sheria za nchi hii . Wa kwanza amehitimu ubalozi, na wa pili ni mufti katika ukadhi. Wote wawili ni watu mashuhuri sana. Mashahidi hawa hawakuonyesha dalili yoyote kuwa ushahidi mwengine ulilazimu. Kwa hivi, naona kama kwamba hawakuwa na neno lingine la kuongeza. Kama hili likiwaafiki kazi yetu itupasayo itatimizwa. Mwasemaje waungwana?" (Uk.47)

Mtafiti akihusisha nukta hii na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji amethibitishakuwa ni kweli kwamba kila msomaji husoma na kufasiri kazi za fasihi vizuri kuliko wasomaji wengine, kila muhakiki huwa mawazo yake yenye kulingana na fikra, akili na ubunifu aliojaaliwa kuwa nao, juu ya kipimo hicho ndipo unapoona kuwa hata kama watu wote wako kazi moja,wana elimu kiwango kimoja ila miongoni mwao wengine huwa na umuhimu zaidi ukilinganisha na wengine. Pamoja na hayo, elimu ndio inayomtoa mtu katika kiza cha ujinga na kumpeleka katika mwangaza. Mwenye kuelimika huwa tofauti na mjinga, huheshimika, hutukuka na mawazo yake huthaminiwa zaidi ukilinganisha na jahili yaani mjinga kwan sababu yeye huwa duni, dhalili na mara nyingi hudharauliwa kwa namna moja au nyengine. Si hivyo tu; pahala popote, elimu ndio ufunguo wa maisha. Pasipo elimu ujinga hutawala na kupelekea kutendwa mambo yasiyofaa.

### 4.6.3 Ukombozi wa Kiuchumi

Ni ukombozi unaohusiana zaidi na masuala ya uchumi juu ya mahitaji ya jamii.Taifa au jamii yoyote inapaswa kutafuta mbinu za kujitafutia mahitaji yake ya lazima kwa lengo la kuishi katika maisha yaliyobora na yenye kuridhisha. Kukosekana kwa uchumi mzuri katika nchi kutapelekea uzoroteshaji wa maendeleo ya jamii husika. Mwandishi ameonesha uchumi katika maeneyo yafuatayo:-

#### 4.6.3.1 Kilimo bora

Mtunzi wa riwaya hii hakurudi nyuma katika kueleza umuhimu wa kilimo kwa jamii ya Wasadikika. Ametumia muhusika Karama kwa kufanya makarama yake ya kuonesha kilimo bora katika marejeleo ya Buruhani kwa kusema:

> "Marejeo ya Buruhani yaliyazibua masikio ya Wasadikika. Ilikua ni mara ya kwanza katika maisha ya Wasadikika kusikia kuwa nchi za kaskazini watu wamestawi zaidi kuliko …Ukulima,mbolea na hifadhi ya udongo...Kilimo ni uti wa mgongo wa maisha ya mwanadamu, bila kilimo maisha hayawezi kudumu, nchi hii yaonekana kama imesahau wajibu wa kazi hii, udongo usipohifahiwa hupotelewa na rutuba yake kila mwaka na mara kwa mara njaa kali hutokea."(uk:12-13)

Kwa kuhusisha nadharia lengwa ni kwamba inakubaliana uhusiano wake na baina ya mtunzi na mawazo ya mhakiki, kama alivyosema mwandishi kuwa kilimo ni uti wa mgongo ni vyema kujishuhgulisha nacho kwa hali na mali. Pia ili kuboresha kilimo, wakulima wanatakiwa kutumia nyenzo za kisasa kama magari ya kulimia na mbolea ili kuzalisha mazao mengi na mazuri yatakayowapatia chakula na kunyanyua uchumi wa nchi kwa kuuza mazao na kupata pesa za kuwasaidia katika matumizi yao ya kila siku. Karama ameikomboa jamii juu ya suala hilo. Ameinyanyua Kusadikika kwa kuielimisha kuhusu kilimo na jinsi ya kutumia njia nzuri ya kuboresha kilimo hicho.

#### 4.6.3.2 Kuboresha Ufugaji

Katika riwaya lengwa, mwandishi ameeleza umuhimu wa mifugo na namna ya kufuga mifugo hiyo katika njia ya kisasa. Amesema kuwa:

> "Na kuwa mfugaji mwema hasiti kushirikiana nyumba moja na wanyama wake. Fikra za washauri hawa zilikuwa hazifanani na kitu chochote chema katika dunia ujinga wao haukuyazuia maendeleo tu lakini hasa ulirudisha nchi nyuma vile vile."(uk:13)

Kwa kuhusisha nadharia tajwa ya Mwitiko ya Msomaji ni kwamba inaenda sambamba na uhalisia wa jamii, kwani mifugo ni kikomboleo cha maisha ya binaadamu kwa sababu ndani ya mifugo tunapata vyakula vyenye rutuba na siha njema katika miili yetu pia ni mali ghafi kwa matumizi ya mwanadamu. Kwa mfano,

ng’ombe hutoa maziwa na nyama ambayo ni chakula bora kwa mwanadamu na ngozi yake hutengenewa nguo, viatu,ngoma na zana nyenginezo. Kuku hutoa mayai na nyama pia hutoa manyoa ambayo hutumika kutengenezea kofia, mito n.k. Si hivyo tu,wanyama kama punda na farasi hutumika kama vipando vya wanadamu na mizigo yao, pia manyoya yao hutengenezea nguo. Hivyo, Karama ameonesha mchango mkubwa juu ya suala hili kwa raia wa Kusadikika kwani ufugaji ni katika nyezo kuu za mandeleo ya jamii.

#### 4.6.3.3 Kufanya kazi kwa bidii

Bidii hupatikana wakati ambapo mtu atajitahidi kufanya kazi bila kutia uzito wowote utakaomfanya kurudi nyuma au kukata tamaa na kuliwacha kabisa. Katika riwaya hii, bidii nayo inasaidia kiasi kikubwa katika kufanikisha maendeleo na kupata ukombozi katika jamii. Jamii ya Kusadikika ni mfano mzuri na kigezo katika kuidadavua nukta hiyo adhimu, kwani, Karama alifanya kazi kwa bidii alizojaaliwa juu ya kutoa ushahidi dhidi ya kesi yake iliyokuwa katika baraza ya waziri Majivuno. Kwa kuthibitisha hayo alimtumia Buruhani kama ni kiigizo cha watu wenye bidii katika kazi zao na kuonesha kuwa kila anapohitaji maedeleo ni vyema pawe na bidii kinyume chake itakuwa ni udhorotaji wa mabadilio ya jamii hiyo. Hivyo, Buruhani alisafiri kwa matumaini makubwa ya kurudi salama, alitumia bidii zote za kuvuka mito, misitu, nyika na vibuko vyengine na alipopata shida ndipo alipozidisha bidii ya kuendelea mbele kwa lengo la kukamilisha matarajio yake.Mtunzi anasema:-

> “Kila alipokutana na shida ndipo bidii yake ilipozidi kukua.Baadhi ya watu hulegea mioyo mbele ya dhiki,lakini wengine hukazana mpaka wameishinda.Bidii ya Buruhani ilifanya mwangaza kama wa

> taa mbele yake,akazidi kupanua hatua kufululiza katika kazi aliyotumwa kwa uthabiti na furaha kubwa."(*Kusadikika uk11*)

Katika kukusisha na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ni kwamba nukta hii msomaji ametumia kigezo cha kuhakiki maelezo yaliyopo juu na yaliyomjuilisha kuwa mawazo yake yanafaa katika maendeleo ya jamii, bidii ndio chachu ya mendeleo, pasipokuwa na bidii hapana kazi yoyote, uduni wa mambo hutawala na kusababisha uzoreteshaji wa maendeleo katika jamii husika.

**4.6.3.4 Kuondosha uvivu**

Ni hali ya mtu kuwa na jitihada ya hali ya juu katika kufanya jambo. Katika riwaya hii ya *Kusadikika* mebaini juhudi kubwa aliyoielezea Karama juu ushahidi wa mashtaka yake. Zaidi hasa aliwaelezea wajumbe na namna walivyoelekea pande mbali mbali za dunia iliyoizunguka Kusadikika. Hii ni kwa sababu walitaka zaidi kujua ni namna gani wanaadamu walio wengi katika ulimwengu wamefanikiwa kimarika kulingana na maendeleo na mahitaji ya nchi zao,kwa kadiri walivyotoka ndivyo walivyoyakuta mengi na mazuri yasiyolingana au hata kukaribiana na nchi yao ya Kusadikika. Hivyo, juhudi zao ndizo zilizowapa faraja na kujua hali za walimwengu wengine duniani kote kwa sababu kila walipotembea ndipo waliposoma maisha ya wengine.

Mtafiti amehusisha na nadharia ya Upokezi na amedhihirisha ya kwamba,hakika kuna uwiano wa kina kabisa kati ya maana inayosomwa na jinsi msomaji anavyohakiki kwani kulinganana uchambuzi wake ameona wazi kuwa juhudi ni kiungio adhimu cha mapambano pamoja na kupata maendeleo juu ya mahitaji ya jamii au mtu mmoja mmoja.Mfano hata katika kusoma mwanafunzi kila anapokuwa

na juhudi za kusoma na kutafuta mambo juu ya masomo yake ndipo anapopata mafanikio na kufaulu vyema kuliko asiyejali na kudhau masomo yake. Kutokana na hayo ni vyema kwa mwanaadamu yeyote mwenye akili timamu kuwa na juhudi na jitihada katika kufanya jambo jema kwa sababu siku zote mwenye kujitahidi hufaulu.

#### 4.6.3.5 Kuondosha umaskini

Umaskini na hali ya mtu au jamii ya watu kushindwa kujitatulia mahitaji yao. Mahitaji hayo yanaweza yakawa kama ukosefu wa elimu, upungufu wa uchumi na mengineyo. Ili kuokoa hali hiyo, Karama aliitalka jamii ya Wasadikika wajihusishe zaidi na masuala ya uchumi kulongana na mahitaji ya jamii yao la si kwa mahitaji ya watu wachache kama ilivyooneshwa katika riwaya hiyo. Karama alibainisha ya kwamba, taifa lolote liwalo au jamii nyngine yoyote, inapaswa kutafuta mbinu za kujitafutia mahitaji yake ya lazima kwa lengo la kuishi katika maisha yaliyobora na yenye kuridhisha. Kukosekana kwa uchumi mzuri katika nchi kutapelekea uzoroteshaji wa maendeleo ya jamii husika, pia umaskini utatawala ndani ya jamii hiyo. Katika riwaya teule sehemu nyingi zinaonesha suala la uchumi. Mfano, Buruhani anatoa rai yake katika taifa lake kama anavyoeleza mwandishi.

> “Rai ya Burhani ilikuwa kukutanisha bidii za taifa la Kusadikika katika shabaha moja. Alitaka maendeleo ya nchi yachangiwe na kila mtu kwa ushirika wa kazi, fikra na mali.Ushirika huu ulikusudia kuendelea mpaka Kusadikika isitawi kama nchi nyengine zilivyositawi na zitakavyokua baadaye…. “Kilimo ni uti wa mgongo wa maisha ya mwanaadamu. Bila ya kilimo maisha hayawezi kudumu. Nchi hii yaonekana kama imesahau umuhimu wa kazi hii, udongo usipohifadhiwa, hupotelewa na rutuba yake kila mwaka na mara kwa mara njaa hutokea. Njaa hiyo hufanyiza madhara makubwa katika maisha ya watu wanaoishi juu ya udongo uliochujuka(uk:15).

Kwa kuhusisha na nadharia ya Mwitiko wa Msomajikatika mihimili yake inaonekana kuwa kuna uwiano mkuwa kati ya maana na jinsi mhakiki alivyoihakiki kazi yake kwani, maendeleo ya nchi hayapatikani bila ya ushirika wa wanajamii husika, hapana ubaguzi katka kujenga nchi, watu wote lazima wawe kitu kimoja na wajumuike pamoja kwa kuamua na kutekeleza majukumu yao. Ni vyema wapangiane majukumu ya utendaji yatakayowapelekea ufanisi wa kazi. Kila mshiriki atapangiwa kazi kulingana na kipaji chake alichojaaliwa. Mfano, mwenye uwezo wa kusomesha vijana atapewa jukumu la kusomesha, mwenye uwezo wa kulima atapangiwa jukumu la kushughulikia mas-ala ya kilimo na mwenye sifa ya kutibu atapewa jukumu hilo ili mradi mambo yende sawa na yenye kuridhisha.

### 4.6.4 Ukombozi wa Kisiasa

Ni ukombozi unaojumuisha namna ya uwendeshaji siasa bora, kuwa na uzalendo, kuwa na subra pamoja na ushirikiano, ujasiri, upendo n.k.

#### 4.6.4.1 Namna ya kuendesha siasa bora

Ni hali inayuhuiana na ukombozi unaohusu mtu au jamii kuweza kujikomboa juu ya siasa ya nchi yao kwa lengo la kurekebisha utawala uliopo au kuubadilisha na kuweka utawala mwengine yaani utawala mpya. Kwa kawaida kila nchi inakuwa na sera yake ya siasa na kila mtawala au kila siasa vilevile huwa na sera yake. Mfano, Mwalim Juliasi Kambarage Nyerere alikuwa na sera ya “Ujamaa” na Raisi Magufuli aa sera ya “Hapa kazi tu.” Wakati mwengine huwezekana kabisa sera ya mtawala aliyepo kuwa haitakikani au haifai na huhitajika kuondoshwa na kuwekwa sera nyengine au kurekebishwa ili iwe nzuri itakayotumika vyema kwa mujibu wa mahitaji ya jamii husika. Karama pia hakuwanyuma juu ya kuielimsha jamii yake juu

ya siasa iliyobora yenye kufuata miiko na taratibu ya nchi yake kwa kupitia mawazo na mitizamo ya jamii husika. Kwa kurejelea **r**iwaya ya *Kusadikika* ukombozi wa aina hii ulijitokeza zaidi katika ukurasa wa 16, 17, 18, 34 na 35.

Katika ukurasa wa 16 hadi 18 anaonekana Fadhili ambaye alikuwa mjumbe wa Mashariki na kuitembelea nchi hiyo, pamoja na vikwazo vilivyomkabili ila alifanikisha kupata mengi aliyokusudia ambayo aliamini kwamba lau yangalifuatwa katika nchi ya Kusadikika, matunda ya maendeleo yangalikuwepo na kupelekea faraja kwa umma wa nchi ya Wasadikika. Badala yake alipotowa taarifa juu ya ustawi wa mashariki, rai yake ilipokewa kwa kuzomewa na kuitwa mwongo, mwoga na mwotaji wa ndoto zisizotabirika. Siasa iliyojitokeza ni kama ambavyo mwandishi anavyoeleza:-

> "Karibu watu wote huko walichukia uchokozi kama aibu kubwa,na waliviapiza vita kama laana ipitayo kiasi kwamba viumbe waliojaaliwa busara ya haki, moyo wa wema, ulimi wa nasaha, masikio ya kusikilizana, macho ya uongozi, pua ya kutambua harufu, ushirika wa amani, ajali moja na mungu mmoja, hapana kabisa kitu hata kimoja katika hivi alichopewa mtu kwa ajili ya uharabu. Siasa kubwa huko ilikuwa ni kuwaunganisha watu wote katika urafiki, juu ya urafiki huo amani ya ulimwengu imekusudiwa kujengwa"(uk:16).

Kwa kuhuisha nadharia yetu katika kipengele cha uhusiano kati ya mtunzi na namna mhakiki alivyoihakik kazi yake ni kuwa inkualiana vyema kwa sababu katika nchi au jamii yoyote ile ya kileo, siasa ni jambo la msingi katika kuleta maendeleo endapo itafanywa kwa kuzingatia masharti yake na mipaka ya nchi inayokubalika itakayopelekea kuwa sisa bora. Ili kupatikana maendeleo kuishi kwa udugu na kuwa kitu kimoja, kuchukia vita, uadui, uchokozi ni nyenzo kuu ya mafanikio. Mahali

penye mapambano ya vita siku zote hukosa maendeleo mazuri ya maisha ya wanajamii husika.

#### 4.6.4.2 Ulafi wa madaraka

Katikariwaya ya "*Kusadikika*" suala hili limejitokeza mara kadhaa, viongozi wamejikwazia madaraka kwa kurithishana. Mfano, Majivuno ameshika uwaziri tokea enzi za babu yake, kisha baba yake hadi kufikia mfalme aliyepo sasa. Pamoja na uzee wake na kuishi mno ndani ya serikali miaka mingi, hadi sasa anaonekana aking'ang'ania na kukumbatia madaraka. Mtunzi anadhihirisha hayo katika maelezo yafuatayo:-

> "Nataka ifahamike wazi wazi kuwa mimi nina hofu kubwa sana juu ya mshtakiwa. Sababu za hofu yangu ni kuwa kama akiamriwa kuwa atakavyoleo, kesho atadai udiwani, kesho kutwa uwaziri na baadaye ufalme. Kwa desturi tamaa za watu kama yeye alivyo zitaamka. Tamaa hizo zikiamka hazitakuwa na mpaka. Watu kama hao lazima wafunzwe kuzijua hali zao vile vile."(uk:3)

Kwa kuhusisha na nadharia teule ni wazi kuwa inaakisi. Kwani, nchi nyingi duniani kote zimemezwa na janga hili potofu, mara nyigi viongozi hutokea koo ambazo zimo ndani ya serikali. Kwa mfano, ikiwa baba ni raisi mtoto atakuwa waziri mkuu au mbunge au ikiwa baba ni kiongozi wa nchi, mtoto naye lazima atakalia kiti kile kile hata kama wanavyoongoza sivyo. Hali inayopelekea kukomaa kwa desturi na mila zisizofaa katika jamii zao. Karama ameeleza wazi kuwa kiongozi namtu yoyote mwenye uwezo na sifa stahiki za kuongoza raia wake kwa kufuta misingi iliyobara na imara na sikwa kuangalia ukubwa wa mtu au cheo.

#### 4.6.4.3 Kuondosha uhasama

Mwandishi mashuhuri Shaban Robert alifanikisha kiasi kikubwa kumchora Karama kama ni mtetezi wa tatizo hili. Haya yamethibitishwa kupitia safari ya mjumbe wa Mashariki ambaye alikua ni Fadhili. Mwandishi anasema:

> "Imekwisha thibitishwa huko kuwa kama kwa vita mshindwa hupata hasara; na mshindi kadhalika huundamwa na kisasi cha milele. Hapana mtu yoyote mwema apendaye hasara ya kushindwa wala kisasi cha ushindi katika maisha yake."(uk:17)

Kwa kuhusisha nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ni kwamba ina uhusianao mkubwa kati ya mtunzi na namna msomaji alivyoihkiki kazi yake kwa sababu uhasama na mzozoz ni uadui katika jamii, palipo uhasama uadui hukithiri na upendo huondoka, kila mtu humuona mwenzake kama chui kwa ukali. Zaidi ya hayo, amani katika nyoyo huondoka kabisa, udugu hukatika na urafiki hukimbia kabisa. Mwenye kufikwa na dhiki hushinwa ni wakumtatulia shida yake jambo ambalo huzidisha husda huondosha huruma kwa jamii.

#### 4.6.4.4 Fursa ya kujitetea

Kwa kawaida, palipo tawaliwa ni siasa mamlaka huwa ya wachache,wenye mamlaka ndio wanaojipa hadhi ya kusema wanalotaka hata kama halifai kwa kutoleta faida yoyote. Pia raia huwwza wakateswa ovyo ovyo bila kujaliwa haki zao kiasi abambacho hata kama mtu atakwazwa na jambo hawezikukisema katika hadhara na badala yake hubaki katika mawazo yasiyo utatuzi wowote. Kwa bahati njema Karama alifanikiwa kujitetea kwa moyowa ushindi hadi akapata mafanikio ya malengo yake kwa wananchi wa Kusadikika**.**

> Hii ilikuwa siku ya kwanza ya muda ulioamriwa. Baraza ilihudhuriwa na Mfalme, waziri pamoja na wasimamizi wengine wa serikali. Sudusi moja ya watu wa Sadiki, mji mkuu wa Kusadikika, walikuwapo vile vile. Mbele ya baraza hii Karama, Mshtakiwa alisimam kujitetea bila ya kutetemeka. Alisema kwa makini kama mtu aliyezoea kusema hadharani". (uk:9)

Kwa kuhusisha nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ni kwamba inaakisi kwani palipo na siasa bora ni pale papatikanapo uhuru wa kuzungumza pamoja na kutoa maamuzi au kujitetea kwa mkosa hadi kufikia suluhisho kwani hapo atakuwa amepata uhuru wake kwa kiasikinahotakikana.

**4.6.4.5 Kuwatowa wafungwa**

Karama kama watetezi wengine alifanikisha kuwatoa wafungwa waliokuwa gerezani kwa miaka mingi kwa sababu ya kutetea nchi yao. Wafungwa hao ni Buruhani na wajumbe wengine. Kwa hoja za Karama walitolewa gerezani na kuamuriwa walipwe fidia kipindi chote walichokuwamo humo.Mtunzi amsema:

> Mfalme alinena. "Taibu, hiyo ni hukumu njema, naafikiana na nyinyi kabisa. Hapana hukmu nyengine iliyowezekana juu ya ushahidi uliokuwa mbele yetu. Zaidi ya hayo, natoa amri kuwa watu sita waliotajwa katika kesi hii-Buruhani, Fadhili, Kabuli, Auni, Ridhaa na Auni-wafunguliwe mara moja."(uk:48)

Kwa kuhusisha nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ni wazi kuwa ina uhusiano nyeti kulingana na mawazo ya mwandishi na namna mhakiki alivyoihakiki kazi yake kwa sababu aghlabu katika jamii pakiwa na watu wanaotoa mwamko juu ya jambo fulani lisilojulikana huonewa kwa kuteswa na kudhalilishwa hadi kutiwa gerezani bila ya sababu yoyote, hii hutokea kwa sababu wakuu wa nchi hiyo huwa hawako tayari kuelimshwa, jambo kubwa wanalowafanyia ni kuwatesa na kuwadhulumu bila ya kujali kuwa wanazidisha uovu na chuki dhidi ya jamii yao. Pamoja na hayo,

wafungwa hao hunyimwa haki zao za msingi kama kula, kunya na pia hufanyiwa vitendo vya kikatili na vya kinyama.Hii inapelekea kuwatia huzuni na simanzi wao na familia zao kuishi maisha yasiyoridhia kutokana na kukosa awezo wa kujikimu.

#### 4.6.4.6 Kujenga hoja za wajumbe

Katika riwaya ya "*Kusadikika*" mtunzi maemtumia Karama kama kikomboleo cha kujenga hoja za wajumbe, anaonekana akiwajengea hoja mbele ya mahakama kutokana na haki walizonyimwa ni serikali yao. Mwandishi amelionesha hili katika sehemu ifuatayo:-

> "Wa aidha, hata kama matokeo ya mjumbe wa Mashariki yalibuniwa kama walivyodai washauri wa serikali, lakini yalikuwa si mabaya kamwe.Yalibuniwa kwa njia inayowezekana kutendwa na watu kwa faida ya maisha yao na Kasadikika nzima. Izara na kifungo ilikuwa si tunzo njema kwa Fadhili. Uko wapi uso asiotahayari kwa aibu kama hii?"(uk:18)

Kwa kuhusisha nadharia ya Mwitiko wa Msomaji, kweli inaendana vyema kati ya mawazo ya mtuzi na namna mhakiki anavyoikiki kazi yake. Kwani, mara nyingi katika jamii wamo watu wanaozijenga hoja za wajumbe wao kwa kuwatetea au kuonesha dhima mbali mbali ya kijamii. Karama alijenga hoja tafauti hoja tafauti juu ya mas-ala mbali mbali waliyokuja nayo wajumbe hao.Mfano, kuhusu uchumi wa nchi, mara baada ya kupingwa mjumbe wake na kuonekana kama mwendawazimu Karama hakukaa kinya bali alionesha umuhimu wa umuhim wa uchumi kuptia nyenzo za kilimo, mifugo, barabara, maji safi na vyombo vya usafiri.Si hivyo tu, alijenga hoja nyingi kulingana na matokeo ya wajumbe hao.

### 4.6.4.7 Utetezi wa haki za binaadamu

Utetezi wa haki za binaadamu nayo ni kiwakilishi cha kupatikana ukombozi katika jamii.Kupitia Riwaya ya *Kusadikika* Karama ameonesha namna maendeleo yalivyopatikana kutokana na haki aliyoifanya mfalme wa Kusadikika, kwa sababu aliruhusu wajumbe wafunguliwe gerezani na walipwe haki zao kwa mujibu wa siku zote walizowekwa katika gereza na Karama pia hana kesi isipokuwa alifanya mema ambayo lau maneno yake yangalifuatwa tangu mwanzo,maendeleo ya wananchi yangalipatikana kwa haraka sana.Mwandishi anasema:

> "Mbele ya umati huu Karama alitamka. "Baada ya kutenda yote waliyoweza kwa ajili ya nchi yao, Buruhani aliponzeka, Kabuli alihusudika, na Fadhili akateswa mateso makubwa zawadi walizotunikiwa na nchi waliyoipenda zilikuwa ghira na adhabu tupu. Ingawa watu hawa wangali hai hata sasa, lakini wake zao wamekwishaonja eda chungu na watoto wao wameachwa na uyatima wa kusikitisha. Dhiki za nchi na misiba ya watu hawa ikiwekwa pamoja hutosha kuifanya jumla ya mashaka ya Kusadikika kuwa kama nusu moja ya mashaka ya dunia nzima." (uk:25)

Mwisho wa siku Mfalme aliyakubali maombi ya Karama na kuruhusu wafungwa hao waachwe huru na walipwe fidia. Mwandishi anasema:

> Mfalme alinena. "Taibu, hiyo ni hukumu njema. Naafikiana na nyinyi kabisa. Hapana hukumu nyengine iliyowezekana juu ya ushahidi uliokuwa mbele yetu. Zaidi ya hayo, natoa amri kuwa watu sita waliotajwa katika kesi hii - Burhani, Fadhili, Kabuli, Auni, Ridhaa na Amini - wafunguliwe mara moja. Inasikitisha sana kuwa dhuluma juu ya watu hawa hazikutengenezwa mpaka leo. Gereza ni makao ya wahalifu. Watu hawa si wahalifu ila wafadhili bora. Wanastahiki uhuru na heshima kubwa. Hasara zao lazima zifidiwe.Kusadikika inamshukuru sana Karama kwa kuitanabahisha wajibu wake".(uk:48)

Kupitia nadharia ya Upokezi ni kuwa kuna uwiano wa wazi kati ya maana inayosomwa na jinsi msomaji anavyohakiki kwa sababu kitendo cha kutiwa gerezani wajumbe na kutiwa hatiani kwa kuteswa na kudhalilishwa bila makosa ni ishara tosha ya ukosefu wa haki za binaadamu na ndio maana mfalme wa Kusadikika akalaani tukio hilo na kuamuru watu waachiliwe huru na walipwe fidia ili iwe kama kikomboleo juu ya madhila na mateso waliyoyapata wakati wakiwa ndani ya gereza.

#### 4.6.4.8 Kupunguza vifo

Pia mtunzi amemtumia Karama kama kiwakilishi cha watu wanaoielimisha jamii yao juu ya athari ya vifo na kuitaka jamii kuachana na tatizo hilo. Katika riwaya tajwa, msanii ameonesha nukta hii katika maeneo tafauti. Katika ukurasa wa kumi na sita amesema haya yafuatayo:-

> “Kwa muhutasari alisema kuwa katika nchi ya Mashariki kengele ya mauti ya uchokozi na vita kati ya wanaadamu, nchi kwa nchi, au taifa kwa taifa imeanza kulia amani sana. Bidii kubwa zilikuwa zikifanyizwa za kuyazika mambo hayo mawili katika kaburi lasahau.”(uk:16)

Kwa mujibu wa nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ni kwamba inauhusiano mkubwa kati ya mtunzi na namna mhakiki anavyoihakiki kazi yake, kwani mtafiti anaona kuwa ipo haja ya kusitisha vifo vya papo kwa papo. Jamii nyingi duniani hukumbwa na tatizo hili, vifo hukihiri hadi ikawa tishio kubwa kwa uma, hivyo ni vyema kutafuta suluhisho la kupunguza hatari hiyo kwa kujenga udugu, upendo na mahusiano mema badala ya kupambana kwa kugombana na kuuwana. Karama kama wananchi wengine licha ya udhaifu wake, hakurudi nyuma katika kutetea hili ndani

ya jamii yake ya Kusadikika na mwisho wasadikika walielewa na kutafuta suluhisho sahihi la janga hilo.

### 4.6.4.9 Subra

Subra ni hali ya mtu au kikundi cha watu kuweza kusubiria juu ya shida,taabu au mateso yoyote yanayomkabili kwa kutarajia mafanikio mazuri ya baadaye.Katika *Kusadikika*, wajumbe sita walisubiria vyema juu ya shida waliyokuwa nayo gerezani na kutumaini mafanikio ambayo waliyapata na jamii yao kwa ujumla.Kwa kuthibitisha hili,mtunzi ameonesha haya wakati ambapo mwisho wa mashtaka anaonekana mfalme juu ya taabu waliyoipata na hukmu yake iliyokuwa faraja kubwa kwa jamii Wasadikika wote. Mwandishi anaweka wazi:

> "Mfalme alinena. "Taibu hiyo ni hukmu njema.Naafikiana na nyinyi kabisa.Hapana hukumu nyengine iliyowezekana juu ya ushahidi uliokuwa mbele yetu. Zaidi ya hayo natoa amri kuwa watu sita waliotajwa katika kesi hii: Buruhani, Fadhili, Kabuli, Auni, Ridhaa na Amini wafunguliwe mara moja. Inasikitisha sana kuwa dhulma juu ya watu hawa hazikutengezwa mpaka leo. Gereza ni makao ya wahalifu, watu hawa si wahalifu ila wafadhili bora.Wanastahili uhuru na heshima kubwa. Na hasara zao lazima zifidiwe.Kusadikika inamshukuru sana Karama kwa kutanabahisha wajibu wake" Mwisho wa maneno ya Mfalme alivunja baraza. Watu walisimama wakaenda zao. Baada ya miaka michache kupita mazungumo yote yaliyoletwa Kusadikika na wajumbe wake yaliamsha bidii zilizokuwa zimelala. Mavuno ya mafunzo hayo yaliifanya Kusadikika kuwa nchi moja katika nchi zilizostawi kabisa".(uk:48-49)

Kwa kurejeleana nadharia teule ya Mwitiko wa Msomaji ni kwamba, msomaji ametumia kigezo cha kutafsiri maelezo aliyoyasoma ambayo ndio yaliyomjulisha kuwa mawazo yake yanafaa juu ya kazi anayoifanya kwa sababu anaona kuwa subra ndio nyenzo kuu ya mafanikio bila kusubiri hakuna mafanikio yoyote yatakayopatikana na siku zote mwenye kusubiri hakosi.

#### 4.6.4.10 Uvumilivu

Ni hali ya mtu kuwa katika hali ya ustahamilivu kutokanana masaibu yatakayokumba au kukukabili. Katika riwaya hii, dhamira ya uvumilivu nayo pia imekuwa nyezo kuu ya kujipatia ukombozi katika maisha ya mwanadamu, ili kuendeleza na kupatikana mafanikio ni budi kwa mtu yoyote kupambika kwa uvumilivu,akaweza kustahamili vikwazo na vitisho vitakavyotokana na adui zake kwa sababu mara nyingi wao huwa ndio wenye nguvu kuliko wanaotafuta ukombozi. Si hivyo tu, kuwepo na jambo hili ni muhimiii mkubwa wa maslahi ya jamii na umma kwa ujumla kwa sababu kutawafanya hata wale wanaojidai kuwa ama wana madaraka au nafasi fulani kusalimu amri na kukata tamaa na mwisho utesaji huondoka na kuwapa fursa na uhuru wale watafutaji wa uhuru au ukombozi na hapo hufikia kilele cha matajio na mafanikio ya jamii. Hakuna shaka yoyote katika Kusadikika kuwa uvumilivu ndio kigezo kilichowapelekea wajumbe sita ili kupata mafanikio ya nchi yao licha ya vikwazo viliyowakabili, wajumbe hao walikumbwa na tufani za mateso na kebehi hadi kufikia kuzomewa na kutupwa jela ila hawakukata tamaa dhidi ya mateso hayo bali walizidi kusonga mbele kwa kadiri wanavyoweza ili kuhakikisha wanapata suluhu wa makusudio yao. Kwa mfano, mtafiti anapomuangalia mjumbe wa Mashariki anayeitwa Fadhili alithibitisha ya kwamba mja huyu alikuwa mvumilivu kwa kustahamili vikwazo kadhaa hadi kufikia alikokusudia.Mtunzi anasimulia kwa kusema:

> “Nchi za Mashariki kama zijulikanavyo ziko n’gambo ya matlai na bahari zilizo pana sana.Fadhili ilimpasa kuabiri na kujihaulisha katika vyombo mbalimbali.Kwa kufanya hivyo aliingia katika bandari kadhaa wa kadhaa.Safari yake ilichukua miaka mingi ya majaribu magumu,walakini alikuwa ni mvumilivu wa ajabu,uvumilivu wake

> ulikuwa hauna mwisho.Labda kwa kufadhiliwa kipawa hichi ndipo alipoitwa Fadhili”.(uk:16)

Mtafiti akihusisha na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ameona kuwa kipengele hiki kina uwiano halisi kati ya maana inayosomwa na jinsi msomaji anavyohakiki kwa sababu kwa mujibu wa riwaya hii ya *Kusadikika* bila shaka dhamira ya uvumilivu ndio aliyoibaini mtafiti. Mfano, Fadhili hakujali vikwazo vya safari isipokuwa alizidi kustahamili na kusonga mbele.Vilevile na wajumbe wengine waliosalia.

#### 4.6.4.11Ushujaa

Ni hali ya mtu kuweza kujiamini na akajiepusha na hofu kwa kuweza kueleza ukweli uliofichikana na kuudhihirisha hata kama utawachukiza walengwa, au ni kuweza kujitetea ama kwa kauli au kimatendo bila ya kutetereka.Katika riwaya ya *Kusadikika,* mtafiti amegundua kuwa ushujaa nao umekuwa kiwakilishi kikubwa cha maendeleo ya jamii na upatikanaji wa ukombozi dhidi ya udhalilishwaji juu ya jamii husika. Jamii yoyote iwayo ikiwa inahitaji ukombozi, ushujaa ni kikomboleo cha ukombozi huo. Hata jamii ya Wasadikika ilikomboka kutokana na ushujaa wa Karama. Yeye ni muhusika aliyejikita zaidi katika masuala ya uanasheria ambayo ilikuwa haijulikani kabisa kwa jamii ya wasadikika, hivyo ilikuwa kikwazo, shida na dhiki kubwa kuelimisha hadi ikafahamika kwa jamii hiyo iliyopofuka kabisa na kuwa nyuma kwa maendeleo yote ya jamii. Kwa ustadi mkubwa, Karama ambaye alikuwa kiumbe duni na dhalili kwa serikali wa Wasadikika, alitumia ushujaa wake aliokuwa nao ambao ndio uliomtengeneza na kumpa hadhi hadi akuvuta nyoyo za wasikilizaji wote waliokuwapo katika mahakama hiyo mbele ya kiongozi Majivuno aliyejaa taadi na inda dhidi ya Wasadikika wote. Msanii anasema:

> “Kwa wasifu wa nje,mshtakiwa alikuwa hana umbo la kufanya mvuto kwa watu,lakini kwa wasifu wa ndani alikuwa na ajabu tatu,kichwa chake kilikuwa na ubongo wa hekima,kifua kilikuwa na moyo wa ushujaa na kinywani ulimi wa ufasaha.Vitu hivi vitatu vilikuwa katika siri kubwasana.Hata baadhi ya wasiri wake hawakuweza kukisia kuwa alikuwa na hazina kama hii….Basi pale kizimbani alipokuwa amesimama wima aliinama kwa unyenyekevu mbele ya baraza, alipoinuka kwa sauti ya taratibu lakini imara,aliyavuta masikio ya baraza mzima kumsikiliza kama imamu aliyekuwa akihutubu juu ya mimbari ya msikiti mkubwa”(uk:7).Ushujaa ni hazina kubwa na bora ya kudumishwa .Ushujaa kwa mtu ni ngao,kwa nchi ni tegemeo na kwa taifa ni uwezo.(uk:17)

Kwa kuhusisha na nadharia teule ya Mwitiko wa Msomaji,inaonesha kwamba ni kweli kuna wasomaji ambao husoma na kufasiri kazi za fasihi kutokana na kuwa mawazo yake yanafaa na yana maana pana katika jamii iwapo watayasikilizwa, kuyapima na kuyafuata katika matendo yao ya kila siku. Mtafiti anaona kuwa kwa kila mwana maendeleo anayo haja ukubwa ya kupambana na vikwazo vitakavyomkabili ili kama alivyobainisha msanii, kwa hasa anakusudia kuielimisha jamii iachane na woga, hofu au shaka yoyote katika kupambana na maendeleo yake, hata kama pana adui zake ni vyema kusimama wima kwa lengo la mahitaji yaliyomzunguka.

**4.6.4.12 Ujasiri**

Ujasiri ni hali ya mtu kuweza kufanya kitu au kuzungumza kitu kilichomea katika moyo mbele ya wakubwa wake, viongozi wake au waliomzidi kwa hali moja au nyengine bila ya woga hata kama anaamini kuwa kitawaudhi na kuwakera katika nyoyo zao. Katika riwaya ya *Kusadikika*, ujasiri unaonekana kupitia Karama ambaye alitoa dukuduku lake mbele ya kaumu na Mfalme, waziri na viongozi wengine hadi akaweza kuitoa elimu juu ya uanasheria ambayo inaaminika kuwa ni elimu ngeni katika jamii hiyo. Vile vile, katika ukurasa wa kumi na moja anaonekana mjumbe

wake akisafiri kwa ujasiri licha ya vikwazo vilivyomkabili katika safari yake. Hii ni kwa sababu, alitaka zaidi mambo ya Wasadikika yawe mazuri na sawiya kwa watu wake. Mwandishi anasema:

> "Ujumbe huu ulikuwa na dhima kubwa, zamani wasafiri walivyoondoka katika nchi walizozijua na kusafiri katika nchi walizokua hawazijui, msafiri huyu pia alikujua alikotoka lakini hakukujua alikokwenda.Hakujua kama mbele alikua akingojewa na msaada wa kumsaidia au maangamizi ya kumuangamiza, alijitolea sadaka katika ujasiri ambao misiba yake ilikuwa katika mwangaza lakini faraja yake ilikuwa katika kiza kikuu". (uk:11)

Kwa kuhusisha na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ni kuwa kuna uhusiano wa kutosha kati ya maana inayosomwa na jinsi msomaji anavyohakiki kwa sababukuweza kujitetea mbele ya hadhara pasi na tone la woga wala kutetemeka ni ishara tosha ya ujasiri,mtu ovyo ovyo hawezi kuzungumza chochote kwa woga na pengine asiweze hata kusimama hadharani kama hivyo.

#### 4.6.4.13 Kutokata Tamaa

Ni hali ya mtu au kikundi cha watu kutorudi nyuma katika kutafuta maendeleo ya jamii zao. Kwa mujibu wa mtafiti katika riwaya hii ya *Kusadikika* ameona kuwa ni wazi kabisa kuwa mwanandamu hatakiwi kukata tamaa katika kutafuta maslahi binafsi au ya umma. Mwanaadamu huyo, ni vyema awe anawajibika kufanya juhudi za kusudi kadiri anavyoweza ili kuleta mafanikio ya jamii na nchi husika. Hivyo, kuna maeneo mbali mbali yanayoonesha ushahidi wa kutosha juu ya maelezo yanayothibitisha ukweli wa nukta hii, nayo ni katika ukurasa wa 16,17,18,21,34 na 35. Katika ukurasa wa 21 anaonekana Kabuli aliyekuwa mjumbe wa Kusini amabaye hakuonekana kukata tamaa na alifanya juhudi ya kuzitembelea nchi za

upande huo, Pamoja na vikwazo vilivyomkabili, alifanikisha kupata mengi aliyokusudia ambayo aliamini kwamba lau yangalifuatwa katika nchi ya *Kusadikika*, matunda ya maendeleo yangalikuwepo na kupelekea faraja kwa nchi ya Wasadikika. Badala yake yalipokewa marejeo yake kwa kuzomewa na kuitwa mwongo, mwoga na mwotaji wa ndoto zisizotabirika. Mwandishi anasema:

> "Kama ijulikanavyo Kusini ni upande wa dunia yatokayo matufani mengi makubwa na baridi kali sana.Kabuli aliyakabili mashaka na kigeugeu. Pamoja na mashaka hayo alikwenda na safari zake hadi akapata faraja na mafanikio juu ya nchi yake … Zamani za marejeleo yake hapa, alisema habari za mamlaka ya kiasi, heshima iliyo ya wastani, uhuru wa kadiri na nguvu yenye mpaka. Mtu mwenye mamlaka ya kiasi hatwesi watu waliochini ya mamlaka yake wala hajitesi yeye mwenyewena wengine,mwenye heshima iliyo ya wastani ni hujiheshimu yeye na wengine,mwenye uhuru wa kadiri ni muungwana yeye mwenyewe na wengine na mwenye nguvu yenye mpakahadhulumu wala yeye hadhulumiwi".(uk:23,25)

Kwa kuhusisha na nadharia ya Upokezi ni kuwa mtafiti ametumia kigezo cha kupambanua maana kulingana na maelezo yaliyotolewa katika nukuu iliyotangulia kwa sababu maelezo aliyoyatoa Kabuli katika kuijenga nchi yake na lau yangalifuatwayangalitoa maendeleo makubwa ila yalizamishwa katika dimbwi na kiza kinene chaujinga uliwogubika wakuu wa nchi ya Kusadikika na wakaazi wake kwa ujumla.

#### 4.6.4.14 Kujitolea Muhanga

Ni hali ya mtu au kikundi cha watu kupigania haki zao kwa namna yoyote hata kama wanaamini ya kwamba wanaweza kupata matatizo au vipingamizi vizito katika mapambano hayo.Katika riwaya ya *Kusadikika*,dhamira ya kujitolea muhanga nayo ni nyenzo muhimu katika kutafuta ukombozi juu ya jamii husika. Pahala popote pale

pakiwa na watu wenye moyo huo, maendeleo ya wanajamii yatapatikana kiurahisi kabisa. Katika riwaya hii ya *Kusadikika* wajumbe wote walijitoa muhanga bila ya kujali ajali yoyote itakayowatokezea katika safari zao, Kwa sababu waliamini hakuna hata mmoja kati yao aliyejua endako wala kujua safari hiyo itakuwa namna gani ila kwa bahati njema walikwenda wakiwa katika furaha kama kwamba ni wenyeji wa nchi hizo. Nae Karama aliweza kujiteta mbele ya mahakama pamoja na umati mkubwa uliokuwapo bila ya hofu wala shaka yoyote juu ya kikwazo chochote ambacho kingeweza kutokezea na kuwa kafara ya uhai wake. Mtunzi anathibitisha kwa kusema:

> “Hii ilikuwa siku ya kwanza ya muda ulioamriwa.Baraza ilihudhuriwa na Mfalme,Waziri pamoja na wasimamizi wengine wa serikali.Sudusi moja ya watu wa Sadiki,mji mkuu wa Kusadikika,walikuwapo vile vile. Mbele ya baraza hii, Karama, mshtakiwa alisimama kujitetea bila kutetemeka.Alisema kwa makini kama mtu aliyezoea kusema hadharani.(uk:9)

Mtafiti kwa kuhusisha na nadharia teule ya Mwitiko wa Msomaji ni wazi kuwa ametumia kigezo cha maelezo yaliyomo katika riwaya aliyosoma na kuihusisha na jamii halisi na ameona ya kwamba kuna uwiano mkubwa kati ya mambo hayo mawili.Mataifa yote duniani yamekuwa na watawala wake, ikitokezea mtawala kushindwa kutekeleza majukumu ya wana jamii hutokea wengine wakahalifu na kutaka mabadiliko ili kuondosha migogoro na uonevu huo

**4.6.4.15 Uzalendo**

Hii ni hali ya mtu au jamii kuipenda nchi au taifa lao kwa kutaka kulikwamua kwa kulipatia maendeleo ama juu ya udhalilishwaji, unyonywaji au dhulma nyengine yoyote ambayo inaweza ikawa ni kikwazo kwa wanajamii au wananchi kwa pamoja.

Mtafiti amebaini kuwa suala la uzalendo katika” *Kusadikika”*limejitokeza zaidi kupitia Karama, aliipenda nchi yake na kuiona ni bora kuliko kitu kingine chochote. Hivyo, kupitia wajumbe waliowatajwa, Karama alibainisha kuwa  wajumbe hawa ni kigezo tosha cha watu watakaojaribu kuwa na mwenendo kama huu, kutokana na mateso aliyoyapata kama si kupambika na sifa hii asingalikubali tena kushirikiau kuendelea ila alikwenda kwa furaha na matumaini mema bila kulazimishwa na hata kuhofia kifo. Kwa mfano, mjumbe wa ardhini alitaka nchi ya Kusadikika iwe na vyombo vya usafiri badala ya kuja na mangera kama alivyofanya mjumbe wake. Alitaka kuchukua mwalimu ila ikashindikana kutokana na shida ya usafiri.Mtunzi nasema:

> “Mjumbe wa ardhi aliporudi Kusadikika alinena kuwa wenyeji katika ardhi walikuwa waadilifu wakubwa kabisa, na kuwa walipasa kuigwa katika bidii zao kama Kusadikika ilitaka kuendelea katika ustawi. Alitaka sana kuja na mtu mmoja wa Ardhi katika nchi hii. Mtu huyo alikusudiwa kuwa kama mwalimu hapa lakini haikuwezekana. (uk:40)

Karama alileleza hilo kupitia mjumbe huyo kwa kujua ya kwamba endapo Kusadikika itafanya hayo, itajipatia uhuiano mkubwa na nchi ya Ardhini. Pia,Karama alionesha uhusiano mkubwa wa nchi jirani kwani, kwa uthibiisho wa wajumbe hao  ni kuwa, walikwenda nchi tafauti wakaweza kuhimili mateso na vikwazo na kila mmoja alikuja na malekekezo yake kwa jamii hii ya Kusadikika ila kwa bahati mbaya na upofu wa serikali yao wakapata zawadi wasiyoitegemea kabisa. Hivyo, Karama alionyesha uchukivu wa jambo hilo walilotendewa wajumbe hao dhidi ya serikali yao na kuiomba iwape haki zao kama raia wengine ikapelekea kuanzisha elimu ya uanasheria.

Kwa kuhusisha na nadharia teule ya Mwitiko wa Msomaji kupitia mihimili yake inaonekana kwamba kuna uwiano mkubwa kati ya maana inayosomwa na jinsi msomaji anavyohakiki. Dhamira hii ya uzalendo inathibitisha kuwa kupitia mjumbe huyu hakuona tunu kitu chochote wala mali aliyoipata zaidi ya nchi yake na hata katika jamii za kawaida baadhi ya watu huhiari wahatarishe maisha yao ila wapambane juu ya nchi zao kwa lengo la kuleta maendeleo ya mataifa yao. Hivyo, hujiunga na nchi nyengine na kujenga uhusiano kwa baadhi ya mambo.

#### 4.6.4.16 Kuondoa vita na chuki

Katika riwaya ya *Kusadikik*a mtunzi ameeleza juu ya suala hili kupitia Mjumbe wa Mashariki ambaye alikuwa ni Fadhili, alipotembelea huko aliwakuta watu wanaishikwa upendo na udugu wala hakukuwa na vita vya aina yoyote, hivyo alikuja na ujumbe nzuri kwani alinenena kuwa watu wa huko hawakujihusisha na vita kama ilivyo Kusadikika, vita kwao vilikua kama adui mkubwana aibu tosha kwa taifa lao. Mtunzi anasema:-

> “Karibu watu wote huko walichukiauchokozi kama aibu kubwa, na waliviapiza vita kama laana ipitayo kiasi kwa viumbe waliojaaliwa busara ya haki, moyo wa wema na ulimi wa nasaha.”(uk:16)

Kwa mujibu wa nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ni kwamba vita ni adui wa maendeleo na ni janga sugu katika jamii kwa sababu inapelekea maafa na madhara ya kila aina. Mji au taifa lolote liwalo hata likawa juu na bora kuliko kiasi gani ilijihusisha na vita hukosa hadhi na ufanisi wa kazi zake, pia hutoa maafa na makubwa kama vifo, maradhi, umaskini na utelekezwaji wa watoto na wanawake. Mfano, Kongo, Kagera na Palestina hadi leo hakuna amani katika nchi, watu

wanaishi uhamishoni kwa sababu ya kukimbia vita. Jambo linalopelekea kukosa uhuru wa kuishi kwa namna wanavyotaka wenyewe. Karama alieza vyema kuwa palipo vita hapana mandeleo, hivyo vita havifai katika jamii yoyote duniani kote.

#### 4.6.4.17 Viongozi wawapende raia zao

Upendo ni kitendo cha mtu mmoja kumpenda mwengine. Katika riwaya ya *Kusadikika*, dhamira ya upendo imebainishwa na Karama kupitia simulizi la Fadhili aliyekuwa mjumbe wa Mashariki. Alipofika huko alikuta jamii inasomeshwa namna ya kupendana baina ya wanaadamu, walijifunza urafiki ambao iliaminika kuwa ni kiungio cha maendeleo yao. Mwandishi anasema:-

> "Mafunzo yote katika nchi hiyo yaliambatanishwa na siasa hii. Katika vyuo, watoto walikuwa wakijifunza taaluma ya kufanyiza urafiki mkubwa ambao mwanaadamu aliupoteza mwenyewe; lakini baada ya kuliona kosa lake, sasa amejifunga kwa kuutafuta tena, watoto wote walikuwa pamoja kwa upole kama kondoo"(uk:17).

Hivyo, Karama aliitaka serikali ya Kusadikika kuwapenda raia zake kwa namna inavyostahiki na kujua ya kwamba serikali na raia ni kitu kmoja na bila ya raia wema hapana serikali nzuri na imara. Ni vyema kuwatunza na kuwapenda ili wawe wazuri na wema wenye kuwapenda viongozi wao.Nukuu hii inaonesha kwamba, nchi za mashariki uelewano na urafiki ndio nyezo muhimu kwao katika kuleta maendeleo.

Mtafiti amekuja na maoni hayo hukuakihusisha nadharia ya Mwitiko wa Msomaji kupitia muhimili wake unaompa fursa ya uhakiki wa matini kutoikana na uoni wake. Kupitia muhimili huu unaosema kwamba kila kazi ya fasihi ina maana kufutana na msomaji binafsi na jinsi anavyoichukulia. Kwa muktadha huo mtafiti anaamini kwamba, mafunzo ya kufanyiza urafiki ni mfano hai unaoonesha kupatikana kwa

upendo. Binaadamu wakiwa marafiki bila ya shaka watapendana na kuoneana huruma kwa kila jambo. Hii husaidia kujenga udugu wa hali ya juu na kuwa karibu kama kwamba ni ndugu wa familia moja na pengine hawana uhusiano wa aina yoyote isipokuwa urafiki tu.

#### 4.6.4.18 Kuendesha nchi kimabavu

Ni hali ya kiongozi kujiepusha kutumia nguvu kwa raia wake badala yake akajitahidi kuwa na hekima ambayo inahusisha maneno yaliyo mazuri na yenye unyenyekevu mkubwa katika mazunguzo na vitendo. Maneno yanapokuwa mazuri na thabiti yakaweza kuzungumzwa kwa ufasaha na namna inavyostahiki huwa ni kivutio cha watu kwa kujenga uelewa mwema kwa wasikilizaji.Katika kazi za fasihi,kunamsemo usemao kuwa: "*Maneno mazuri humtoa nyoka pangoni*".Katika kuthibitisha hili kupitia riwaya ya "*Kusadikika*" anaonekana Karama namna alivyojengeka kwa hekima. Hii pia ilikuwa sababu ya kumfanya mfalme akhairishe kesi ampe siku zake sita kama alivyoomba.Si hivyo tu, wakati anaelimisha jamii juu ya elimu ya uaanasheria alivuta nyoyo za watu wote ikapelekea kila siku ikawa uwanja unafura kwa kujaa watu ili kumsikiliza mshtakiwa. Mwandishi anasema:

> "Wasifu wanje mhtakiwa alikuwa hana umbo la kufanya mvuto kwa watu, lakini kwa wasifu wa ndani alikuwa na ajabu tatu, kichwa chake kilikuwa na ubongo wa hekima, kifuani alikuwa na moyo wa shujaa na na kinywani ulimi wa ufasaha."(uk:7)

Katika kuhusisha na nadharia teule ya Mwitiko wa Msomaji katika kipengele cha uwianao, mtafiti anaona kuwa kuna uwiano wa kutosha kati ya maana inayosomwa na jinsi msomaji alivyohakiki,maneno yenye hekma siku zote huwa ni kikomboleo cha mafanikio,pasipokuwa na hekma mara nyingi hutokezea kibri,jeuri na kebehi

kwa wengine.Jambo ambalo halipendezi na huleta uchukivu na husda kwa walengwa.

#### 4.6.4.19 Kuhubiri amani

Ni maneno mazuri yenye kuambatana na hekima, pia hujikita zaidi katika kuafanya mambo/ tabia njema. Kwa kawaida, amani hupambwa na busara ambayo hupelekea wema na upendo ndani mji. Katika riwaya hii, Karama ameieleza dhamira hiikupitia mjumbe husika katika ukuarasa wakumi na sita wakati Fadhili alipokwenda upande wa mengi yakiwemo ambayo aliamini kuwa endapo yatafuatwa katika jamii ya Wasadikika basi mambo yangalikuwa mazuri.Mwandishi anasema:

> "Karibu watu wote huko walichukia uchokozi kama aibu kubwa na waliviapiza vita kama lana ipitayo kiasi kwa viumbe walojaliwa busara ya haki,moyo wa wema…Neno uadui na mengine mabaya kama yajulikanavyo watu walikusudia kujaribu kuyatoa katika lugha na kuyafuta katika vitabu. Kwa amri ya serikali matangazo yalienezwa juu ya njia panda, bara bara kuu na kila mahali pa mikutano ili kuzuia matumizi ya maneno hayo."(uk:16-17)

Mtafiti akihusisha na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji anahakikisha kwamba ni kweli kila kazi ya fasihi ina maana kufuatana na binafsi na jinsi anavyoichukulia msomaji na kuona kwamba palipo na amani hutawala huruma na upendo hukithiri, hata mapambano ya kivita na uadui si rahisi kutokezea, watu hujitahidi waishi kwa udugu na kuhurumiana na endapo patatokezea mzozo wa aina yoyote basi jamii huwa tayari kutafuta suluhisho la kuondoa mzozano huo.

### 4.6.5 Ukombozi wa kijamii

Ni ukombozi unaojikita zaidi juu za huduma za kijamii kama makazi bora, maji safi na salama, elimu, barabara n.k. Mtafiti ameubainisha katika utafiti wake kama unavyoonekana.

#### 4.6.5.1 Makaazi bora

Katika riwaya lengwa, mtunzi amemtumia Buruhani kama ni kiwakikishi cha ukombozi wa makaazi yaliyomazuri na salama. Anaamini kuwa, miji safi na salama ndio kivutio cha nchi na humfanya mwanadamu kuishi katika hali iliyo bora na yenye kuvutia, anaona kuwa ipo haja kwa wana jamii ya Kusadikika kujiingiza katika ustaarabu huu na si kudhani kuwa ni uharibifu wa mazingira au ubadhirifu wa mali za uma.Mtunzi anasema mupitia Buruhani kuwa:-

> "Kwa kukosekana maji safi, maisha ya Kusadikika yanachukiza. Jengo la kitambo linalopendwa lina gharama kubwa sana kuliko jingo la aushi lilokataliwa. Kibanda hutaka kutengenezwa siku zote, mtu akiishi umriwa miaka mia moja itampasa kukitengeneza kibanda chake karibu kila mwaka mmoja. Gharama na kazi za jengo hili huanza kidogo lakini huzidi kuwa kubwa kila wakati, jengo la aushi lina gharama na kazi kubwa pia lakini baada ya kukamilika gharama wala kazi hizohazikaririwi mara mara. (uk:13)

Kwa kuhusisha nadharia ya Mwitiko wa Msomaji, katika kipengele cha uhusiano uliopo kati yamawazo ya mtunzi na namna mhakikialivyoihakiki kazi yake ni kuwa inawiana kwani inaonekana wazi katika jamii, popote panapokuwa na majengo mazuri na mazingira pia huwa mazuri na kuvutia kiasi ambacho kitakuwa ni kivutizi tosha kwa wageni na nifahari iliyoje kwa wenyeji na wakaazi wa eneo hilo. Majengo mazuri pia humfanya mtu kuishi maisha yaliyomema na kupata matumaini

ya kuishi kwa usalama zaidi kuliko kuishi katika vibanda kama walivyoishi Wasadikika.

#### 4.6.5.2 Maji safi na salama

Katika riwaya ya *Kusadikika*, mtunzi ameeleza umuhimu wa maji safi na salama. Watu wa Ardhini wakinywa maji meupe, jambo lililomshangaza Amini kwani, Kusadikika hakukuwa na maji safi kama hayo. Pia, hakurudi nyuma katika kueleza athari ya maji yasiyofaa kwa jamii ya Kusadikika ili iwe nikiwakilishi cha jamii nyengine duniani kwa ujumla. Amesema:

> “Walikuwa wakinywa maji meupe na si damu. Amini alisema kuwa sababu ya kukosekana rangi katika kinywaji chao ilikuwa damu yenyewe ilikuwa ikivuja kutoka mbali Sana, ilichujuka rangi yake kwa upepo ikawa nyepesi kama maji, Maji ya Kusadikika yalikua meupe kama theluji na mepesi kama hewa. Watu wa Ardhi walinena kuwa maji yaliyo meupe kma theluji si maji ila ni theluji na yaliyo mepesi kama hewa si maji ila ni hewa. Jibu likisadifu swali shaka huondoka”.(uk:43)

Kwa kuhusisha na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji nikuwa inaakisi vyema uhusiano uliopo baina ya mtunzi na mawazo ya muhakiki kwani bila ya maji yaliyosalama maisha wanaadmu na viumbe vyengine kwa pamoja yatakuwa hatarini. Hivyo, ni vyema kwa kila mwanajamii kutumia maji mazuri na salama pia kutunza vianzio vyake ili kuokoa maisha yake kutokana na magonjwa ya mripuko kama kipindu pindu, kichocho na malaria,kwani yatapelekea vifo na kusababisha umasikini kwa kukosa wazalishaji. Kupitia Amini ambaye alikuwa mjumbe wa Ardhini, Karama ameielimisha jamii ya Wasadikika kutokana na maji yaliyobora kwani wao hawakuwa wakiywa maji bali ilikuwa theluji na hewa. Kiasi ambachoyalikuwa ni hatarishi kwamaisha yao

### 4.6.5.3 Umiliki wa mali

Katika riwayaya *Kusadikika*, umiliki wa mali ulionekana katika maeneo mbali mbli, Karama aliuainisha kupitia maelezo ya wajumbe kadhaa wakati ambapo wajumbe hao walipata maelezo mara tu baada ya kurudi safari zao. Kila mjumbe alikuja na maelekezo yake kulingana na aliyoyakuta. Kutokana na hayo, muhusika Kabuli, ambaye alikuwa mjumbe wa Kusini katika nchi ya Kiasi, alikuja na namna watu wanavyomiliki mali katika nchi hiyo ya Kiasi. Huko kabuli alikutana na mengi ambayo yaliendana na jina la nchi hiyo. Mfano kila kitu alichokutana nacho Kabuli huko kilikuwa kwa kiasi, hakuna kilichotumiwa kwa fujowala mmiliki aliyejiringa na kujiona kwa sababu ya kuwa kwake na mali au awezo bali vyote vilipangwa kwa kiwango maalumu kulingana na mahitaji ya wana Kiasi kwa pamoja. Kutokanana hali hiyo, jamii ilijipatia faraja kubwa kwani kila mmoja miongoni mwao aliheshimiwa na kupata uhuru wake wa kuishi, jambo lilipelekea upendo mkubwa katika jamii ya wana Kiasi. Ushahidi wa hayo umedhihirishwa kama inavyoonekana hapo chini:

> "Zama za marejeleo yake hapa alisema habari za mamlaka ya Kiasi, heshima iliyo na wastani, uhuru wa kadiri na nguvu yenye mipaka, mtu mwenye mamlaka ya kiasi hawatesi watu walio chini ya mamlaka yake wala hajitesi yeye mwenyewe, mwenye uhuru wa kadiri ni muungwana yeye mwenyewe na wengine, mwenye nguvu yenye mpaka, hadhulumu wala yeye hadhulumiwi, mambo manne haya ni mbegu za mimea ya mazao ya hali njema, mapatano, ustawi na amani duniani"(uk:23).

Kwa kuhusisha ya Mwitiko wa Msomaji katika nukta inayoonesha uhusiano kati ya mtunzi na namna muhakki alivyoihakki kai yake ni kuwa, bila ya shaka ni wazi kuwa panapohitaji maendeleo lazima papambike kwa kuheshimiana na kuhurumiana, kila mtu awe na uhuru wa kufanya au kutenda atakalo,mwenye nguvu, mamlaka, mali na

uwezo asijione na kuwadhulumu au kuwatesa wengine. Kila chembe ya kinachomilikiwa katika jamii husuka chatakikana kiwe mali ya uma na si kwa wenye mamlaka. Hapo ndipo patakapopatikana upendo, huruma na busara na kuondokana katika vizingiti vya uziwi na upofu wa chuki na husda baina ya sererikali na wananchi kwa ujumla. Kwa sababu raia hao watawapenda viongozi wao na viongozi watawapenda raia wao. Pia, itapelekea waishi kindugu bila ya kuzingatia hadhi zao ama zakimamlaka au kikabila na hapo ndipo maendeleo ya nchi na jamii kwa pamoja yatakapopatikana na kuwa mazuri na salama.

**4.6.5.4 Uharifu wa mali za umma**

Nukta hii pia anaelezwa katika riwaya ya "*Kusadikika"*, viongozi wengi ni wabadhirifu wakutumia mali katika njia isiyofaa. Mfano, kutumia fedha za serikali kwa starehe na mengineyo hivyo hutumbukia katika maangamizi ya ufukara wa milele. Pia majina ya watu nayo yanaashiria uharibifu. Mfano, Majivuno, Bora Mimi, Fujo, Fila na Sapa. Mwandishi amedhihirisha athari ya uharibifu wa mali katika maelezo yafutayo:-

> "Kwa ujinga wa kimatumizi yetu, mali zetu zote huishia katika ngoma na tafrija za kufukarisha...Watu watumiyao mali zao kwa uharibifu husemwa kuwa wametumbukia katika maangamizi ya matumizi, mwisho watu hao huvunjwa vunjwa katika maanguko ya umasikini, yaani, njaa, kiu na uchu….. Ujinga wa matumizi yetu hututenga na hazina zetu, na uvivu wa kunyanyua hazina zetu hutuchelewesha nyuma siku zote."(uk:30)

Kwa kuhusisha nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ni hakika inakwenda sambamba kulingana na mawazo ya msanii na namna mhakiki anavyoihakiki kazi yake kwa sababu jamii nyingi zimekumbwa na tatizo hili, viongizi hutumia mali za uma bila ya

uangalifu. Mfano, kutumika katika tafrija za papo kwa papo badala ya kutumika kwa shughuli za kijamii kama ujenzi wa shule, hospitali, barabara na vianzio vya maji. Jambo hili hupelekea uduni wa maisha katika jamii hizo. Karama amelisema hili kupitia mjumbe wa Magharibi ili kuidhihirishia jamii yake hatari ya jambo hili. Hivyo, ni vyema litupiliwe mbali kwa lengo la kufanikisha maendeleo ya uma wa Kusadikika.

#### 4.6.5 .5 Kuondosha chuki na uadui

Ni hali ya mtu kujiepusha uchungu au uchukivu kwa mwenginee. Badala yake, kuweza kuungana baina ya kikundi cha watu au jamii moja kuungana na jamii nyengine. Mfano, tunaposema Umoja wa Afrika Mashariki, hapa tunafahamu kwamba ni muungano wa nchi za Afrika Mashariki (mfano; Tanzania, Kenya, Uganda).Mtafiti amegundua kuwa suala la umoja na mashirikiano limetawala katika jamii ya Kusadikika kupitia wajumbe wote sita. Wajumbe haowaliungana kwa moyo wa dhati na kitu kimoja kwa hali na mali, jambo lililostaajabisha wana Kusadikika na kujenga imani ya kutaka kusikiliza ili kujua hatima ya kikao hicho.Mshtakiwa Karama aliweza kulieleza hili kupitia wajumbe sita ambao hawakuogopa vitisho na vikwazo vilivyowakabili wao pamoja na familia zao, ilikuwa taadi na inda za taabu na mateso yaliyokithiri, bila ya kujali utu wala hisani za kibinadamu. Kitendo cha wajumbe kujitolea bila kulazimishwa ni uthibitisho tosha wa hoja hiyo.Kwa mfano, mtunzi anasema kupitia mjumbe wa Magharibi kuwa:

> “Mtu aliyejitolea mwenyewe kwaujumbewa Magharibi alikuwaAuni. Auni alijuakaziyawatangulizi wake ziliishia katikamto wa jangwani unaoyapoteza kazi yake bure lakini hakulegea”(uk:28)

Kwa kuhusisha na nadharia teule ya Mwitiko wa Msomaji mtafiti amethibitisha ya kwamba kuna uwiyano kati ya maana inayosomwa na jinsi msomaji anavyohakiki kwa sababu pahala popote patafutwapo ukombozi au maendeleo lazima kwanza watu wawe kitu kimoja kwa kuungana na kushikamana bila utengano au khitilafu yoyote. Aidha, wanajamii wanatakiwa wasiwe na ubaguzi kwa kuangalia rangi, cheo au kabila kinyume chake itakuwa vigumu kupata mafanikio wanayoyahitaji.

#### 4.6.5.6 Upapiaji wa mali

Katika riwaya ya "*Kusadikika"***,** suala la upapiaji wa mali limejitokeza katika sehemu tafauti. Viongozi walipapia mali kiasi ambaho kila kitu kwao kilikuwa hakitoshi. Kwa mfano taifa la Majuju ni taifa ambalo lilikula na kun'gan'gania kila kitu. Kitu kigumu kilikua rahisi na laini walikula na kupapia na awakutosheka. Mwandishi anasema:

> **"**Majuju ni taifa lafi na litishalo kabisa. Kila kitu kigumu kijulikanacho duniani kilikua laini kama mkate katika meno ya Majuju; na kilicho kichungu kilikua kitamu kama asali katika maonjo yao, kwa ulafi uliokithiri viumbe hawa."(uk:21)

Kwa kuhusisha nadharia ya Mwitiko wa Msomaji, katika kipengele cha uhusiano uliopo kati ya mawazo ya mtunzi na namna mhakiki alivyoihakiki kazi yake ni kwamba inaligana vya kutosha kiasi ambacho, watu wengi katika jamii za kawaida wanan'gan'gania na kupapia mali huku wakijitapatapa kwa kiu na njaa.Hawashibi, hawatosheki wala hawachoshwi na chochote wanachokiona. Hawajui halali wala haramu kila kitu kwao ni sawa hata kama kitaleta madhara kwao na kwa jamii zao.

#### 4.6.5. 7 Barabara safi na salama

Katika kutetea hilipia Karama hakurudi nyuma, amemtumia Buruhani kama ni kiwakilishi cha kukombolea hali hii. Mtunzi ameeleza kuwa bara bara ndio chachu ya maendeleo ya uchumi wa nchi, palipo bara bara wakulima watapata njia ya kusafirisha mazao ya kila aina kutoka sehemu mbali mbali. Kwa kuthibitisha hayo, Shaban Robert mesema:

> "Uchache wa njia nzuri huchelewesha mwendo na huufanya uchukuzi wa bidha kuwanzito.Hapana kitu kijacho wala kiendacho kwa upesi kama itakiwavyo, hata kama nchi ina mazao namna gani lakini kama haina njia ya kuyapeleka mazao yake katika soko kubwa faida haipatikani hata kidogo.Kwa kukosekana kwa madaraja,mito inafanya shida juu ya watu walio ng'ambo moja kukutana na walio ng'ambo nyengine." (uk:13)

Kwa kuusisha nadharia tajwa ya Mwitiko wa Msomaji ni kwamba inaakisi vya kutosha kwa sababu inaaminika kuwa, njia ni kiungio kikubwa baina pande moja na nyengine kwani husaidia wasafiri kutoka sehemu mbali mbali za dunia. Kwa mfano, daraja ni kivuko nyeti kwa wasafiri wa sehemu zilizo mabonde au maji. Kwa upande mwegine ni kwamba, pasipo bara bara nzuri na salama wa wasafiri, biashara zitakua ngumu kuendelea. Hali itakayozorotesha maendeleo ya biashara katika jamii husika.

#### 4.6.5.8 Matibabu bora

Katika riwaya teule, mtunzi ameainisha matibabu yaliyo mazuri ili kuondosha magonjwa. Amesema:

> **"**Mardhi hayajapata uuguzaji wa kutisha. Vifo vya mapema hapa katika mwaka mmoja jumla yake yatisha sana kuliko ile ya vifo vitokeavyo katika nchi nyengine katika karne moja. Fikirini kama maisha kama haya yanavumilika au hayavumilika, kama hatari hii ya maangamizi ya watu kabla ya wakati wao halazimu kuzuiwa kwa

> bidii yote aliyonayo mwanadamu. Katika amani watu hawatazamii kuchukuliwa na mauti kwa wingi kama ilivyo katika baa la vita."(uk:13)

Kwa kuhusisha na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ni kuwa, mtafii ni kwamba kuna uhusiano mkubwa baina ya mtunzi na namna mhakiki anavyoihakiki kazi yake. Kila mwana jamii ni vyema kupata matibabu sahihi. Kutokana na hayo, yatakikana pawe na hospitali na waganga wanaofaa wenye kiwango kwa kutibu wagonjwa katika njia stahiki, Pia, serikali iajiri na kutoa nafasi za kuelimisha vijana ili waweze kujitolea kwa moyo mkunjufu na waimani. Karama amefanikishakwa kiwango kikubwa juu ya suala hili, ameitaka jamii ya Wasadikika kutafuta mbinu za kupata huduma nzuri kwa wagonjwa ili kupunguza maradhi ya ovyo ovyo na vifo vilivyokithiri.

#### 4.6.5.9 Kuwepo kwa vyombo vya usafiri

Katika riwaya hii ya *Kusadikika*, mwandishi amemtumia Karama kupitia amni ambaye alikuwa mjumbe wa Ardhini, mjumbe huyu alisafiri kwa mangera ambaye ni ndege na kushuka chini baada ya kusafiri kwa chombo kiachoongozwa na watu, kufika katika Ardhi raia wa huko walistaajabu sana na kuahidi kuwa na waowatatengeneza chombo kinahopaa juu kwa kuongozwa na wao wenyewe kwa walivyofanikiwa kuunda marekebu ya kusafiria majini na magari ya kusafiria nchi kavu sasa wanataka chombo kinachopita hewani. Mtunzi anasema:

> "Amini alipowaambia kuwa alisafiri kuwa alisafiri kwa mangera kutoka Kusadikika aliajabiwa sana, alisifiwa kuwa alifanya jambo kubwa kwa kusafiri kwa chombo ambacho mwendo wake haukuwa kwenye uongozi wa kiumbe kama yeye, lakini wao watajaribu kufanyiza jambo lililokubwa sana kuliko like kwa kusafiri katika hewa kwa chombo ambacho mwendo wake utakuwa katika uongozi

> wao wenyewe. Ahadi ilitolewa na watu wa Ardhi kuwa watafanyiza yote waliyoweza mpaka hali ya kusafiri katika hewa ishinde kabisa. Amini aliwaacha katika matengenezo ya chombo cha kuwawezesha kuruka hewani, wakifanikiwa kutengeneza chombo walichokitaka watakuja huku. Walikwishafaulu kusafiri baharini kwa marekebu na barani kwa magari. Vyombo hivi viliweza kuchukuwa bidhaa nyingi nzito mbali na kwa wakati mfupi sana".(uk:40).

Kwa kuhusisha nadharia yaMwitiko wa Msomaji ni kwamba inalingana na mawazo ya mtunzi na namna mhakiki alivyoihakiki kazi yake. Kwani, kuwepo kwa vyombo vya usafiri ndani ya nchi hupelekea wepesi wa safari, masafa ya mbali huwa karibu jambo linalipelekea usitawi wa jamii na maendeleo ya nchi kwa ujumla. Kwa mfano,chombo kama ndege husaidia kwa usafiri wa angani, gari husaidia kwa usafiri wa nchi kavu na meli husaidia kwa usafiri wa ndani ya maji. Pia bidha zitasafirishwa kutoka eneo moja na lengine kwa urahisi kabisa. Karama ameisaidia jamii ya Wasadikika umuhimu wa kuwepo vyobo vya usafiri katika nchi ili vitowe matunda kwa jamii yao.

#### 4.6.5.10 Kuikomboa nchi kutokana na utabaka

Katika Kusadikika, utabaka umekuwa kama ndio dira ya viongozi wake. Tabaka la juu linawadharau na kuwanyanyasa watu wa tabaka tawaliwa. Kwa mfano, Majivuno akiwa kama kiwakilishi cha viongozi hao, anaonekana akileta dharau na kejeli kwa akina Karama. Hivyo, licha ya kuwa Karama ni tabaka la chini; dhaifu na dhalili kwa Majivuno na viongozi wenzake amefanikiwa kuikomboa nchi kutokana na uonevu huo. Kwa kuchambua nukta hii mtafiti ameona yafuatayo:-

#### 4.6.5.10.1 Kujitukuza na kujisifu kwa baadhi ya viongozi

Mwandishi wa riwaya ya *Kusadikika* amufaulu vya kutosha kuonesha watu kama hawa katika riwaya yake. Viongozi wanapenda zaidi kujikuza kwa sababu ya vyeo vyao na si kwa matendo yao. Hivyo, mtunzi amemchora Majivuno kama kiwakilishi wa viongozi wa aina hii Amesema:

> "Matendo ya mshatikwa yalipasa kukomeshwa wakati yalipoanza. Walakini kwa sababu ya tabia yangu njema, na saburi ambayo kila waziri lazima kuwa nayo, mashtaka haya sikuyaleta uwanjani hadi leo." (uk:3)

Kwa kuhusisha nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ni wazi kuwa inawiana kati ya mawazo ya msanii na namna msomaji alivyoichambua kazi yake kwa sababu mara nyingi katika jamii watu hujigamba na kujiona kutokana na nasabu zao au vyeo walivyojaliwa na Mola wao, jambo ambalo huleta utafauti baina yao na wengine. Pia, kwa ajili ya nasabu bora au cheo huona ndio wenye hadhi ya kufanya mambo yanayofaa katika jamii zao ilhali ni kinyume na mawazo yao.

#### 4.6.5.10.2 Kuepuka Kibri

Suala la kibri nalo limeelezwa katika riwaya hii, mwandishi anaonesha kuwa kibri ni hatari katika jamii na paliposheheni kadhwaya hii hapakosi mtetereko wala hakuna liwalo kiusahihi, kila kitu kinakwenda ovyo ovyo hapana liwalo wala liendalo. Kutokana na hayo,yamethibitishwa kupitia Majivuno ambaye ni waziri mwenye kibri cha hali ya juu kabisa. Mwandishi anasema:

> "Majivuno, mtu aliyejihesabu mwenyewe kuwa kidole chake kidogo kilikuwa na akili nyingi kuliko vichwa na miili ya Wasadikia wote ikiwekwa pamoja alikuwa amejifunga kwa kumtosa mshtakiwa katika bahari ya maangamizi" (uk:6)

Kwa kuhusisha naharia ya Mwitiko wa Msomaji ni kwamba kweli inakwenda sambamba kulingana na mawazo ya msanii na namna mhakiki anavyoihakiki kazi ya yake kwa sababu watu wengi katika jamii wametawaliwa na hali hujipamba kwa kibri na kujifanya kama hawahakosi kwa kitu. Pia, wakiishi na watu hujigamba na kujidai kama kwamba wamekamilika hali ya kuwa ndio wapungufu kuliko hao wanowafanyia kibri hicho. Kwa mfano, Majivuno kama alivyokwishaelezwa hapo awali. Kutokana na sifa yake hiyo, Karama alipambana nayo kwa kujitolea mbele ya Mfalme kwa kuzungumza yaliyosahihi juu utetezi wa wananchi, hadi ikathibitika kuwa kumbe akili zake ni bora kuliko Wasadikika wote. Hivyo walipokubali maoni yake na kufuata ushari wake nchi ilineemeka baada ya miaka kadhaa.

#### 4.6.5.10.3 Kutojiona bora

Kama ilivyo kawaida, riwaya ya *Kusadikika* haikurudi nyuma katika kueleza suala hili. Watu kama Majivno waliringa na kujiona ndio watu bora na wenye thamani kubwa kuliko Wasadikika wote kutokana na hali nzuri za kimaisha na utukufu wa serikali waliyokuwa wakiiongoza.Si hivyo tu wenye hadhi na kipaji cha kufanya mazuri na tabaka la juu tu, na sikwa watu wote. Mtunzi anathibitisha kwa kusema kuwa:-

> "Jalali Mfalme na madiwani wakuu, mtakumbuka kuwa tangu zamani matendo makubwa yoyote yaliamriwa na kutendwa kwa watu wenyenasaba bora kama wafalme na madiwani. Watuovyo kama alivyo mshtakiwa hawakuachiwa kujishughilisha na mambo yaliyo zaidi ya yale yaliyohusiana na maisha yao wao wenyewe tu. Kama wangaliamriwa kujishughulisha na mambo yapitayo vimo vyao kama mshtakiwa aonekanavyo kuwa ndilo kusudio lake, mabadiliko ya kuchukia yangalikuwako mara kwa mara katika nchi hii". (uk:3)

Kwa kuhusisha nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ni kwamba inawiana vyema ati ya mawazo ya mtunzi na namna mhakiki alivyoihakiki kazi yake kwani, watu wote duniani kote hudhani kuwa tabaka la juu ndio wenye hadhi na haki ya kutenda mema na wanaona kila wanalosema au kufanya ni haki hata kama litawaudhi wengine. Hali inayoleta misuguano baina ya pande hizo mbili.

#### 4.6.5.10.4 Kuepuka dharau na kejeli

Dharau na kejeli nayo pia imeshamiri katika riwaya iliyoteuliwa, watu kama Majivuno wamekithiri hali hii. Wanadharau wengine na kuwafanyia kejeli ati kwa sababu wao ni bora kwa cheo, wanadhani hawawezi tenda wema wowote mbele ya kaumu yao utokana na udhaifu wao, pia wapo chini ya mamlaka. Hivyo, wanadharauliwa mbele ya watu bila ya kujaliwa kuwa na wao wanauwezo wa kufanya kila linalowezekana. Karama kama kawaida yake hakuwa nyuma katika kutekeleza

Mwandishi anasema**:**

> "Mikono ya mshtakiwa ni mifupi kwa kutenda wema wowote".
> (uk:3)

Kwa kuhusisha nadharia tajwa ya Mwitiko wa Msamaji ni kuwa inaakisi hasa kwani, mara nyigi katika jamii tabaka tawala huwadharau tabaka tawaliwa, walio chini hata kimaisha huwadharau waliojuu wanajiona kama waliojipa wenyewe hadhi hiyo, hawajui kwamba aliyejaliwa kipato na aliyenyimwa wote waja wa Allah. Hivyo ni vyema kuishi kwa upendo kati ya hawa wawili na kuepushana vikwazo vya kutojaliana kwa sababu ya kihali au kihadhi ya serekali.

Katika kuangalia zaidi juu ya ukobozi wa kijamii, mtafiti pia amechunguza ukombozi wa wanawake na watoto. Ameona kuwa, watu hawa wanahaki nyingi ambazo wananyimwa katika jamii zao. Mfano, wanaonekana kama hawana haki ya kufanya lolote kwa famiia zao, ni watu duni wasioweza kitu, hawastahiki kuibua jambo litakaloinua jamii zao.

**4.6.5.11 Kuwakomboa wanawake na watoto**: Karama aliitaka jamii ya Kusadikika kujikita katika kuwakombowa wanawake na watoto kwa ujumla ili kuleta maendeleo yao. Hivyo kwa vile ni watu kama wengine ni yema kupata yote yanayowawajibikia kupata ili kuondoa tafauti baina yao na waaume. Watu hawa wana haki ya mambo yafuatayo:-

### 4.6.5.12 Haki ya kupata elimu

Kwa kawaida imezoweleka kuwa, elimu ni uwezo wa kuandika nakusoma ulichoandika au kilichoandikwa. Lakini hasa ni kuwa, elimu ni ufundi, ujuzi au fani ya kazi fulani ambayo mwanadamu anaweza kukabiliana nayo. Jamii ikielimika bila ya shaka hutoka katika ujinga na kupelekea maendeleo kwa sababu “elimu ni ufunguo wa maisha”. Maisha ya mwanadamu mwenye elimu yanakuwa rahisi zaidi na yenye matumaini mema ukilinganisha na yale ya mjinga asiye na elimu Mwanadamu mwenye elimu ataweza kutumia akili yake ipasavyo katika kujikwamua na matatizo yote yatakayomkabili. Mshtakiwa Karama alikusudia kuielimisha kwa kina jamii yake juu ya umuhimu wa elimu kwa watoto, ili watoto hao waondokane na janga la upofu, uziwi  na ujinga wa kutojua umuhimu wa elimu. Hivyo, Karama aliiasa jamii ya Wasadikika kuwa, iwapatie watoto elimu iliyomakini

itakayowafunza dhima zao kwa mujibu wa majukumu yao. Katika marejeleo ya Auni, mwanadishi anabainisha kuwa:

> "Tunazaa watoto wengi lakini hatuwalei kiungwana kwa kuwafunza kuzijua dhima zao katika dunia."(uk:31)

Kwa kurejelea nadharia yetu katika kipengele cha uwiano kati ya mtunzi na namna mhakiki alivyoihakiki kazi ni kuwa inalingana na nukuu hiyo kwa sababu, mtafiti amebaini kuwa Karama analenga kuwataka watu wa Kusadikika wawaelimishe watoto ili waijue elimu itakayowakomboa na kuwafanya waepukane na dhulma, udhalilishwaji, unyanyaswaji na uovu wanaotendewa dhidi ya serikali ya Majivuno na kaumu yake. Si hivyo tu kama ilivyobainishwa kuwa watoto ni taifa la kesho, Utakapomuelimisha mtoto huyo utakuwa umelimisha taifa bora la baadaye.Watoto waliobora niwale walioelimishwa na kuifanyia kazi elimu yao kulingana na mahitaji yao na familia zao.

**Jedwali na. 4.1: Muhutasari wa Dhamira za ukombozi katika riwaya ya Kusadikika**

| | Aina za dhamira | Dhamira |
|---|---|---|
| 1 | Ukombozi wa kififkra | Kufikiri mbinu za kukomboa, fikra ya kukomboa nchi, kutafuta mawazo ya wananchi, fikra ya kuanzisha elimu ya uanasheria na fikra za wajumbe. |
| 2 | Ukombozi wa kielimu | Umuhimu wa elimu, elimu ya uanasheria, elimu ya namna ya kuishi na watu, elimu ya kuondosha ubaguzi, kuwaelimisha wanawake na watoto, elimu ya kujenga urafiki na wengine na elimu ya kujikomboa kutokana na madhila. |
| 3 | Ukombozi wa kiuchumi | Kilimo bora, ufugaji, kufanya kazi kwa bidii, kuondosha uvivu na umaskini. |
| 4 | Ukombozi wa kisiasa | Namna ya kuendesha siasa bora, umiliki wa nchi, ulafi wa madaraka, kuondosha uhasama, fursa ya kujitetea, kuwatoa wafungwa, utetezi wa haki za binaadamu, kupunguza vifo, subra, uvumilivu, ushujaa, ujasiri , kutokata tama, kujitolea muhanga, uzaendo, kuondosha vita na chuki, kuwapenda raia na kuhubiri amani. |
| 5 | Ukombozi wa kijamii /kiutamaduni | Makazi bora, Maji safi na salama, umiliki wa mali, kuondosha ubadhirifu wa mali za umma, kuondosha chuki na uadui, kuepuka uchoyo, kuepuka uvivu, upapiaji wa mali, barabara, matibabu, vyombo vya usafiri, kujitukuza, kibri, kujiona na zarau na kejeli. |

**Chanzo: Data kutoka riwaya ya *Kusadikika* 2017**

### 4.6.6 Hitimisho

Kwa hakika katika riwaya ya*Kusadikika* dhamira kuu hasa iliyojitokeza ni ukombozi kwa sababu ndani ya riwaya hiyomumekithiri matukio kadhaa yasiyofaa ikiwemo utabaka,ukatili,ukosefu wa haki za binaadamu,ukosefu wa miundo mbinu,usaliti choyo,kiburi,wivu, ukandamizwaji na udumishwaji wa wananchi wa Kusadikika.

Hivyo muhusika Karama na wajumbe wake wote sita walikusudia kujikwamua katika makucha hayo ya kikatili yaliyosababishwa na tabaka tawala.Serikali ya Majivuno imejaa kibri, ujeuri, kejeli kwa jamii yake na haijali wala haina utu hata kidogo inafanya mambo yake kwa maslahi ya wachache tu imesahau kuwa wananchi ndio wenye kujenga nchi na maendeleo ya wananchi yanapatikana kwa kuwa na itifaki na wananchi au jamii husika.

## 4.7 Kubainisha Dhamira za Ukombozi katika riwaya ya Vuta N'kuvute

Katika *Vuta N'kuvute,* ukombozi uliojitokeza zaidi niukombozi wa kiutamaduni, kijamii, kisiasa, kifikra, kiuchumi na kielimu.

### 4.7.1 Ukombozi wa Kiutamaduni

Huu ni aina ya ukombozi wa kuepuka mila, desturi, silka, ukabila na mfano wa hayo katika zile tabia ambazo hazistahiki kwa mwanadamu kutenda au kutendewa. Aina hii ya ukombozi katika riwaya ya *Vuta N'kuvute* imekithiri zaidi wakati ambapo Yasmin ambaye aliyetoka kabila la Kihindi alikataa mila zakena kujiingiza katika utamaduni wa Waswahili bila ya kujali rangi, ukabila au sura za Waswahilihao.Mfano wa ukombozi wa Kiutamaduni umejitokeza katika maeneo yafuatayo:

#### 4.7.1.2 Kuvunja Ndoa yake kwa Bw.Raza

Mtafiti amebaini dhana ya kuvunja ndoa kupitia Yasmini ambaye ndiye aliyeozeshwa na wazazi wake,aliona kwamba kuishi na babu lililozeeka ni bora kukosa mume kuliko kuwa katika hali hiyo.Alifanya kila njia kuhakikisha anafanikisha kumtoroka,aliamua kukimbia usiku na kumuacha Raza akiwa katika majonzi na huzuni za kukosa mke wake kijana na mrembo. Mtunzi anasema:

> “Ulikuwa usiku wa kawaida tu, Bwana Raza keshakoga amejifunga kanga kiunoni,….“Unasemaje?”Aliuliza….”Kwani hukusikia?”. Naye Yasmin aliuliza,amekaa kwa maringo juu ya kiti,ameshika tama akimtazama Raza bila wasi wasi,pua ameikunja,mdomo ameufidua,jeuri ya kitoto inamwenda ndani ya damu yake.Bwana Raza akaona sasa maji yamezidi unga,hajui la kulifanya,Yasmin amechachamaa amekuja juu kama moto wa kifuu lakini naye akajikaza ikambidi aoneshe urijali wake.”Siku hizi umekua huna adabu”! “Zinauzwa wapi?…“Niwache au nitapiga kelele kama unataka kuniua mpaka majirani wote watoke madirishani”. …“Nani? Mimi? Unani…”.Kabla hakumaliza aliyotaka kuyasema Yasmini alitandikwa kofi kubwa vimurimuri kila rangi vikawa vinameremeta mbele ya macho yake…Unani………”Hajawahi kumaliza akachapwa kofi la pili,Yasmin alianguka juu ya kochikama mzigo anatweta kama mgonjwa wa pumu.Bwana Raza akili hana kichaa hana midomo inamtetemeka,maneno yamemkwama hayatoki kinywani.Alitaka kumnyanyua Yasmini pale alipoanguka, Yasmini alichomoka ghafla akakimbilia mlangoni akatimua mbio”.(uk:15-16)

Kwakuhusisha nadharia ya Mwitiko wa Msomaji katika kipengele cha uwiano baina ya mawazo ya mtunzi na namna muhakiki alivyoihakiki kazi yake ni kuwa yanalingana kwa kiasi kikubwa kwa sababu katikajamii halisi, jambo hili huonekana, Wako wanawake ambaoendapo watalazimishwa kuolewa na watu wasiowataka, migogoro haiachi katika nyumba hiyo. Mara nyengine husambaratishana na kuachana kabisa. Endapo wataishi hukosa amani na hupelekea kugombana hadikufikia kukimbiana.

### 4 .7.1.3 Kujiunga katika Ngoma za Waswahili

MuhusikaYasmini aliamua kuandamana na Waswahili katika starehe zao, alishiriki katika Usiku wa Jumamosi akishirikiana na Waswahili akiwemo Mwajuma,Salum na wengineo,kitendo ambacho kilikua ni marufuku kuchanganyika katika starehe kati ya Waswahili na Wahindi.Mwandishi anasema:

> “Kama Mwajuma na Yasmini nae aliondokea kuwa mshabiki wa kuingia taarab,ushabiki uliomfanya na yeye kuingia ndani ya kundi la wale wanaodiriki kufungua midomo yao wakaimba.Na yeye pia alijiunga na chama cha “Cheusi Dawa” Na ushoga wake na Mwajuma ukazidi kutia mizizi,Yasmini aliona vioja,vituko na mikasa,zogo na vurugu,raha na buraha.Tokea alipokua mtazamaji mpaka akawa mshiriki katika mambo yote yaliyomzunguka ndani ya nyumba ilemtaani pale.”(uk:56)

Sehemu nyengine zinazoonesha kuwa Yasmini alijihusisha na ngoma za Waswahili zinaonekana katika ukurasa wa 36,50 na 61.

Kwa kuhusisha nadharia ya Upokezi ni kwaba inaakisi mazingira halisi kwani, vijana wengi wanapenda anasa hivyo hujihusisha na ngoma zinazoonesha mitido mbali mbali licha ya kuwa nyengine hazitokani na tamaduni zao ilimradi kufurahisha nafsi zao tu. Mfano, asili ya ngoma za kizanzibari ni msewe, sindimba, taarabu na msondao. Lakini baadhi ya Wazanzibari hujihusisha na ngoma zisizokuwa zao kama bongo fleva n.k

#### 4.7.1.4 Kuwa na Marafiki Waswahili

Yasmini aliachana na mashoga wa kabila lake na kuungana na waswahili na kuwa swahiba zake walioishi na kupendana kama ndugu wa baba na mama. Mwajuma ambaye alikua ni Mswahili alifanya urafiki nae tokea Yasmini hajahamia Mombasa na ndio maana alipotoroka kwa mume wake na kurudi Zanzibar ilikua rahisi kupata mwenyeji wa kumsitiri. Mtunzi anathibitisha kwa kusema:

> “Ijapokua Yasmini alitumia muda wake mwingi dukani,lakini alipata muda wa kupanga ushoga na jirani yake Mwajuma.Mwajuma alikua ni msichana wa Kiafrika na tabia yake ya ucheshi na masihara ilimfanya Yasmin avunje miiko ya Kihindi ya kuingiliana na Waafrika”(uk:4)

#### 4.7.1.5 Kuhamia Uswahilini

Miongoni mwa mambo aliyoyafanya Yasmini ambayo yalikuwa hatakikani katika kabila la Kihindini kuhama katika utamaduni wa Kihindi na kuhamia katika utamaduni wa Waswahili ikiwa ni pamoja na makaazi ya Uswahilini.Marabaada ya kumtoroka mume wake kule Mombasana kuamua kurudi kwao Unguja,yaliyojiri kwa jamaa zake hasa ndio yaliyomfanya akhiari kuishi na Mwajuma kuliko kurudi kwa mume wake Bw.Raza. Hivyo aliishi na Waswahili hadi akazowea maisha yao na yakawa rahisi na yafuraha.Shafi anasema katika riwaya yake:

> "Miezi kadhaa ilipita, Yasmini alikua amezama katika maisha ya Uswahilini ambayo kidogo kidogo alianza kuyazoea,si kama aliyazoea maisha tu bali na Waswahili wenyewe vile vile".(uk:42)

Kwa kuhusisha nadharia tajwa katika kipengele cha uwiano baina ya mtunzi na namna mhakiki alivyoihakiki kaziyake ni kuwa, hata jamii zetu za kawaida wapo watu wanopenda kuhama katika familia zao na kujiunga na familia nyengine ama kwa kutafuta maisha au kujikwamua na matatizo yanayowakabili ndani ya jamii zao. Hivyo inaonesha kwaba si vibaya kuhamia popote mtu anapopenda ikiwa maslahi yake yatakuwa mazuri na salama.

#### 4.7.1.6 Dhamira ya Mapenzi na Ndoa

Mapenzi na ndoa ni katika msingi adhimu ya kuweza kufikia hatua ya ukombozi na maendeleo ya haraka. Mapenzi hujenga urafiki, huruma, masikilizano na matumaini mema katika maisha ya kila siku. Kwa upande wa ndoa huimarisha familia na kujenga jamii yenye mwamko na juhudi za kufikia maendeleo kutokana na usimamizi mwema.

**4.7.1.6.1 Mapenzi:** Mtafiti amebaini kuwa yametandawaa katika riwaya ya *Vuta N'kuvute*. Mtunzi amemchora Yasmin ambaye alikuwa na mapenzi ya hali ya juu ya vijana wa Kiswahili kuliko watu wa ukoo wake wa Wahindi ambao ndio wa kabila lake la Ithnaashiria. Kwa misingi hiyo Yasmini alijikomboa kutoka katika makucha ya Kihindi licha ya kuwa yeye alikuwa ni mtoto wa Kihindi. Kwa mintarafu wa hayo Yasmini aliamua kumpenda Denge ambaye alikuwa Muafrika halisi na kuwa karibu naye kwa kila jambo. Hili lilimfanya Yasmin akamatwe na Koplo Matata na Inspekta Wright na kuwekwa kizuizini kwa lengo la kutakikana atoe taarifa za Denge.Hayo yanadhihirika kupitia ukurasawa 88,89 na ukurasa wa 96 hadi100.Mwandishi anasema:

> "Saa tano za usiku Yasmin alijikuta amewekwa katikatibaina ya Koplo Matata na Inspekta Wright wote wawili wakimtazama kama aliyeua.Yasmin hakujua ovu alilolitenda hata ikabidi akamatwe na polisi …" "...wakati Yasmin amezama katika mawazo ya Inspekta Wright aliita kwa ghafla "Koplo kwenda leta ile file" ndio afandi". Koplo Matata alitoka kwa haraka sana na kiasi cha kufumba na kufumbua alirudi na jalada mkononi na kumkabidhi Inspekta Wright…" "…Sasa tunataka ufanye jambo moja, "Koplo Matata aliendelea. "Kama Denge unamjua tunataka umjue zaidi,uzidishe uhusiano naye kiasi ambacho atakukinai na kukueleza nyendo zake zote,halafu kila atakalokwambia likiwa zuri au baya uje uniarifu.Hiyo ndio njia pekee itakayokunusurisha tusikurudishe kwa muumeo.Unasemaje?"(uk:96-100)

> "Yasmin aliinamia chini akawaza, akainua kichwa chake kumtizama Bukheti akamwambia, "Sikiliza Bukheti nimeolewa nikamkimbia mume wangu kwa kufanya hivyo nikahasimiana na wazazi wangu.Nimempenda Denge ili awe mume wangu hajawahi ila nimezaa naye akawa baba watoto wangu kwa kitendo hicho nimelaaniwa na jamaa zangu,nimeolewa tena bila ya idhini ya wazazi wangu mume wangu kafa hata ndoa haikuchangamka moyoni mwangu,mara tu baada ya mume wangu kufa Denge niliempenda, nikategemea kuishi naye akachukuliwa,si wangu hapa nilipo niko hohe hahe sina mbele sina nyuma,siko kwake siko kwangu nadhani nataabishwa na radhi za wazaziwangu"(uk:231)

Kwa kurejelea nadharia ya Upokezi mtafiti amedhihirisha kwa uwazi kuwa kuna uwiano kati ya maana inayosomwa na jinsi msomaji anavyohakiki kwani hata ndani ya jamii halisi muna watu wenye kupendana na kuzoweana vilivyo kiasi ambacho mmoja anaweza hata kutoroka nyumbani kwao na kumfuata mwenzake kutokana na uhalisia wa maisha ya mapenzi baina yao.

**4.7.1.6.2 Ndoa:** Yasmini alikubali kuolewa na Waswahili hali ambayo ilikuwa ishara tosha inayoonesha kuwa muhusika huyu alikomboka.Mfano, aliolewa na Shihaab na baada ya kifo chake Yasmini aliolewa na Bukheti ambaye pia alikuwa Mswahili.Mtunzi anasema:

> "Kufa kufaana, Shihab kafa harusi ya Bukheti inanukia, Yasmin anajua kwamba hakuna amuwezae mjomba wake isipokua Kermali".

Kwa kuhusisha nadharia ya Mwitiko wa Msomaji, mtafiti amedhihirisha ya kwamba kila kazi ya fasihi inamaana kulingana na msomaji binafsi na jinsi anavyoichukulia. Kwa sababu kitendo cha Yasmin kukubali kuolewa ni Waswahili na kukataa kuolewa ni wahindi ambao ni katika kabila lake kimedhihirisha hasa kuwa ni kikomboleo cha maisha yake na kuonesha kwamba inawezekana kwa mtu yoyote kuchanganyika kindoa na kuishi kama kwamba munatoka katika kabila au taifa moja, hakuna ulazima wa kuangalia ukabila isipokuwa kitu muhimu hasa ni kuangalia maslahi, maelewano, heshima na kuthaminiana juu ya ndoa hiyo.

### 4.7.2 Ukombozi wa Kisiasa

Ukombozihuu umeonekana kupitia kwa Denge ambaye ndiye kiongozi wa kudai uhuru, akishirikiana na wananchi wengine akiwemo Chande, Pazi, Mambo, Sukutua, Mwajuma wanaharakati wengineo wanaounda kundi la wapigania uhuru linaloitwa “Lipua” Hawa wameonekana wakidai uhuru wao wa nchi kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo vipeperushi. Walieneza makaratasi hayo kila pembe,mfano Mahonda, Dar es Salaam, Pemba n.k. Jambo hili lilimfanya Inspekta Wright kupata taharuki na “Lipua” walidiriki hadi kumbandikia kwenye kioo cha gari yake.Mtunzi amesema:

> “Inspekta Wright alikuwa amekaa ofisini mwake kama mwehu,simu zinalia mtindo mmoja, akiwacha hii inalia hii na mara nyengine simu zote mbili zinalia kwa pamoja ikawa hajui aisikilize ipi.Alikuwa amebabaika kuitumbulia macho hajui afanye nini kwani alikuwa na hakika yatakuwa yale yale.Akainua ule mkono wa simu taratibu kama mtu aliyechoka sana “Haloooo”aliitika kwa sauti ya mtu aliyekata tamaa. “Afandi!” iliita sauti katika simu, “naongea kutoka kituo cha polisi cha Mahonda.Mahonda nzima imebandikwa karatasi za kudai uhuru,haijulikani nani aliyefanya kazi hiyo”. (uk:188-189)

.kumjuilishaMambo ambaye ni mshabiki mwenzake ya kuwa anataka kuyasambaza makaratasi hadi Pemba, hivyo anamtaka Mambo ayachukue makaratasi hayo na kuyapeleka melini kwa lengo la kufika Pemba.

#### 4.7.2.1 Subra na Uvumilivu

Subra na uvumilivu ni miongoni mwa nyenzo muhimu katika kufikia mafanikio. Msanii amewatumia wahusika kadhaa katika riwaya yake ya *Vuta N’kuvute* ambao wamekuwa na subra na uvumilivu.Mfano Denge,aliitwa majina yasiyofaa kama msaliti,komunisti hadi kufikia kukamatwa na kufungwa mara kadha lakini hakurudi

nyuma katika kupambana na utafutaji wa uhuru akishirikiana na wafuasi wake akiwemo Mambo na Chande na kundi lao la Lipua. Hata walipoingiza makaratasi walikamatwa na kuhukumiwa kifungo cha miaka mitatu jela.Msanii anasema:

> “Siku ya pili walipelekwa mahakamani kila mmoja kahukumiwa kifungo cha miaka mitatu na kazi ngumu,usiku Inspekta Wright alisherehekea ushindi wake English Club kwa kunywa pombe akijisifu na kujigamba mbele ya wenzake kama kwamba amefanikiwa kwelikulizuia wimbi la mapambano ya kupigania uhuru visiwani Zanzibari.Lakini sivyo kabisa,kufungwa kwaDenge na Chande kulikuwa kama cheche iliyosababisha moto mbugani,wanasiasa walipiga kelele majukwaani,wananchi wakalaani ukoloni”(uk:227)

Mtafiti kwa kurejelea nadharia ya mwitiko wa msomaji ameona fika kuwa dhamira ya subra na uvumilivu inalingana  na mawazo aliyokusudia, kwa sababu pahala popote pale panapotafutwa ukombozi au maendeleo, subra na uvumilivu ni katika misingi ya maendeleo hayo,mtunzi anaielimisha jamii kujipamba na tabia hii subra na uvumilivu wakati wanapohitaji mabadiliko ya aina yoyote.

#### 4.7.2.2 Kujitolea Muhanga

Kujitolea muhanga ni dhana ya kuwa tayari kukubali lolote linaloweza kumfika mhusika  (jema au baya), bila ya kutetereka au kuhofia hata kifo.Kujitolea muhanga kumekuwa ni miongoni mwa hazina muhimu ya kupatikana kwa ukombozi katika jamii. Mtafiti amebaini kuwa Denge alionafika kuwa muhusika huyu alijitoa muhanga kwa ajili ya nchi yake.Denge alijua kuwa kwa vile yeye si kiongozi wa nchi,hana silaha yoyote ya kumsaida itakuwa vigumu kupigania uhuru wa nchi na kuupata kama alivyotarajia,lakini alikhiari kukosa kazi na kuteswa kuliko kuwa kibaraka wa nchi hiyo.Pamoja na hayo aliteswa na kukandamizwa ila aliona kuwa litakalokuwa naliwe na yeye yuko tayari kwa lolote litakalotokea. Denge alitiwa

gerezani mara kadhaa na kufanyiwa vitendo visivyofaa kama kuvuliwa nguo na kubaki uchi na kufanyiwa vitisho vingi ili asiendelee na mapambano lakini hakukubali wala hakujali kabisa.Mtunzi anasema baada ya Denge kufikishwa gereani:

> “Wale askari kanzu walitoka na lile lango likafungwa. “Vua nguo”.Askari mmoja alimuarisha Denge.Denge alishangaa kwani hakuwa na nguo ya kuivua.Alikuwa kama aliuepigwa na bumbuazi anamtazama yule askari. “Nakwambia vua nguo”, aliamrisha tena yule askari.Denge ikambidi aitii ile amri,akavua chupi na kubaki uchi.Yule askari alimgeuza na kumuamrisha.”Vaa nguo”.(uk:191)

Kwa kuhusisha na nadharia teule ya Mwitiko wa Msomaji, ni wazi kuwa kila kazi ya fasihi ina maana kufuatana na msomaji binafsi  na jinsi anavyoichukulia kwa sababu kwa mujibu  wa  mtafiti ameona kwamba ipo haja kwa mwanaharakati wa ukombozi kujipinda na kujitolea muhanga kwa kuwa tayari kwa yote yatakayoweza kutokezea kwani wanaweza hata kuondoshea heshima na wakubwa, hivyo ni vyema kuzidisha muelekeo kwa kadiri anavyoweza ili wafuasi wake wasije wakavunjika moyo na kuacha kuendeleza harakati hizo.

**4.7.2.3 Umoja na Ushirikiano**

Umoja na mshikamano ndio kiu ya kufikia maendeleo, kwa sababu wanopigania watajipanga na kudhamiria mafanikio yao,hawatabagua rangi wala kabila.Yasmin hakuwa mswahili ila alishirikiana na wenzake katika mapambano, nae Bukheti hakuwa Mzanzibari ila alishirikiana na akina Mambo kumtorosha Denge. Mwandishi amewaonesha akina Bukheti wakishirikiana katika kumkimbiza Denge ili asikamatwe na polisi. Anasema:

> “Jumapilijioni tunapakia embe na machungwa jahazini,”alieleza Bukheti.“Jahazi lenyewe linaitwa Komamanga,lishike vizuri hilo jina Mambo. Komamanga”, “Wewe endelea tu sote tunalijua Komamanga,’ alisema Mambo.“Mimi na Yasmin tutaingia jahazini siku ya Jumatatu alfajiri.Jahazi litatweka kuelekea Kusini kama linakwenda Dar es salam. Litatua Tanga nje kidogo, halitatosa nanga litakuwa likielekea mpera mpera mpaka mtakapofika nyinyi na Denge akishaingia tu mimi na Yasmin tutashuka, jahazi litatweka ya hom, safari ya Kismayu.” Bukheti alimtazama Mambo na kumuliza, “Unasemaje?”.Shabash Bwana Badi!” alisema Mambo amefurahi.“Nahodha Fikirini anaelewa kila kitu na huko Kismayu, Denge atafikia kwa rafiki zake huyo nahodha.”(uk:262)

Mtafiti akihusisha na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji mtafiti anaamini kuwa kuna wasomaji ambao husoma na kufasiri kazi za fasihi vizuri kuliko wengine kwa sababu alivyofasili yeye huwenda ikawa bora au kinyume chake kwani kila mhakiki ana mawazo yake binafsi wala hakuna wa kumzuia kutoa uchambuzi alioweza kuutoa katika kazi yake. Kwa upande wa mtafiti, ameona kuwa umoja na ushirikiano ni nyenzo hasa ya maendeleo kwa jamii,hivyo ni vyema katika maendeleo watu wote kuwa kitu kimoja na kuonekana na usaliti miongoni mwao,wasiwe wengine wavuta huku na wengine kule wakubaliane na washirikiane kabla yakutenda jambo husika.

#### 4.7.2.4 Kutokata Tamaa

Kutokata tamaa nayo ni dhamira yenye mchango mkubwa katika kufikia hatua ya ukombozi, katika riwaya *Vuta n’kuvute*kunawahusika waliokuwa washabiki wakubwa katika kazi zao, hawakukata tamaa kwa lengo la kutafuta mafanikio ya nchi yao. Mfano Denge na wenzake walitumia juhudi zote na hawakuwa radhi kuona wengine miongoni mwao wakikata tamaa na kuacha kupambana na wakoloni kwa hali zote. Mfano, Denge alishirikiana na wenzake wakaharibu katika vilabu vya starehe. Msanii anasema:

> **“**Wahuni wale walilala ndani muda wa siku mbili na siku ya tatu walifikishwa Mahakamani kwa kosa la kufanya fujo ilisababisha hasara kubwa hapo Karimjee Club” (uk: 138).

Mtafiti akihusisha na nadharia teule ya Mwitiko wa Msomaji ameona kuwa kuna uwiano mkubwa kati ya maana inayosomwa na jinsi msomaji anavyoihakiki wakati ambapo, wahusika kadhaa walionesha matendo yanayowiana na jamii husika,hadi sasa wako wasiokata tamaa katika kutafuta maendeleo hata kama watakuwa katika matatizo,huzidi kukaza kamba na kuwa  kufanya kila hila zinazowezekana hadi kufikia suluhisho linalotakikana.

#### 4.7.2.5 Juhudi na Bidii katika Kazi

Juhudi na Bidii katika kazini dhamira ambazo zinaonekana katika riwaya ya *Vuta N’kuvute*, wahusika wengi wamejitahidi katika matendo yao.  Mfano Yasmin alifanya juudi zote hadi akafanikisha kumtoroka mume wake Bwana Raza, Mwajuma alikuwa na juhudi ya kujikimu kwa sababu aliishi akiwa mbali na wazazi wake. Kwa upande mwengine Denge na kaumu yake walifanya hila zote katika kupambana na wakoloni na vijibwa vyao.Mfano alifanikisha kuandika vipeperushi vinavyohusu habari za kuwakashifu wakoloni na kuvieneza maeneo tafauti na kila sehemu au pembe ya Tanzania hasa Unguja na Pemba na nchi za nje. Mwandishi anasema:

> “Unaandika nini?” aliuliza.Habari! Habari gani? Habari za kuwakashifu wakoloni wa Kiingereza na vibaraka wao jinsi wanavyowatesa wananchi, sio Zanzibari tu Afrika nzima”.Sasa unamuandikia nani habari hizo?”Habari hizi nazipeleka gazeti moja nchi za nje”. (uk:120-121)

Mtafiti akihusisha na nadharia teule ya Mwitiko wa Msomaji  ameona kwamba inatoa maana yenye kuwiyana kimaana baina ya msomaji na jinsi alivyoihakiki kwa

sababu, kwa mujibu wa mtafiti alivyosoma amedhihirisha ya kwamba juhudi na bidii katika kazi ni kiwakilishi tosha cha mabadiliko katika jamii. Wahusika wote waliofanisha mahitaji yao katika riwaya hii, kitu cha mwanzo kabisa walichofanya ni kuwa nabidii mpaka kufikia kikomo cha ukombozi.

#### 4.7.2.6 Ushujaa na Ujasiri

Ushujaa na Ujasiri ni miongoni mwa dhamira ambazo zina mchango katika kufanikisha vyema ukombozi katika jamii. Dhamira hizi zimeonekana katika riwaya hii teule ya *Vuta Nkuvute*. Kwa mfano muhusika Denge na kundi lake la Lipua walikua mashujaa na majasiri wasioogopa wala kutishika katika kupambana na wakoloni. Waliingia ndani ya vilabu vya wakoloni kikiwemo Karimjee Club na kufanya uharibifu wakati wakoloni wakiwakatika starehe zao. Si hivyo tu, walifanikisha kuingia katika nyumba ya Inspekta Wright na kuharibu kila kitu, jambo lililopelekea mshtuko mkubwa kwa Inpekta Wright Mwandishi anasema:

> “Ndani ya nyumba hiyo, vitu vilikuwa vimechafuliwa na vitabu vilivyokuwa kwenye maktaba kwenye chumba cha kupumzikia vilitupwa na kutawanywa chumba kizima,alikwenda kwenye rafu ambayo huweka majalada yenye nyaraka zake muhimu na aliyakuta majalada yake yamechafuliwa na baadhi ya nyaraka hazimo. Mke wa Inpekta Wright alibakia nje roho inampiga hajui kilichotokea. Inpekta Wright alijiona amekabiliwa na mtihani mkubwa…..”(uk:150)

Mtafiti akihusisha na nadharia ya mwitiko wa msomaji ameona inaendana mawazo yake kwa sababu mara nyingi mtu akiwa na sifa hizi mbili, hutisha na kuogopewa hata kama hana kisaidizi chochote cha kumsaidia. Kilichowasaidia Denge na kundi lake la Lipua ni ushujaa na ujasiri wao wa kutoogopa lolote kutoka katika tabaka tawala. Kundi hili waliamini kuwa vitu hivi ndio silaha kubwa ya kuwatetea dhidi ya

utawala huo usiofaa juu yao, utawala ambao ulikuwa ni kikwazo kikubwa kwa Waafrika.

**4.7.4.7 Uzalendo**

Dhamira ya Uzalendo nayo nikiwakilishi stahiki cha kupata ukombozi. Katika riwaya ya *Vuta N'kuvute* kitendo cha uzalendo kimeonekana maeneo tafauti na kwa wahusika kadhaa. Kwanza muhusika Denge alikuwa mzalendo na nchi yake kiasi ambacho alibahatika kupendwa na Yasmin ila yeye alijikita zaidi katika siasa ya nchi kuliko binti huyu. Vilevile muhusika Denge na kundi lake la Lipua ndio walifanya kila hila kwa wakoloni na kuwafanyia vitimbi baada ya kuona kwamba wakoloni hao wamekuwa usumbufu mkubwa kwao. Mtafiti ameona kuwa Denge alisoma Urusina pengine angaliishi huko ingekuwa rahisi kupata ajira katika nchi hiyo na kuwa tajiri lakini kwa bahati njema aliona bora arudi kwao Afrika kwa lengo la kusaidia jamii yake na kuipapatua ndani ya mateso ya wakoloni.Kwa hiari yake alishirikiana na vikundi vya wanaharakati ndani na nje ya Zanzibar kwa ajili ya kuunganisha watu watakaomsaidia kutetea hadhi ya nchi yake ambayo ilikwishatawaliwa na wakoloni hao.Juu ya utetezi huo wa nchi yake aliokuwa nao,alipatavikwazo vingi katika harakati hizo na nyingi zilisababishwa na waafrika wenyewe.Hawa walikuwa wasalitiwa nchi yao.Mfano nzuri wa wasaliti hao ni Koplo Matata aliekhiari wageni waonevu kuliko jamaa zake. Pia alimuhatarishia Denge maisha yake kwa kumpa Yasmin makaratasi ya hatari akaweke kwa Denge ili iyonekane kama yeye ndie aliyachapisha akamatwe na kuteswa ila Yasmin alimuonesha Denge na kumpa habari kuwa alipewa ni Koplo Matata. Hivyo dhamiri yake haikuwa kama alivyotarajia.Kwa kuongezea kijana huyu alifika hadi kuwa na nambari ya simu ya

Polisi ambayo alipewa na Yasmin na akiitumia kwa kuwadanganya wakuu wa nchi yake.Mwandishi anathibitisha hayo kwa kusema:

> “Mimi nazungumza kwa niaba ya kikundi kinachoitwa Lipua. Juzi tulilipua Karimjee Club na ule ulikuwa mwanzo tu,sasa tutalipua English Club siku yoyote”.Denge aliweka simu chini na kwenda zake”(uk:147)

Mtafiti kwa kurejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ni kuwa ametumia kigezo cha kusoma matini ya riwaya hiyo na ndio iliyompa mwelekeo na kujua kuwa kumbe hata katika mazingira halisi kuna watu ambao wanajali zaidi maslahi ya wengi kuliko maslahi yao binafsi na hivi ndivyo inavyotakiwa hasa kwa lengo la kufanikisha mahitaji ya jamii.

**4.7.2.8 Utetezi wa Haki za Jamii**

Katika riwaya hii pia, wamo wahusika wanaotetea jamii zao kutokana na mateso yanayowakabili.Mfano mzuri ni Denge na kikundi chake hawakukubali manyanyaso yaliyosababishwa na kikundi kidogo cha watu waliokosa tone la imaani na hisani dhidi ya waafrika. Mtunzi amesema:

> “Unaandika nini?” aliuliza.Habari! Habari gani? Habari za kuwakashifu wakoloni wa Kiingereza na vibaraka wao jinsi wanavyowatesa wananchi, sio Zanzibar tu Afrika nzima”.Sasa unamuandikia nani habari hizo?”Habari hizi nazipeleka gazeti moja nchi za nje”.(uk:120-121)

Kwa kuhusisha nadharia ya Upokezi, mtafiti amethibitisha ya kwamba kuna uwiano mkubwa kati ya maana inayosomwa na jinsi msomaji alivyoihakiki kwa sababu anapoileta katika jamii halisi Denge alitetea haki za raia hadi akajiunga na

wafanyakazi katika maandamano dhidi ya unyanyaswaji licha ya kuwa yeye hakuwa mfanyakazi wa serikali.

### 4.7.3 Ukombozi wa Kifikra

Ukombozi huu umejitokeza katika riwaya hii ya *Vuta Nkuvute* nao umekithiri katika sehemu nyingi na ndio maana ikafikia hadi kila mmoja akajua hali inayomkabili. Kuna seheu kadhaa ndani ya riwaya hii zilizoonesha aina hii ya ukombozi miongoni mwao ni kama zinazofuata:-

#### 4.7.3.1 Kufikiri mbinu za kujikomboa

Yasmin alitambua jinsi alivyoonewa na wazazi wake kwa kuozesha babu asiyelingana naye badala ya kupewa kijana saizi yake watakaoweza kufurahishana na kupendana na kila mmoja kati yao akalionesha pendolake kwa mwenzake katika hali ya kuridhiana, lakini ilimradi tu babu huyu ametoka katika kabila lake. Hivyo alifikiri akaona kwamba jambo litakalomsaidia kujikwamua na hali hiyo ni kumkimbia hata kama atatengwa na ukoo wake.Ushadi umeainishwa katika kiengele cha kiutamaduni.

Kwa kuhusisha nadharia Mwitiko wa Msomaji ni kwamba ingawa kukimbia matatizo sio njia ya kuepuka matatizo, wakati wengine hepuka yakaondoka kabisa ila hilo huwa ni nadratu, si vyema kwa mwanajamii kuikimbia jamii yake ili kujikomboa kutokana na masaibu yanayomkabili, ama ikibidi kufanya hivyo hapana kizuizi. Yasmini alibahatika kuepukana na Bwana Raza ila kwa bahati mbaya alifukuzwa na utengwa katika familia yake kwa sababu waliamini kuwa aliwatia aibu kubwa isio mithilika.

**4.7.3.2 Fikra ya kujitambua na kujielewa:** Katika riwaya Tajwa anaonekana yasmini akiwa anajielea na kujifahamu kuwa ni nani na anapaswa kuolewa na nani, hiyo ilikuwa kikwazo kikubwa kwa kijana huyu kuolewa na tu anaejukuu badala ya kuolewa na kijana aliyelingana naye kwani alitarajia kuwa na mume wa aina hiyo ila kwa bahati mbaya haikuwezekana kutokana na mila finyu zilizozama ndani ya jamii yake. Mtunzi anasema kuwa:

> "Yasmini hakupenda hata kidogo kuolewa na mume kama yule, kwani yeye mwenyewe alipendelea sana kupata mume kijana kama yeye mwenyewe.Alipenda ampate mume ambaye yeyote aliyemwona angelisema "Kweli Yasmin kapata mume."Alikua anatamani kupenda lakini hakupata wa kumpenda.Yeye alitaka kijana wa makamu yake ambaye angelimuonesha pendo na yeye angelimmiminia pendo lote alilokuwa nalo moyoni mwake."(uk:1)

Kwa kuhusisha nadharia tajwa ni kuwa ni vyema kwa mwana jamii kujielewa kwanza kwani haitakuwa kikwazo kubadilisha mawazo yake kwa wana msimamo bora na imara akaolewa na katika kujikomboa. Yasmini ni mfano nzuri kwani mwisho wa siku akifanikiwa kuolea ni aliempenda tena kwa kuridhiwa ni jamaa zake.

**4.7.3.3 Fikra za kuchoshwa na nyendo zisizofaa:** Mfumo mzima waliokuwa wakiishi jamaa zake Yasmin, alichoshwa na nyendo hizo za kung'ang'ania ukabila na kufuata mila za Waswahili. Hii ni kwa sababu kwake yeye Yasmini suala la utabaka halikua na maana yoyote bali ni kudumisha hadhi za binaadamu ilhali binaadamu wote ni ndugu na wameumbwa na Mungu mmoja.Kwa mujibu wa hayo aliweza kuchanganyika nao kwakuishi na kufanya kila kitu shirika.Mtunzi anayathibitisha hayo wakati Bukheti alipotaka posa kwa Yasmin ila alikua akiogopa

kwenda kwa wazazi wake kwani yeye si Muhindi alijua atakaliwa. Mwandishi anaweka wazi kwa kusema:

> “Yasmin popote penye jambo la kheri basi njia hufunguka”alisema Bukheti,sasa furaha yake imezidi, harusi inabisha hodi, “Tuombe Mungu wakubali,mana yake n’dokama nilivyokwambia,jamaa zako unawajua tena,wao mtu kama si Muhindi wanamuona ni kinyaa tu.” “Bukheti mtu ni mtu. Hakuna mtuna mtu kinyaa,wote ni watu walioumbwa na Mungu.Ikiwa wao hawatotaka kuelewa hivyo mimi nitawafahamisha,”Yasmin akieleza, “Ikiwa wao watakuangalia wewe kama Mswahili kinyaa kwanguwewe ni mtu,ikiwa wao watajiona bora kuliko wengine ati wao ni Wahindi,mimi nawaona wao ni watu kama watu wengine.”(uk:248)

Kwa kuhusisha nadharia teule katika kipengele cha uwiano uliopo baina ya mtunzi na namna muhakiki alivyoihakiki kazi yake ni kuwa, kweli inkwenda sambamba na jamii husika kwa sababu ili kuokoa na kukomboa jamii, ni vyema kwa wana jamii kwanza kufikiri nyenzo za kuweza kukomboa na namna ya kupata wasaidizi wa ukombozi ili kupatamaendeleo kwa haraka iwezekanavyo. Ikiwa utavamia bila kufikiri itapelekea kukosa unachohitaji na kusababisha hata kuadhibiwa au kuteswa kabisa. Nae Denge alionesha fikra za mambo kadhaa. Miongoni mwao ni kama yafuatayo:-

#### 4.7.3.4 Kufikiria juu ya uongozi usiofaa

Kwa hakika Denge alikua kijana mweledi na mtambuzi wa mambo licha ya kuwa hakuwa mtu wa serikali. Alijua wazi kuwa uongozi uliopo haufai kutokana na vikwazo na mateso unaowafanyia watu wake. Denge kama raia wengine alikaa na kufiki uovu huo hadi akajua kuwa si hohote si lolote ila kufanya ila hila hadi kuhakikisha wanakwamuka na uongozi huo.Uthibitisho wa hayo umeonekana katika nukta ya ukombozi wa kisiasa.

Kwa kuhusisha nadharia teule katika kipengele cha uhusiano uliopo baia ya mtunzi na namna muhakiki alivyoihakiki kazi yake ni kuwa kweli inawiana kwa sababu ndani ya jamii husika, kwa kawaida huwana watu walio muamko mkubwa dhidi ya udhalilishwaji juu ya nchi yao ila huwa hawana madaraka wala nguvu za kufanya suluhisho kwa jambo hilo. Hivyo huzama katika mawazo na uchovu wa kiakili hafi kufikia muafaka wajambo hilo. Denge aliathirika na hilo akawa hana amani wala raha hata ya kuishi na watu vizuri. Mfano, pamoja na kupendwa ni Yasmini hadi kufikia kimpa mtoto hakua tayari kumuoa. Mwisho Yasmin aliolewani mtu mwengine.

**4.7.3.5 Kufikiri namna ya Kujikwamua kutoka katika Makucha ya Wakoloni**

Mtunzi wa riwaya hii pia alimtumia Denge kama kitambulisho cha watu wanaopambana na Wakoloni kwalengo la kuleta maendeleo. Hivyo alifikiria ni jinsi gani ataweza kujikwamua dhidi ya udhalilishwaji wa Wakoloni. Kwa sababu hiyo alifanikisha kutafita njia muafaka na kufikia kilele cha matarajio yake ingawa hakupata uhuru kamili baada ya hutiwa gerizani. Uthibitisho wa nukta ii nao ameshatangulia katika maeleze yaliyokwisha tajwa.

Kwa kuhusisha nadharia teule inaonekana fika kwamba inakwenda sambamba kwa sababu, kufikiri namna ya kufanyafanya jambo ni bora kuliko kulivamia. Kufikiri kutakufanya uwelewe yote yakayokukwaza katika harakati hizo na yatakayokusaidia katika kupeleka mbele gurudumu la maendeleo yako. Hii ni kwa sababu kiti chotechote ukikifanya kwa kufikiri mpangilio ni bora kuliko kukifanya kwa kukivamia kwani ufanisi utazidi na kupelekea kukomboa katika misingi inayostahiki.

### 4.7.4 Ukombozi wa Kiuchumi

Ukombozi wa kiuchumi umeonekana wakati ambapo Denge na wenzake wanadai uhuru, bila ya shaka yeyote kwamba miongoni mwa uhuru wanaouhitaji ni pamoja na uchumi wa nchi kwa sababu kila kitu kilihodhiwa na Wakoloni. Baadhi ya dhamira za kiuchumi ni kama zinavyofuata:-

**4.7.4.1 Uhuru wa Kutafuta Mali:** Muafrika akiwa hana hadhi ya kufanya lolote ndani ya nchi yake mwenyewe. Alionekana kama nyani tu asiye na wajibu wala haki ya kuchuma anachokihitaji. Hata katika starehe,Waafrika walikuwa hawathubutu kuingia katika starehe zao labda wale vibaraka tu. Kutokana na hayo ikawapo haja kubwa ya kutafuta ukombozi kwa Waafrika kwa kuvunja baadhi ya tabia zao kwa kutoa vipeperushi na mengineo. Pia Denge alishirikiana na wafanyakazi wakati wa maandamano. Mwandishi anasema:

> Wakati wa maandamano hayo,Denge alikuwa mstari wa mbele amekumbatia furushi la makaratasi aliyokuwa akiyagawa kwa mtu yoyote aliyemkurubia”(uk:139)

Kwa kuhusisha nadharia lengwa katika kipengele cha uhusiano baina ya mtunzi nanamna muhakiki alivyihakiki kazi yake ni kuwa inakubaliana vyema kwa sababu uchumi wa nchi unategemea wananchi na serikali yao, serikali ni wananchi, bila wananchi hapana serikali kwani itakosa waongozwaji ambao ndio watakaosimamiwa ili kunyanyua uchumi huo. Hivyo serikali kama serikali ni vyema kusimama wima kwa kuwashuhulikia raia wote wa nchi yake na sikwa kuangalia kabila ua ukoo wake tu kwani huo hautamuezesha kutanua uchumi wa nchi.

### 4.7.5 Ukombozi wa Kielimu

Ukombozi huu umepatikana kupitia kwa Denge kwa sababu yeye ndiye aliwapa elimu jamii yake ya Waswahili juu ya udhalilishwaji wa wakoloni dhidi yao. Kabla alikwenda kusoma Urusi na kufanikiwa vizuri kielimu ila kwa bahati mbaya aliporudi Zanzibari hakuajiriwa na alionekana kama mtu mbaya ambaye anataka kusababisha hatari katika nchi.Ikabidi aonekane mtu hatari na hivyo ikawa sasa anabandikwa majina yasiyofaa kama Komunisti na mengineo.Pamoja na vitimbi hivyo havikumchosha isipokuwa aliwaelimisha wenzake hadi wakafahamu athari iliyopo mbele.Mwisho wakajuwa ukweli nawakawa wa mwanzo kupigania uhuru wao.Mfano,akina Mwajuma mara ya mwanzo kuviona vikaratasi nyumbani mwake vilimfanya aghasike lakini mwisho wake yeye alishiriki vya kutosha katika mapambanona alikuwa mstari wa mbele hata katika kumtorosha Denge baada ya kutiwa gerezani.

atu ambao wanajali zaidi maslahi ya umma kuliko maslahi yao binafsi na hivi ndivyo inavyotakiwa hasa kwa lengo la kufanikisha mahitaji ya jamii.

#### 4.7.5.1 Dhamira ya Umuhimu wa Elimu

Kama inavyoelezewa katika *Vuta N'kuvute*, muhusikaDenge alisoma nje ya nchi - Urusi,akafanikisha vizuri katika masomo yake na ndio maana alipowasili nchini mwake aliweza kupigania uhuru wa nchi yake kirahisi,kwa sababu aliandika vipeperushi vyenye kupinga ukoloni na kuwashajihisha watu juu ya kupigania uhuru na kuondoa manyanyaso na dhulma kwa wananchi.Mwandishi anasema

> "Alikwisha jua kwamba karatasi hizo zimekwisha enea katika kila pembe ya kisiwa cha Unguja, Kaskazini mpaka Kusini, Mashariki mpaka Magharib, lakini sasa hivi alishangaa zaidi alipopekea simu kutoka mkoani ikimpasha habari hizo hizo,alikurupuka kutoka ofisini mwake kama mtu aliyepandwa na pepo akatoka kwa hasira kuelekea kwenye gari yake. Alipofungua mlango akakaa ndani ya gari aliikabili karatasi iliyoandikwa juu ya kioo cha mbele ya gari hiyo **"**kufa au kupona tunataka uhuru**"**

Kwa kuhusisha nadharia ya mwitiko wa msomaji, mtafiti ameona inawiyana kimaana kwa namna alivyoisoma na alivyoihakiki kwa sababu Denge kama vijana wengine katika jamii ameelimika na ndio akawa kiongozi jasiri na msomi wa kikundi chake cha Lipua. Watu walimuamini na kumpenda. Pia alikuwa kama kiungo kilichoaminika katika kazi aliyokuwanayo ya ukombozi wa taifa.

**Jedwali na. 4.2: Muhutasari wa dhamira za ukombozi katika riwaya ya *Vuta N'kuvute***

| | Aina ya ukombozi | Dhamira |
|---|---|---|
| 1 | Ukombozi wa kiutamaduni/ kijamii | Kuvunja ndoa, kujiunga katika ngoma za waswahili, kuwa na marafiki waswahili, kuhamia uswahilini na mapenzi. |
| 2 | Ukombozi wa kisiasa | Subra na uvumilivu, kujitolea muhanga, umoja na ushirikiano, kutokata tamaa, juhudi na bidii, ushujaa na ujasiri, uzalendo na utetezi wa haki za jamii. |
| 3 | Ukombozi wa kifikra | Kufikiri mbinu za kujikwamua, kujitambua na kujielewa, fikra ya kuchoshwa na nyendo za zisizofaa (za Wakoloni), kufikii juu ya uongozi usiofaa na kufikiri namna ya kujikwamua kutoka katika makucha ya Wakoloni. |
| 4 | Ukombozi wa kiuchumi | Uhuru wa kutafuta na kumiliki mali |
| 5 | Ukombozi wa kielimu | Umuhimu wa elimu. |

**Chanzo: Data katika riwaya ya Vuta N'kuvute 2017**

### 4.7.6 Hitimisho

Kwa kuhitimisha ni dhahiri kuwa, dhamira ya ukombozi iliyochambuliwa katika riwaya ya *Vuta N'kuvute* ni kama ilivyobainishwa katikariwaya ya *Kusadikika* kwa sababu inalenga zaidi katika kumkomboa mwanadamu katika mazingira yaliyomzunguka. Licha ya changamoto zilizowakabili wahusika wake katika harakati za kutafuta ukombozi walisimama wima kupambana na udhalilishwaji huo. Pia, walitafuta kila njia iliyowezekana kuhakikisha kuwa maendeleo ya nchi yanapatikana katika sekta zote zilizowazunguka juu ya maisha yao ya kila siku.

## 4.8 Kulinganisha na Kulinganua Dhamira ya Ukombozi katika ya *Kusadikika* na *Vuta N' Kuvute*

### 4.8.1 Kulinganisha

#### 4.8.1.1 Dhamira ya Juhudi na Bidii katika Kazi

Ni kufanya kazi katika hali ya juhudi na bidii zote ili lipatikane lengo linalohitajika. Katika fasihi linganishi mtafiti anaweza kulinganisha dhamira hii katika *Kusadikika* na *Vuta n'kuvute* kwa kuonesha kuwa wajumbe wa Kusadikika walikuwa na bidii na juhudi za hali ya juu katika kupambana na utafutaji wa ukweli, walitumia hila zao zote huku wakipata moyo wa kufaulu katika kazi hiyo. Msanii anasema:

> "Kila alipopata shida ndipo bidii yake ilipozidi kukua. Baadhi ya watu hulenga mioyo yao mbele ya dhiki lakini wengine hukana mpaka waishinda*"(Kusadikika uk:11)*

Ama katika *Vuta N'kuvute* ameonekana Denge na Zanga wakifanya bidii na jitihada zote ndani ya nyumba pamoja na mashaka yaliyomo humo ila

hayakuwakera, walitafuta mashine ya kuchapisha na wakafanikiwa kuitoa. Mtunzi anathibitisha kwa kusema kuwa:

> "Ndani ya nyumba waliyoingia hamkuwa na dalili ya kuishi mtu,mabuibui yametanda kila pembe na Denge alipoinua macho kutazama juu mandhari yake aliyoiyona ilikuwa ni mijusi iliyokuwa ikifukuzana,madirisha yalikuwa yamefungwa na hewa ndani mle inanuka vumbi.Aliyaangalia jinsi mabuibui yalivyojifuma na kusokotana yakatanda juu ya kuta za nyumba ile.Denge alishangaa hakuelewa safari yake ya kuja Dar es salam inahusiana na nini na kupelekwa ndani ya nyumba kama ile iliyokaa kama gofu lililokimbiwa kwa kuogapa wafu wanaoranda usiku kucha ndani ya gofu hilo.Walinyemelea na walipofika mbele kidogoZanga alifungua mlango mmoja wa vyumba vya nyumba ile,aliingia chumbani akafungua dirisha na nuru ya mchana ikatapakaa chumba kizima hewa ya kutoka nje ikapigana kikumbo na ile itokayo ndani kwa kugombea nafasi ya uwazi wa dirisha ya nje inataka kuingia na ya ndani inataka kutoka ugonvi wa hewa ukatifua vumbi chumba kizima.Denge na Zanga wakenda chafya kama wanaojifunza kunusa ugoro, nuru ile iliyojitawanya kwa marefu na mapana ndani ya chumba iliikatisha kwa ghafla faragha ya chumba kile ikakashifu uchafu uliokuwa umetawanyika pembe ya chumba.
> ”Ile pale” Zanga alionesha bado mpya kabisa imetumika labda miezi mitatu tu.Denge alinyatia akichukua hadhari asije akakanyaga chochote katika matakataka yaliyokuwemo mle akenda mpaka kwenye pembe ya chumba akauvua mfuko wa plastiki uliokuwa umefunika mashine ya kuchapishia makaratasi"(*Vuta n'kuvute uk:224)*

Hivyo Denge walifanikisha kuipata ile mashine aliyoitumia katika kuchapisha magazeti yatayowakashifu Wakoloni na vibaraka vyao.

#### 4.8.1.2 Uzalendo

Kitendo cha Uzalendo ndio kinaoneka katika riwaya teule. Katika fasihi linganishi mtafiti anaweza kuilinganisha nukta hii kwa kuonesha baadhi ya wahusika wa riwaya ya "*Kusadikika*" na "*Vuta N'kuvute*"ambao walikuwa na uzalendo na upendo wa hali ya juu kiasi ambacho hawakuthamini chochote walichopata zaidi ya kuafiki nchi yao.

Mfano katika *"Kusadikika"* muhusika Karama alikuwa uzalendo wa kutetea nchiyake. Vile vile wajumbe sita walifikia wakati wajitolea wenyewe wao bila kuchaguliwa mjumbe wa kwanza ni Burhani ambaye alijitolea mwenyewe kuwa ni mjumbe wa Kaskazini, wa pili Fadhili alijitolea kuwa ni mjumbe wa Mashariki, wa tatu ni Kabuli aliyejitolea kuwa mjumbe wa Kusuni, wa nne ni Auni aliyejitolea kuwa mjumbe wa Magharibi wa tano ni Radhaa aliyekuwa mjumbe wa Mbinguni na wasita ni Amiri aliyekuwa mjumbe wa Ardhini. Wote hao hawakujali mateso wala dhulma walizofanyiwa bali walikuwa na lengo la kumuunga mkono kiongozi aliyeaminika kuwa mkombozi wa uuma wa Wasadikika wote kwa upande wa vuta nikuvute pia wanaonekana wasuka kadhaa waliokuwa na uzalendo juu ya nchi yao.

Kwa upande wa *Vuta N'kuvute* Denge ni mfano mzuri wa wahusika aliyechorwa kama ni kijana mwenye uzalendo juu ya nchi yake. Nae Yasmini alikhiari awe msaliti wa koplo Matata ila ahakikishe anatoa siri na kumpa Denge. hata alipopewa vikaratasi vinavyoonesha mapinduzi ili akaviweke kwa Denge ati aonekane kuwa yeye ndie aliyeviandika alimuonesha Denge (uk:154) Mtunzi anasema:

> "Waliingia ndani na baada ya kuingia tu Yasmin alimkabidhi Denge yale makaratasi.Koplo Matata kanambia nije niyalete kwako lakini wewe usijuwe kama nimeyaleta" (uk:154)

Pamoja na kuwa Koplo Matata alikuwa Muafrika ila aliwasaliti Waafrika wenzake na kufuata Wakoloni kwa maslahi yake binafsi, jambo ambalo lilikuwa halipendezi na halifai katika jamii.

### 4.8.1.3 Umoja na Mshikamano

Nao unaonekana katika riwaya zote mbili, mtafiti anapolinganisha kupitia nadharia aliyoteuwa anaona wazi kuwa matendo mengi ya wahusika yalifanywa kwa kushirikiana bila utengano wa hali yoyote kiasi ambacho hata ulipo wadia wakati wa kutoroshwa kwa Denge katika gereza alishirikishwa hadi askari ambaye alikuwa ni mlinzi wa gereza hilo. Msanii anaonesha haya kupitia kwa Mambo ambaye alimpa Yasmini pakiti ya sigara na kutamka akampe askari baadaye ampe taarifa kuwa siku ya Jumatatu ni safari ya kumtorosha.

> Denge itakuwa tayari. Sasa Yasmini Mambo alisema "Wewe nenda kamuone yule bwana mpe paketi moja ya sigareti senti amwambie Denge siku ya Jumatatu mashua itamngoja Mbweni tushajua huko (uk: 24).

Nayo riwaya y*a Kusadikika* haikuwa nyuma juu ya dhamira hii, wajumbe walimuunga mkono Karama kwa ushirikiano wao waliokuwa nao, walijitolea wenyewe bila kutezwa nguvu wende katika nchi zinazostahhiki. Walikwenda na kurudi na ujumbe mzuri ambao unaaminika kwamba lau ingelikuwa unafuatwa na serekali ya Kusadikika mambo yangekuwa mazuri kwa muda mchache ila ilikuwa serekali ya vipofu wasioona mbele wala nyuma na viziwi wasiosikia wala kuhisi waliyokuwa wakiambiwa ni wajumbe hao. Mtunzi anathinbitisha kwa kusema kuwa:

> " Kwa hakika mafunzo ya Auni yalikuwa mema na yaliyoingika lakini yaliangukia katika masikio ya viziwi. Kusadikika itashukuru lini fadhila za watu wake bora." (uk:31)

### 4.8.1.4 Ushujaa na Ujasiri

Katika fasihi linganishi, mtafiti analinganisha dhamira hizi kupitia riwaya mbili alizoteua. Kwani zote zinaelezea suala hili.Mfano, katika Kusadikika dhamira hii inaonekena sehemu tafauti kila mjumbe kati ya hao sita na kiongozi wao walionesha ushujaa wa hali ya juu na ujasiri juu ya changamoto zilizowakabili.Mtunzi anasema:

> "Ushujaa ni husuni kubwa hazina bora ya kudumishwa.Ushujaa kwa mtu ni ngao kwa nchi ni tegemeo na kwa taifa ni uwezo jambo hili hukubaliana bila swali". (uk: 17)

Kwa upande wa *Vuta N'kuvute* wanaonekana akina Chande wakiwa majasiri na mashujaa wakubwa kwani walifanikisha kumtoa Denge katika gereza amabalo linalindwa ni askari, hivyo tendo kama hilo tujue ya kwamba hawezi kulifanya yoyote ambaye atakuwa na chembe ya woga.Msanii anasema:

> "Mashua inakaribia Sukutua ameikamata sukani anaongoza anaielekeza sawa sawa pale ilipo Komamanga. Denge amekaa upande mmoja wa mashua na Mambo upande wa pili Denge yuko vile vile na magwanda yake ya Gereza.Chande yuko wapi anauliza "Chande yuko gereza la Kinumoshi. Tutamtoa kama tulivyokutoa wewe" (uk: 273)

Hivyo wafuasi hao walimtorosha Denge na kuahidi kumtorosha Mambo kutoka katika makucha ya Wakoloni waliowakamata na kuwatia gerezani ili wasiendeleze harakati zao za kutafuta uhuru na ukombozi wa nchi yao.

### 4.8.1.5 Utetezi wa Haki za Binaadamu

Katika fasihi liganishi jambo hili linaonekanandani ya riwaya mbili zilizoteuliwa. Mfano katika *Kusadikika* kuna Karama na wajumbe wake lengo lao la lilikuwa ni

kujikomboa dhidi ya utawala mbaya uliokuwepo kwa sababu walikosa haki zao za msingi, licha ya kuwa waliadhibiwa na kubezwa hawakujali na walitaka kuwaonesha kuwa na wao wana haki kama binadamu wengine. Kwa bahati mbaya kilikuwa kikwazo kwa wajumbe, pia zinaonekana familia zao zikiyumba kwa shida na idhilali ya kukosa viungo vya majumba ambayo ni hao wajumbe sita. Msanii anaeleza kuwa:

> "Mbele ya umati huu Karama alitamka . "Baada ya kutenda yote waliyoweza kwa ajili ya nchi yao. Buruhani aliponzeka, Kabuli alihusudika na Fadhili akateswa mateso makubwa. Zawadi walizotumikiwa na nchi waliyoipenda zilikuwa ghera na adhabu tupu ingawa watu hawa wangalihai hata sasa lakini wake zao wamekwishaonja eda chungu na watoto wao wamepatwa na uyatima wa kusikitisha. Dhiki za nchi na misiba ya watu hawa ikiwemo pamoja hutosha kuifanya familia ya mashaka ya Kusadikika kama nusu moja ya maisha ya dunia mzima nchi moja yoyote ikipatikana na nusu moja ya mashaka ya dunia mzima ni mateso yaliyomakubwa kabisa" (uk: 25)

Mtafiti anaona kuwa kusudio hasa la mwandishi ni kulionya tabaka tawala kuwachana na udhalilishaji kwa binaadamu,viongozi wajue ya kwamba watu wote wana haki sawa wasionewe kwa kuwa kwao wanyonge ama kwa hali zao kuwa duni au kwa uaskini,kwani itapelekea kuwa wanyonge wa maisha na kuichukia serikali yao . Nae mwandishi wa riwaya ya Vuta n'kuvute anaeleza kukithiri kwa utabaka baina ya Wakaloni na Waswahili, Wakoloni walikuwa ni tabaka waliotawala Afrika na kuhodhi kila kitu na kulikuwa pia na tabaka la chini yaani tabaka tawalilwa lililoteswa.Tabaka hilo ni jamii za kiafrika ambazo ziliteswa kwa kupigwa,kuuliwa na kunyan'ganywa mali zao pia kuwaona kama vinyago tu. Hata katika starehe walijitenga na kila tabaka lilikuwa katika Club yake, si hivyo tu katika ndoa walioneka kama hawastahiki kuolewa ni Waafrika. Mfano,

Yasmini alipoolewa na Mswahili alitengwa na familia yake. Pamoja na hayo, kitendo cha Yasmin kumtoroka mume wake Bwana Raza alifukuzwa kabisa na familia yake yote ilimlaani. Msanii anayasema hayo kupitia kwa mjomba wa Yasmini kama inavyoonekena.

> “Kabla ya karamu aliyokuwa akiandaliwa haikuwa tayari, mlango uligongwa na alipokwenda kufunguwa alimkuta mjomba wake amemsimamia mbele. “Mbona upo hapa saa hizi umerudi lini?” mume wako yuko wapi? Yasmini hakujuwa ajibu lipi katika maswali aliyoulizwa. Alinyamaza kimya kama mtu aliyepigwa na bumbuwazi nakuuliza mume wako yuko wapi? aliuliza tena mjomba wa Yasmini. Yuko Mombasa mimi nimerudi. nimeshindwa kuishi naye unasemaje? umeshindwa kuishi naye Raza? mjomba wa Yasimin aliondoka pale mlangoni alipokuwa amesimama, aliingia ukumbini na kukaa juu ya kiti. “Enhe hebu nieleze vizuri” Yasmini aliinamisha uso chini hofu imejaa. “Mjomba kusema kweli thawabu mimi nimeshindwa kuishi na bwana Raza kwa hakika mimi sikumpenda wala sikumtaka nilikubali kuolewa naye kwa kukuridhieni nyinyi tu wazee wangu tu” . Kama hukuweza kuishi na Raza basi na sisi hatuna pa kukuweka mjomba ……….tena upesi tuondokee mbele yetu.” (*Vuta N’kuvute uk:18)*

Mwandishi alikusudia kuonesha kwamba kukosekana kwa haki za binaadamu kunasababisha kufanya mambo yasiyofaa katika jamii,hivyo ilijamii iishi kwa amani ni vyema kila mtu apate haki yake sawa,hii ni kwa sababu palipo na haki sawa na maisha yatakuwa mazuri na salama.

#### 4.8.1.7 Subra na Uvumilivu

Katika fasihi linganishi mambo hayo yanaonekana katika riwaya zote, wahusika wake walisubiria na kustahamili shida zote na dhiki walizopata juu ya harakati zao za kutafuta uhuru na kujikomboa katika makucha ya wakoloni. Mfano, Kusadikika wajumbe wote sita walivumilia na kustahamili masaibu yote waliyopata katika

kutafuta ushahidi juu ya kesi ya Karama, kutokana na uvumilivu wao walifanikisha hadi wakapata sulhu juu ya hilo.Mwandishi anasema:

> “Kila walipopata shida ndipo bidii yake ilipozidi kukua. Baadhi ya watu hulenga mioyo yao mbele ya dhiki lakini wengine hukana mpaka waishinda*”(Kusadikika uk:11)*

Kwa upande wa *Vuta N’kuvute*, wanaonekana wahusika waliopambana na Wakoloni na kutorudi nyuma licha ya vipingamizi walivyofanyiwa na Wakoloni hao. Mfano Denge na wenzake walitumia juhudi zote na hawakuwa radhi kuona wengine miongoni mwao wakirudi nyuma kwa kuacha kupambana na Wakoloni kwa hali zote. Mfano, Denge huyo huyo alishirikiana na wenzake wakaharibu baadhi ya vilabu vya Wakoloni kikiwemo klabu cha Karimjee yaani Karimjee Club.Kwa tendo hilo walikamatwa na kutiwa ndani wakalala siku tatu baadaye wakatolewa na kuendelea na harakati zao.Msanii anasema”

> “ Wahuni wale walilala ndani muda wa siku mbili na siku ya tatu walifikishwa Mahakamani kwa kosa la kufanya fujo ilisababisha hasara kubwa hapo Karimjee” Club (uk: 138)

Pia kila walipotiwa ndani na kutolewa ndipo walipozidi hamasa za kupambana na matatizo yaliyowakabili. Hii ni kwa sababu walitaka kuwang’oa hasa katika maeneo yao au nci yao kwa ujumla.

#### 4.8.1.7 Kutokata tamaa

Kwa kulinganisha kupitia fasihi linganishi mtafiti aliona nayo inalingana. Riwaya ya *Kusadkik*a ilithibika kuwa wajumbe walijitahidi iwezekanavyo katika kutafuta ushahidi, hakuna aliyerudi nyuma kutokana na masaibu aliyoyapata, kila mtu

akikutwa na matatizo ndipoalipozidi kusonga mbele na kutarajia mafanikio ya baadaye. Ushahidi wa nukta hii umeonekana katika nukta iliyopo juu.

Nae Denge na wenzake hawakukata tamaa kutokana na masaibu waliyoyapata dhidi ya kupigania uhuru wa nchi yao kwa kuondosha dhulma na uonevu uliosababishwa na Wakoloni, walikuwa na msimamo wa kutosha na kutumaini maendeleo mazuri ya baadaye.Mwandishi anaonesha vipeperushi vya wanahakati wa uhuru hao vinavyosema kuwa:

“Kufa au kupona tunataka uhuru”

**Jedwali na. 4.3: Muhutasari wa dhamira zilizofanana katika riwaya ya *Kusadikik*a na *Vuta N’kuvute***

| Na | ***Kusadikika*** | Mdafao | ***Vuta N’kuvute*** | Mdafao |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Juhudi na Bidii | 2 | Juhudi na Bidii | 1 |
| 2 | Uzalendo | 3 | Uzalendo | 4 |
| 3 | Umoja na Ushirikiano | 7 | Umoja na Ushirikiano | 4 |
| 4 | Ushujaa na Ujasiri | 3 | Ushujaa na Ujasiri | 2 |
| 5 | Utetezi wa Haki za Binaadamu | 1 | Utetezi wa haki za binaadamu | 1 |
| 6 | Subra na Uvumilivu | 4 | Subra na Uvumilivu | 5 |
| 7 | Kujitolea Muhanga | 2 | Kujitolea Muhanga. | 1 |

**Chanzo:Data kutoka *riwaya ya Kusadikika* na *Vuta N’kuvute***

## 4.9 Hitimisho

Kwa kuhitiisha ni kwamba, ingawa kuna tafauti kubwa kati ya dhamira ya ukombozi ulioelezewa katika “*Kusadikik*a” na “*Vuta N’kuvute*” lakini pia kuna uhuhsiano

uliojitokeza kati ya riwaya hizo mbili. Kwa mujibu wa mtafiti aliona kwamba, dhamira hasa iliyolingana zaidi ni dhamira yakisiasa wakati ambapo wahusia wote walikusudia zidi kupeleka mbele maendeleo ya wananchi na nchi zao.

## 4.10 Kutafautisha Dhamira katika Riwaya tajwa

Kuna tafauti nyingi zilizojitokeza katika riwaya tajwa. Mtafiti alipochambua kazi yake kupitia Fasihi Linanganishi aliona kwamba tafauti hizo zimekithiri kwa sababu za kiamzingira na namna watunzi hao walivyojaribu kuziumba kazi zao ili ziwe na mvuto kwa wasomi. Kwa mfano, katika dhamira ya kiuchumi; ndani ya "*Kusadikika*" mumezungumzwa kilimo, mifugo, n.k, lakini katika "*Vuta N'kuvute*" mumeelezwa juu ya uhuru wa mutafuta mali. Katika dhamira ya kiutamaduni ndani ya "*Kusadikika*"mumeoneshwa malezi, makazi n.k ila katika "*VutaN'kuvute*" muelezwa zaidi mapenzi na mdoa. Katika ukombozi wa kifikra ndani ya "*Kusadikika*" zaidi ni fikra za wajumbe, fikra ju ya kuanzishwa elimu ya uwana sharia n.k, katika "*Vuta N'kuvute*" ni fikra ya namna ya kujikwamu ktoka katika akucha ya Wakoloni n.k. Kwa uchambuzi zaidi mtafiti ataangalia baadhi ya nukta kama itakavyofuata hapo chini.

### 4.10.1 Dhamira ya elimu

Katika fasihi linganishi mtafiti anaweza kutafautisha dhamira hii kupitia riwaya mbili alizochagua kama ifuatavyo.Elimu hasa iliyozungamzwa katika "*Kusadikika*" ilikuwa elimu juu ya uanasheria wakati ambapo muhusika Karama ndiye aliyekuwa mtoaji wa elimu hiyo,kwavile muhusika huyu aliijua vyema elimu aliyokuja nayo ilikuwa rahisi kuijulisha kwa watu bila kukosea au kuwa na wasisi wa anachokisema.Kwa bahati mbaya, serikali ya Kusadikika na wananchiwake

walikuwa wagumu kuikubali na kuifuata, Mwisho ilifahamika kwa baraza nzima na hapo ndipo walipopata mafanikio ya nchi yao. Mwandishi anayasema haya kupitia kwa Karama kama ifuatavyo:

> "Uanasheria ni elimu juu ya hukumu kwa mujibu wa sheria".(uk:8)

Kwa upande mwengine muhusika Denge wa riwaya ya "*Vuta N'kuvute*" alitoa elimu juu ya udhalilishwaji waliokua wakitendewa ni wakoloni na namna ya kudai uhuru kwani yeye ndiye aliyekuwa kiongozi wa mapanbano dhidi ya Wakoloni. Alikuwa msomi aliyepata elimu Urusi na hivyo aliwaelimisha akina Mwajuma na Yasmin hadi wakaijuwa athari inayotokana na utawala huo uliodhalimu.Kutokana na sababu hiyo ni vyema kwa mwana maendeleo yoyote kujifunza kabla ya kuanza kuingia katika harakati kwani elimu ni ufunguo wa maisha. Mwandishi anathibitisha hayo kupitia kwa Denge kuwa aliandika maovu ya Wakoloni na kupeleka nchi za nje ili kudhihirisha umuhimu wa elimu aliyokuwa nayo.Anasema:

> "Unaandika nini?" aliuliza.Habari! Habari gani? Habari za kuwakashifu wakoloni wa Kiingereza na vibaraka wao jinsi wanavyowatesa wananchi,sio Zanzibar tu Afrika nzima".Sasa unamuandikia nani habari hizo?"Habari hizi nazipeleka gazeti moja nchi za nje".(uk:120-121)

**4.10.2 Upendo (mapenzi na ndoa)**

Katika fasihi linganishi,iko tafauti kubwa kati ya mapenzi yaliyozungumwa katika "*Kusadikika*" na "*Vuta N'kuvute*".Mapenzi ya"*Kusadikika*" hayakuwa ya kweli,watoto hawakupendwa ipasavyo wakalelewa katika misingi inayotakikana, wanawake nao hawakutuzwa kwa mtazamo chanya bali walikuwa kama kiburudisho

cha wanaume tu,ikwa wanabadilishwa kama nguo,hakuna mwanamke aliyedumu kwa mume wake zaidi ya kudhalilishwa au kuachwa kabisa. Mwandishi anasema

Katika "*Vuta N'kuvute*" mumetajwa mapenzi ya aina mbili amabyo ni mapeni ya kweli naya uongo.Mapenzi ya kweli zaidi yanaonekana kwa Yasmin ambaye alimpenda Denge hadi akapita kiasi ila Denge alikuwa na mapenzi ya uongo dhidi yake kwani aliona bora siasa kuliko kuwa nampenzi. Mapenzi mengine ya kweli yameonekana kwa Bwana Raza juu ya Yasmin kiasi ambacho alifikia hadi kumzaa mtoto anaeitwa Yasmin ili asimsahau tu.Pia, kuna mapenzi Shihab kwa Yasmin aliyempenda mpaka akafa kwa kihoro baada ya kuona ndege iliyoanguka akafikiria Yasmin naye yumo humo hali ya kuwa Yasmin alikuwa bado yuko Zanzibar.Nae Bukheti alimpenda kikwelikweli hadi ikabidi ahame Mombasa kwa kumfuata Yasmin na mwisho walioana na kuishi raha kwa kupendana.Kwa upande wa "*Kusadikika*", hakukuwa na mapenzi ya kweli kwani mtunzi anasema kuwa watu hasa matajiri walitumia mali vibaya,watoto hawakupata huduma za shule na wakukuwa na mwanamke aliyedumu katika ndoa.Mume leo akioa huyu na kesho kumuacha na kuoa mwengine ndio uliokuwa mtindo wa wana kusadikika.

### 4.10.3 Hekma na busara

Kwa mujibu wa fasihi linganishi, hakuna uhusiano wa dhamira hizi kati ya riwaya ya "*Kusadikika*" na "*Vuta N'kuvute*", Katika "*Kusadikik*a" wajumbe wakiogozwa na Karama walisifikana na tabia njema,walijua la kusema mbele za watu.Ni tafauti na wahusika wa "*Vuta N'kuvute*",wengi wao hawakuwa na busara.Mfano wazazi wa Yasmin hawakufanya kitendo cha busara walipomlazimisha Yasmin kuolewa ni mtu aliyemzidi umri ikapelekea Yasmin kukosa utulivu wa ndoa,

Bwana Raza hakutumia kauli yenye busara alipokuwa akizungumza na Yasmin ikapelekea Yasmin kumtoroka na kuja Zanzibar, mjomba wa Yasmin hakutumia busara kwa Yasmin ikapelekea Yasmin kutoweka na kuishi kwa Mwajuma jambo lilimsababisha awe Malaya kama Mwajuma.

**Jedwali na. 4.4: Muhutasari wa dhamira za ukombozi zilizotafautiana katika riwaya ya *Kusadikika* na *Vuta N'kuvute***

| Na | Dhamira | Kusadikika | Vuta N'kuvute |
|---|---|---|---|
| 1 | Elimu | Uwanasheria | Ya kawaida/ madarasa |
| 2 | Upendo | Zaidi juu ya nchi | Mapnzi na ndoa |
| 3 | Busara | Imesheheni | Wahusia wengi hawana |

**Chanzo:Kutoka katika ya *Kusadikik*a na *Vuta N'kuvute* 2017**

## 4.11 Hitimisho

Kwa kuhitimisha ni kwamba, hakika kila kazi ya fasihi lazima itafautiane na kazi nyengine na ndio inayoonesha upekee baina ya mtunzi mmoja na mwengine. Si hiyo tu, tafauti hizo pia hujitokeza kulingana na mabadiliko ya kijamii wakati msanii anapoitunga kazi yake. Mfano, katika "*Kusadikika"* iliyotungwa miaka ya hamsini ilielezea zaidi juu ya utawala wa kurithishana na "*Vuta N' kuvute*" iliyotungwa miaka ya tisiini ilielezea juu ya utawala wa kikoloni. Hii ni kwa sababu, waandishi wote wawili waliathiriwa ni mazingira yaliyowazunguka katika nyanja za kisiasa, kiuchumi na kijamii ama kiutamaduni.

# SURA YA TANO

# MUHUTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii ni sura ya mwisho ambayo imejumuisha muhutasari, hitimisho na mapendekezo.Ni sura iliyojigawa katika sehemu tatu muhimu ambazo ni sehemu ya kwanza muhutasari, sehemu ya pili hitimisho na sehemu ya tatu mapendeezo ya mtafiti yanayohusiana utafiti husika.

## 5.2 Muhutasari

Utafiti huu ulihusu mada isemayo : *«Kuchunguza dhamira ya ukombozi katika riwaya ya Kusadikika na Vuta N'kuvute : Utafiti linganish* ». Uligawanywa katika sura tano ambazo ni :

### 5.2.1 Sura ya kwanza unahusu utangulizi kwa ujumla

Vipengele vilivyojadiliwa ni utangulizi, usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti (lengo kuu na malengo mahsusi), maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, vikwazo vya utafiti na utatuzi wake, mipaka ya utafiti,muundo wa utafiti na hitimisho.

Katika utafiti huu, mtafiti aliongozwa na lengo kuu moja na malengo matatu mahsusi, lengo la kwanza ni lengo kuu ambalo lilikua ni « *kuchunguza dhamira ya ukombozi katika riwaya ya Kusadikika na Vuta N'kuvute* »na malengo matatu ni malengo mahsusi ambayo yalikua ni (i) Kubainisha dhamira za ukombozi katika riwaya ya *Kusadikika* ii) Kubainisha dhamira za ukombozi katika riwaya ya *Vuta N'kuvute* iii) Kulinganisha na kulinganua dhamira za ukombozi katika riwaya ya *Kusadikika* na *VutaN'kuute*. Vile vilemaswali ya utafiti nayo yamejadiliwa kama ifuatavyo :-

i) Ni dhamira zipi za ukombozi zilizojitokeza katika riwaya ya *Kusadikika*? ii)Ni dhamira zipi za ukombozi zilizojitokeza katika riwaya ya *Vuta N'kuvute* iii)Ni ulinganishaji na ulinganuaji upi uliojitokeza katika riwaya ya *Kusadikika* na *Vuta Nkuvute*?

### 5.2.2 Sura ya pili ilihusu mapitiyo ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia

Kwa upande wake sura hii ilihusu utangulizi, ufafanuzi wa istilahi,nadharia zilizotumika ambazo ni nadharia ya Mwitiko wa Msomaji na na dharia ya Fasihi Linganishi na kumalizia na hitimisho.

### 5.2.3 Sura ya tatu-Mbinu za utafiti

Sura hii inachambua vipengele vifuatavyo: Utangulizi,maana ya mbinu za utafiti, eneo la utafiti, uteuzi wa eneo la utafiti, sababu za uteuzi wa eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji,sampuli ya watafitiwa,sampuli lengwa,ukusanyaji wa data (data za awali na data za upili) mbinu za ukusanyaji wa

data, mbinu ya maktabani,mbinu za kukusanya data za awali/msingi,usomaji wa makini,mbinu za kukusanya data za upili,upitiaji wa nyaraka,mbinu za uchambuzi wa data,mkabala wa kimaelezo,usahihi wa data za utafiti,maadili ya utafiti, baadaye ni hitimisho .

**5.2.4 Sura ya nne -Ukusanywaji ,uchambuzi na uwasilishwaji wa data**:Katika sura hii,mtafiti ameanza nautangulizi, historia ya mtunzi wa riwaya ya Kusadikika ambayo imejumuisha uwandishi wake,falsafa yake,kifo na kumbumbu yake.Baada ya hapo akaingia katika historia ya mtunzi wa *Vuta N'kuvute*.Vile vile kuna muhtasari wa riwaya ya *Kusadikika*, muhutasari wa riwaya ya *Vuta N'kuvute*,ubainishaji wa dhamira za ukombozi zilizomo katika Kusadikika,ubainishaji wa dhamira za ukombozi zilizomo katika *Vuta N'kuvute*,ulinganishaji wa dhamira zilizofanana katika riwaya hizo,utafautishaji wa dhamira zilizotafautiana na riwaya teule baadaye ni hitimisho.

### 5.2.5 Sura ya tano -muhutasari, hitimisho na mapendekezo

Kwa kuhitimisha mada isemayo «*Kuchukuza dhamiza za ukombozi katika riwaya ya Kusadikika na Vuta N'kuvute : Utafiti linganishi* » Kwa kurejelea data zilizokusanywa na uchambuzi wake riwaya hizi zinafanana zaidi kuliko kutafautiana kwa mujibu wa namna ukombozi ulivyowakilishwa kulingana na sababu kadhaa zikiwemo za kisiasa,kijamii,kielimu,kiutamaduni na kifikra.Kadhalika utafiti huu unaongozwa na malengo mahsusi ya utafiti ambayo kwa muhtasari yameainishwa kama ifuatavyo :-

## 5.3 Lengo mahsusi la kwanza

« *Ni kubainisha dhamira za ukombozi katika riwaya ya Kusadikika* ». Lengo hili linaongozwa na suali la msingi lisemalo: *Ni dhamira zipi za ukombozi zilizojitokeza katika riwaya ya Kusadikika ?*

Mtafiti alibaini kuwa kuna dhamira mbali mbali za ukombozi zilizosheheni katika riwaya hii ambazo ni chachu ya maendeleo ya jamii na taifa kwa ujumla.Pia dhamira hizo zinapatikana kupitia matendo ya wahusika ambao ndio aliowaumba mtunzi kutegemeana na uwasilishwaji wake. Hivyo katika riwaya hii, mtafiti aligundua kuwa kuna dhamira tafauti zikiwemo ujasiri, uzalendo, upendo, umoja, ushirikiano, kujitolea muhanga, hekma na busara ambayo zinaaminika fika endapo zitafuatwa na kutekelezwa basi dhulma na uonevu utaondoka na kupata maendeleo stahiki.

### 5.3.2 Lengo Mahsusi La Pili

Lengo hili lina mada isemayo « *Kubainisha dhamira za ukombozi zilizomo katika riwaya ya Vuta N'kuvut* » Lengo hili linaongozwa na swali lisemalo: *Ni dhamira zipi za ukombozi zilizobainishwa katika riwaya ya Vuta N'kuvute?*

Katika kufafanua hili mtafiti anathibitisha zaidi kuwa dhamira za ukombozi zimekithiri kwa kiasi fulani ndani ya riwaya teule. Dhamira hizo zinaonesha matendo yaliyowazi katika jamii nyingi. Miongoni mwa dhamira hizo ni ujasiri, utetezi wa haki za binaadamu, ushujaa, subra na uvumilivu, upendo, umoja na ushirikiano na nyingi nyenginezo. Kwa kuzihusisha na dhamira zilizotolewa katika riwaya ya *Kusadikika* zinaonekana kulingana kwa kiasi kikubwa kuliko kutafautiana.

### 5.3.3 Lengo Mahsusi la Tatu

Hili lina mada isemayo : « Kulinganisha na kulinganua dhamira za ukombozi zilizomo katika riwaya ya *Kusadikika* na *Vuta N'kuvute* ». Lengo hili linaongozwa na mswali lisemalo : Ni ulinganishaji na ulinganuaji upi uliojitokeza katika riwaya ya *Kusadikika* na *Vuta N'kuvute*.

Kwa mujibu wa mtafiti alivyoichambua kazi yake anaweza kusema kuwa kuna mlingano /mfanano mkubwa ndani ya riwaya hizi kuliko ulinganuaji kwani dhamira zote alizoaijadili anaziona zinahusu lengo moja ambalo ni ukombozi.Kwa mfano katika riwaya ya *Kusadikika* kuna dhamira kama ujasiri, subra, uvumilivu, umoja, ushirikiano, busara, hekma, kujitolea muhanga na nyenginezo.Halikadhalika riwaya ya *Vuta N'kuvute* zinaonekana dhamira kama ujasiri, ushujaa, subra, uvumilivu n.k.

## 5.4 Hitimisho

Kwa kuhitimisha ni kwamba dhamira za ukombozi zimesheheni mno katika riwaya ya *Kusadikik*a na *Vuta N'kuvute* pia nimuhimu mno,ni dhamira yenye msukumo mkubwa katika jamii halisi.Ukomnbozi ni dhamira nyeti inayoeleweka na kukubalika katika kufanikisha maendeleo ya jamii.Mtu yoyote anayetafuta ukombozi au maendeleo yake ni budi kuachana na mambo mengine mfano.Mfano, Karama na wajumbe wake sita walizalilishwa na kutiwa gerezani ila hawakurudi nyuma hadi wakapata mafanikio. Si hivyo tu, Denge licha ya kupendwa mno ni Yasmin hadii akataka amuoe ila hakuwa na haja ya kuoa bali fikra zake zote zilikuwa katika kutafuta uhuru yaani ukombozi wa nchi yake na jamii kwa ujumla.Vile vile hakutaka ajira licha ya elimu yake aliyokuwa nayo. Ukombozi huu unasawiri maisha ya zama za Wakoloni walivyowatesa Waafrika na namna Waafrika hao walivyojitahidi

katika kupambambana na Wakoloni hao ili kutetea haki zao.Vile vile katika riwaya hizo, umeelezewa ukombozi katika hali ya kisasa yaani ukombozi juu ya Waafrika wenyewe. Pamoja na kupatikana kwa uhuru wa nchi yao, bado wanadhalilishwa ni Waafrika wenye wao, hivyo kunahitajika kufanya bidii zote ili kufanikisha maendeleo yao ya kisiasa, kiuchumi, kijamii, kifikra na kiutamduni.

## 5.5 Mapendekezo

Kiukweli kabisa kufanya kazi ya utafiti ni kazi ngumu mno hivyo inahitaji muda, subra, uvumilivu na utulivu wa kutosha hadi kufikia kile cha utafiti huo. Utafiti huu umehusu *« Kuchunguza dhamira za ukombozi katika ya Kusadikika na Vuta N'kuvute: Utafiti linganishi»*Kwa hakika ni imani kubwa ya mtafiti kwamba ametimiza hamu yake aliyokuwa nayo kwa kuzingatia malengo na maswali ya utafiti kama yalivyodhihirishwa hapo awali. Kwa upande mwengine, mtafiti ameona kuwa kuna umuhimu mkubwa wa kutoa mapndekezo yake katika maeneo yafuatayo.

### 5.5.1 Mapendekezo kwa Taaluma

Wataalamu mbali mbali wakiwemo walimu, watunga mitaala na wengineo ni vyema kuitilia nguvu lugha ya Kiswahili hasa upande wa fasihi.Vile vile wawashajihishe wanafasihi kutumia muda woa mwingi katika kutuga riwaya kwani mara nyingi inatoa historia au taarifa ya jambo lililofichikana katika jamii.

### 5.5.2 Mapendekezo kwa Serikali

Serikali ina wajibu mkubwa wa kuhamasisha umuhimu wa kufanya tafiti za kitaaluma katika Kiswahili hasa eneo maalumu la fasihi ili kuendeleza na kukiimarisha pamoja na kupeleka mbele maendeleo ya elimu nchini na duniani kote

kwa kukielimisha.Hali hiyo itasaidia kukikuza na kukitunza Kiswahili pamoja na kuipa hadhi serikali na hali ya nchi kwa kuipatia tija na mahitajio.Pia kuongeza idadi ya wasomi na wataalamu wa ngazi za juu ya elimu upande wa Kiswahili hasa upande wa fasihi.Vile vile ni vyema kwa serikali kuwa makini na imara kwa kutoa nafasi za makongomano na warsha mbali mbali za Kiswahili zaidi upande fasihi kwa sababu fasihi ni kiyoo cha jamiihivyo kupitia kiyoo hicho kitazalisha wasanii mahiri, shujaa na hodari wenye weledi nzuri katika kutunga maigizo yao ambayo yatafichua maovu yaliyojificha.

### 5.5.3 Mapendekezo kwa Jamii

Jamiii ina dhima kubwa ya kujifunza Kiswahili kwani ndio lugha ya Taifa. Kiswahili hasa fasihi inatoa ajira kwa wasanii au watunzi wa kazi hiyo na kupata mahitaji yao ya lazima.

## 5.6 Hitimisho

Kwa kumalizia utafiti huu ni kwamba mtafiti amefanikisha kubainisha dhamira ya ukombozi katika riwaya ya *Kusadikika* na *Vuta N'kuvute.* Dhamira hiyo, imejitokeza katika maeneo mbali mbali ambayo ni ya kisiasa, kiuchumi, kielimu, kijamii kifikra. Maeneo yote yaliyoainishwa hapa yamelenga kwenye kujikomboa na mifumo yote ya kimaisha ambayo mwanadamu analazimika kuyapata katika uhai wake. Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ndio iliyotumika kufafanulia dhamira hizo. Hii ilimsaidia mtafiti vya kutosha juu ya ufafanuzi wa dhamira alizobainisha. Vile vile, mtafiti aetumia Fasihi Linganishi ambayo ilimsaidia kulinganishakazi yake kwa kufananisha na kutafautisha dhamira hizo katika riwaya zilizotajwa hapo awali. Kwa kiasi kikubwa, mtafit aliona kuwa zinafanana kutokana na kuwa zote zinalenga katika

maudhui moja ya kumkomboa mwanadamu kutoka hali duni kwenda katika hali inayoridhisha ya kimaisha. Kwa upande mwengine, mafiti aliona kuwa zinatafautiana kwa kiasi fulani kutokana na uwasilishwaji wake. Mfano Riwaya ya *Kusadikika* ni kongwe kuliko *Vuta N'kuvute*, hivyo maudhui yake yanaendana kulingana na wakati aliouandikia kazi yake.

## MAREJELEO


Adam, J. & Kamuzora, F (2008).Research Methods for Business and Social Studies, Morogoro:

Akida,j(2015) Upande Wa Pili Wa Riwaya Teule Za Shafi Adam, Dhamira zilizofichama,Shahada ya Uzamili Chuo Kikuu Huria Cha Dar es salam

Ambrose, B (2014) Kuchunguza dhamira za kisiasa katika riwaya za Shaaban Robert:Mfano wa Kusadikika na Kufikirika,Tasnifu ya uzamil;Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Babbie, E. (1999). The Basics of Social Research. Belmont: Wadsworth Publishing Company. Bassnett, S. (1993) Comparative Literature: A Critical Introduction. Oxford: Blackwell.

Boldor, A. (2003).Perspective on Comparative Literature. A Thesis of Master of Arts in The Interdepartmental Program in Comparative Literature, Louisiana State University, USA.

Bryman, A. (2004). Social Research Methods, New York: Oxford University Press.

Buliba, S. (2014).*Misingi ya Nadharia na Utafiti*, Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) Limited.

Cresswell,J(1998)*Research D esing Qualitative Quantative and Mixed Methods Approaches,Long Angels*:SAGES Publication.

Enon, J. C. (1998). *Education Research Statistics and Measurement*. Kampala: Makerere University Press.

Jilala, H. (2016). Misingi ya Fasihi Linganishi: Nadharia, Mbinu na Matumizi, Dar es Salaam: Daud Publishing Company

Fakih, S (2017*) Kutathmini Mabadiliko Ya Usawiri Wa Mwanamke Katika Riwaya Ya Utengano Na Kamwe Si Mbali Tena*.Tasnifu Ya Uzamili:Chuo Kikuu Huria Cha Dar-es-salam.

Haji, H. G. (2006), *Kamusi ya Kitumbatu*, Express Printing Services, Zanzibar.

Haji, H. G. (1994), *Kimbunga*, TUKI, Dar es Salaam.

Kezi lahabi,E(1976),*Shabarn R Mwandishi wa Riwaya*,Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Cha Dar er salam.

Kezilahabi, (1983), "*Utunzi wa Riwaya na Hadithi Fupi*" *Fasihi*; *Makala ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III*, TUKI, Dar es Salaam.

Khatibu, M. S. (1983), "*Kuli*", *MULIKA*, Na. 15, Pp. TUKI, Dar es Salaam.

Kiango, S. D. (1987), "*Tone la Mwisho*" *MULIKA*, Na. 19, pp. TUKI,Dar es Salaam.

King'ei, G. K. (1987), "*Usanifu wa Lugha katika Uandishi wa Ebrahim Hussein*" *MULIKA*, Na. 19, pp. TUKI, Dar es Salaam.

Kitula, K. na Ahmed, N. (2008), "*Kamusi ya Methali; Toleo jipya*". East Africa Educational Publisher, Nairobi.

Kombo,D and Tromp,D(2006) *Proposal and Thesis Writing Introdaction Pauliness* Publication Afirica:Kenya.

Kothari, C. R. (2004), “*Research Methodology; Methods and Techniques* (2nd ed)”, New Age International (P) Ltd, New Delh

. Kyando,L(2013) *Majina Sadifa ya Wahusika Katika Kusadikika na kichwamaji* Katika Mulika Namba 3 TATAKI Chuo Kikuu Cha Dar es Salam

Madumulla, J. S. (2009), “*Riwaya ya Kiswahili”*, Mture Educational Publishers Ltd, Dar es Salaam.

Maneno, S. K. (h.t), *Uchambuzi wa Mashetani na Masaibu ya Ndugu Jero*, The Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi.

Mapuri, O. R. (1996), *Zanzibar The 1964 Revolution: Achievements and Prospects*, TEMA Publishers Company Ltd, Dar es Salaam..

Margaret, K. (1997), “*Uchambuzi wa Visiki”Makala ya Kiswahili ya Kitaifa*, Kenya Kiswahili Association, Nairobi.

Masebo, J. A. na Nyangwine, (2010), *Kiswahili*, *Kidato cha 3 na 4*, Nyambari Nyangwine Publishers, Dar es Salaam.

Mgeni, A. (1983), “*The Element of Mystery in the Novel of Mohamed Said Abdalla*” *Kiswahili* Vol. 50, no. 2, pp, TUKI, Dar es Salaam

Mjema,R(1990)*Kusadikika* Katika Mulika Namba 22,Dar es  salam TUKI

Mlacha, S. A. K. na Madumulla, J. S. (1991), *Riwaya ya Kiswahili*, Dar es Salamm University Press, Dar es Salaam.

Momany((2001)*Nadharia Ya Uchanganuzi Nafasi Katika Mtazamo Wa Kike Na Uhakiki Wa kifasihi Kiyoo Cha lugha Idara ya Kiswahil*i.Chuo Kikuu Cha Daressalam .

Mohamed, M. (2003), *Malenga wa Mrima Nimerudi*, Oxford University Press, Dar es Salaam.

Mohamed, S. A. (2010), *Nyuso za Mwanamke*, Longhorn Publishers Ltd, Nairobi.

Mulokozi, M. M. na Kahigi, K. K. (1979), *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*, Tanzania Publishing House, Dar es Salaam.

Mussa, F. K. (2007), *"Mchango wa Suala la Ukombozi katika Riwaya za Shafi A. Shafi"*, *Tasnifu katika Shahada ya Kwanza ya Elimu na Sanaa*, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.

Ndungo, C. W. na Mwai, W. (1991). *Kiswahili Studies Part Two*: *Misingi ya Nadharia ya Fasihi Ya Kiswahili*. Nairobi: University of Nairobi.

Njogu, K. na Wafula, R. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: The Jomo Kenyata Foundation.

Njogu, K. & Chimerah, R. (1999).*Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation Ltd.

Ponera,A(2010)*Athari za Ufutuhi Katika Nathari za Sharban Robert,Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Dodoma*:Dodoma Tanzania

Saleh,K(2015) *Fasihi Simulizi Katika Riwaya Za Shaban Robert:Mifano Kutoka Adili na Nduguze Wasifu wa Siti Bint Sadi*. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

Salim, M(2015) *Kuchunguza Ufasihi Simulizi Unaojitokeza Ndani ya Hadithi za Kusakika na Adili na Nduguze*,Tasnifu ya Uzamili,Chuo Kikuu Huria Tanzani

Sengo .T.Y.Y(1975)Shaban Robert uhakiki na machapisho yake:Dar-e-salam:Longman Tanzania limited

Semzaba, (1997), OSW 208, *Tamthilia ya Kiswahili*, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam.

Senkoro, (2011), *Fasihi*, KAUTTU Limited, Dar es Salaam.

Shaban R ,(1991)*Kusadikika* Dar es salam Mkuki na na Nyota Publishers

____________(1980)*Adili na Nduguze* (chapa ya 10)Dar es salam Tanzania Publishing House

Shafi, A. S. (2013), *Mbali na Nyumbani*,Longhorn Publishers (T) Ltd, Dar es Salaam.

-------------- (2003), *Haini*, Longhorn Publishers (K) Ltd, Nairobi.

--------------- (1999), *Vuta N'kuvute*, Mkuki na Nyota, Dar es Salaam.

--------------- (1979), *Kuli*, Longhorn Publishers (T) Ltd, Dar es Salaam.

---------------- (1978), *Kasri ya Mwinyi Fuad*, Vide˜Muwa Publishers Ltd, Nairobi.

Shella, A. M. (2012), "*Athari ya Uhalisia Mazingaombwe kwa Msomaji katika Kuzielewa Kazi za Kifasihi za Said Ahmed Mohamed", Tasnifu katika Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili.* Chuo Kikuu Cha Dodoma.

Simiyu, W. F. (2011), *Kitovu cha Fasihi simulizi*, Serengeti Bookshop, Mwanza.

Songoyi, E. M. and Masele, E. J. (2013), *Prose and Poetry; A teaching manual*, Heritage Tanzania Educational Limited, Dodoma.

Walibora, K.W. (2010). *Uhalisia na Uhalisiamazingaombwe*: *Mshabaha kati ya Dunia Yao na The Tin Drum.* Swahili Forum 17 (2010): 143-157

Wamitila, K. W. (2004), "*Fantansy and Realism in the Modern Kiswahili Novel: A Critical Look at "Babu Alipofufuka*", *Kiswahili* Vol. 67, TUKI, Dar es Salaam.

--------------------- (2002), *Uhakiki wa Fasihi; misingi na vipengele vyake*, Phoenex Publishers Ltd, Nairobi.

------------------- (2003), *Kamusi ya Fasihi; Istilahi na Nadharia*, Focus Publications Ltd, Nairobi.

Yin, R. K. (1994).*Case Study Research: Design and Methods*, (2nd eds.) Thousands Oaks California: SAGE Publishers.

Zepetnek, S. (1998).*Comparative Literature: Theory, Method, Application*: Amsterdam: Atlanta Rodopi.